BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	Mhe.	Zubeir Ali Maulid	-	SPIKA
2.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
5.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
6.	Mhe.	Issa Haji Ussi Gavu	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
7.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais
10.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
11.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais
14.	Mhe.	Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais
15.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani

16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**

34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**

85.	**Mhe. Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe. Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg. Raya Issa Msellem	**-**	**Katibu**

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 25 Juni, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti: Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2018/2019. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 216

Miongozo ya Utekelezaji wa Sera ya Ugatuzi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Hivi karibuni Serikali imeanza utekelezaji wa Sera ya Ugatuzi kwa sekta ya afya, elimu na kilimo katika hatua za msingi. Jambo hili jema limeanza na changamoto kadhaa kutokana na kukosekana kwa miongozo ya utekelezaji tokea mwanzo.

Je, ni lini miongozo ya utekelezaji wa Sera ya Ugatuzi itapelekwa katika sekta husika ili kuondoa matatizo mbali mbali yanayojitokeza hivi sasa katika utekelezaji wa Sera ya Ugatuzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 216 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba utekelezaji wa dhana ya ugatuzi umeanza na baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji ufumbuzi wa kudumu ili azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kupeleka madaraka kwa wananchi iweze kufanikiwa. Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri pia kwamba kukosekana kwa miongozo mbali mbali ya kutoa mwelekeo wa namna gani ugatuzi utekelezwe ilikuwa ni miongoni mwa changamoto ambazo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ ilikabiliana nazo. Katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo, miongozo ifuatayo imetayarishwa:-

i. Muongozo wa uhamisho wa watumishi kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

ii. Muongozo kuhusu uundaji wa Sekretarieti za Mikoa na ile ya Serikali za Mitaa pamoja na majukumu yake.

iii. Miongozo ya Mipango ya Fedha utayarishaji wa Bajeti inakamilishwa.

iv. Muongozo wa majukumu ya kisekta yaliyogatuliwa.

v. Muongozo wa maeneo ya Sera na Sheria za Kisekta na yale ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ na kufanyiwa mapitio.

Mhe. Naibu Spika, miongozo iliyokamilika itasambazwa kwa wahusika wote mara tu baada ya kuchapishwa ambapo kwa sasa ipo kwa Mchapaji Mkuu wa Serikali. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa majibu aliyotoa na amekiri kuwa miongozo yote haijakamilika ya miaka mitano. Kwa mfano suala la fedha ndio *issue* na ndio mzizi wa fitna. Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, tumeingiza fedha mwanzo kabla ya mipango na utakubaliana na mimi hatujawa tayari kuanza na mipango baadae ndio zije fedha.

(b) Je, wananchi wategemee nini wakati fedha zimepelekwae wakati mipango haijawa tayari, hii hadithi itakuwa ni sawa sawa na kuku na yai lipi lililokuja mwanzo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kama nilivyokuwa nishakuelezea utaratibu huu wa ugatuzi umeanza mapema lakini mpango huu ieleweke kwamba ni mpango huu ni mpya na kwa kuwa ni mpya kuna mambo mengi ambayo changamoto nyingi ambazo zipo na tunaendelea nazo kuzitafutia ufumbuzi lakini sambamba na hilo nilitaka nikwambie Mhe. Jaku Hashim Ayoub hatutegemei kwamba yote baada ya ugatuzi tu kwamba mambo yote yatakuwa yamekamilika kwa wakati mmoja. Bali moja ni kwamba tunaenda hatua kwa hatua na hatuwezi tukafikia mafanikio ya haraka haraka kama vile kama hatufuati utaratibu huu ambao nimeuelezea kwa upya wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo kwa namna ambavyo tunakuwa tunaendelea ndio hivyo hivyo ambavyo ndivyo tutakavyobaini kama ni changamoto ama ni mapungufu tutaendelea kuyapatia ufumbuzi wakati tukiwa tunaendelea.

(b) Lakini vile vile kuhusiana na masuala ya kukamilisha kuingiza masuala ya madeni na mambo mengine. Mhe. Naibu Spika, wakati wa hotuba yetu ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ tuliweza kufafanua sana

kwa kina zaidi. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Jaku aendelee kuzipitia zile *Hansard* ambazo tumeweza kuzielezea ili kusudi kwamba kujikumbusha tu kidogo kwa yale ambayo tumeweza kuelezea wakati ule wa bajeti na haya pia ni miongoni mwa mambo ambayo yaliweza kujitokeza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyoo vyote na kumtakia kheri Mtume wetu Mohamed (SAW). Nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini nimpe swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kwa kuwa ugatuzi ni kama ni sera mpya ambayo serikali imeona ina haja ya kuifanyia maelekezo na mambo mengi ambayo yapo swala langu linakuja kwamba:-

(a) Ninaweza kusema ni mwaka mmoja sasa hivi tokea ugatuzi uanze mpaka sasa hivi ni mwaka mmoja. Je, kuna maelezo yoyote hata ya akiba tu ambayo yanaweza kuonesha kwamba ugatuzi unaleta faida au unaleta hasara katika suala hili.

(b) Ni kwamba katika miongozo ambayo unaiona katika sekta nyingi ambazo kama wewe ukiwa ni Waziri katika maeneo hayo ya Serikali za Mitaaa, una maeneo ya afya, uvuvi. Je, ni vipaumbele gani ambavyo unahisi vitakuwa viliongezeka zaidi au vitaongezeka zaidi kuliko pale kila mmoja alipokuwa katika wizara yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kupeleka madaraka kwa wananchi ililenga ni kuboresha upatikanaji wa huduma ili wananchi zile kero zao ambazo zimekuwa zikiwakabili za kila siku kasi zaidi ya kupata ufumbuzi wa zile kero zao ziweze kupatikana. Naomba nitoe ufafanuzi katika suala hili kwamba kutoa majibu ya nyongeza kwamba tokea tumeanza ugatuzi mwaka mmoja sasa hivi ni kwamba yapo mafanikio mengi ya wale ambayo tumeweza tayari kuanza kuyapata.

Moja ni kwamba ukiangalia katika vituo vya afya takriban vingi sana tumeweza kuvifanyia ukarabati na tumeweza vyengine kuvitembelea, lakini vile vile skuli za msingi tayari tumeweza kupeleka fedha ambazo katika kufanya miundombinu tumeshaanza kubadilisha badilisha katika baadhi ya maeneo na hata majengo yetu yale ambayo ya kutoa huduma. Kwa mfano Halmashauri zetu nazo tumepeleka kasma ili kuweza kuona kwamba tunaweka mazingira ambayo yataendana sambamba na saula la ugatuzi. Kwa hivyo nataka niseme tu kwamba Mhe. Naibu Spika, mafanikio makubwa tayari tumeshaanza kuyapata na tunaendelea kusema kwamba ugatuzi utakuwa ni ufumbuzi wa kutatua kero nyingi kwa wananchi wetu kama vile ambavyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipanga.

(b) Lakini vile vile matarajio mengine au vipau mbele ambavyo Mhe. Suleiman Sarahan Said ametaka kujuwa naomba niseme kwamba vipaumbele vipo vingi na ambavyo vitatokana na mipango yale ambayo ya Halmashauri zetu pamoja na wahusika hawa ambao wamegatuliwa

kuweza kulipanga hili jambo kwa kweli litakuwa ni mambo ya kupanga kwa kila mwaka itakuwa vitakuwa vikibadilika, lakini kubwa zaidi kipaumbele chetu ni kwamba ni kuhakikisha kwamba huduma kwa wananchi zinawafikia kwa wakati lakini vile vile na kwa uhakika zaidi . Kwa hivyo Mhe. Sarahan niseme tu kwamba ugatuzi utakuwa ni ufumbuzi au utaleta ufanisi katika mipango yetu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 257

Serikali kuyapa Kipaumbele Maeneo ya Kihistoria Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kudumisha historia ya nchi na kukuza Utalii na kuongeza mapato ya Taifa, yapo mambo ya kale na sehemu za makumbusho ambayo yanajulikana lakini bado hayajapewa kipaumbele katika matunzo na kuyalinda maeneo hayo mengine kuanza kuvamiwa na pia kuyaharibu na kupoteza uhalisia wake.

(a) Je, Wizara inafahamu maeneo yote ya kihistoria na sehemu za makumbusho na mambo ya kale yaliyopo Zanzibar.

(b) Je, maeneo hayo yamepimwa na kupewa hati.

(c) Je, maeneo yanafaa kuwekewa uzio au hayafai, na kama yanafaa kwa nini hayaekewi uzio.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali Nam. 257 kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kwanza nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuifanyia ukarabati na matengenezo TV ya Zanzibar au *ZBC*. Pili napenda nimpongeze Mkurugenzi wa *ZBC* kwa juhudi yake ya makusudi kwa kutafuta kila mbinu na kufanya jitihada ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanajionea Kombe la Dunia ambalo michezo hii inaendelea wakati huu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali 257 la Mhe. Suleiman Sarahan Said lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Serikali inafahamu maeneo mengi ya kihistoria yaliyokwisha kuletwa kwake. Si rahisi kwa Serikali yoyote duniani kusema inajua maeneo yote kwa vile kila uchao orodha huongezeka. Hata hivyo kwa faida ya Baraza lako hili Tukufu naomba niseme kwamba tumeorodhesha maeneo 85 ya kihistoria Unguja na Pemba.

(b) Mhe. Naibu Spika, kati ya maeneo manane (8) tayari yamepimwa lakini hayajapatiwa hatimiliki. Maeneo saba (7) tayari yamepatiwa hatimiliki. Aidha kwa mwaka huu

tunarajia kupima maeneo manne (4) na kupata hatimiliki za maeneo kumi na mbili (12) ukijumlisha pamoja na yale ambayo yamekwishapimwa lakini hayajapatiwa hatimiliki.

(c) Mhe. Naibu Spika, uvamizi ni tatizo kubwa kwa maeneo ya kihistoria hususan kwa shughuli za uwekezaji na wakati mwengine za maendeleo. Kuzuia jambo hili kwanza nikuchukua bidii ya kuelimisha, kuimarisha Sera na Sheria zetu. Hata hivyo baadhi ya maeneo yamewekewa uzio na nguzo za mipaka na kazi hii itakuwa endelevu kadri itakavyoruhusu. Miongoni mwa maeneo yaliyowekewa uzio na nguzo za mipakani ni Chuini, Mangapwani (*Slave Chamber*), Shakani n.k. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale katika melezo yake lakini katika swali la nyongeza nitauliza kama ifuatavyo:-

(a) Tokea Mapinduzi ya 64 ndio suala hili la mambo ya historia limejitokeza kutokana na sehemu mbali mbali ambazo zinaonekana ni miaka karibu 40 mpaka tuseme 45, lakini mpaka sasa hivi umesema katika masuala yako ni kwamba masuala haya yanaibuka ibuka hujayafikia mwisho. Ni vigezo gani unavyotumia mpaka ukaweza kulipata eneo hili kwamba nalo linafaa kuwa la kihistoria.

(b) Unajisifiaje kwamba una maeneo karibu 85 ambayo ni ya kihistoria lakini huna hatimiliki

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, vigezo ambavyo tunavitumia kuna Sheria ambayo inatuongoza ya umiliki wa maeneo haya ya kihistoria au pia na uhifadhi wake wa maeneo haya ya kihistoria ni Sheria Nam. 11 ya 2002 ndio Sheria ambayo inatuongoza kutumia vigezo wa kujua maeneo hayo ya kihistoria.

(b) Mhe. Naibu Spika, bado napenda nijibu kwamba tuna kila sababu ya kujivunia kwamba tunayo maeneo yetu ya kihistoria pamoja kuwa kati ya maeneo haya kama nilivyojibu katika swali mama, yapo baadhi ya maeneo bado hayajapatiwa hatimiliki na tumeshayapima. Kwa kuwa mchakato huu tunahitaji kwamba tushirikiane na taasisi husika au baadhi ya taasisi tushirikiane kwa pamoja tuhakikishe kwamba maeneo haya tunayapatia hatimiliki na tuendelee kujivuna kwamba bado maeneo haya ya kihistoria yapo Zanzibar na wageni wanapokuja bado wanaendelea kuyatambua na kuyakagua maeneo haya. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu ya serikali yenye kigugumizi na mzunguko mkubwa naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa inaelekea maeneo mengi yamepimwa lakini hayajapata hitimiliki na inaelekea kikwazo cha bajeti. Je, ni kiasi gani cha fedha mwaka 2018/2019 kilichotengwa kwa sababu ya kuweza kupimia maeneo hayo.

(b) Na kwa sababu Mhe. Naibu Waziri amekiri kwa sababu ugumu uliopo maeneo mengi yamepimwa lakini bado hakujafanyika chochote na serikali hii ni moja na wizara hii kwa nini isizungumze na wizara nyenziwe ikaweza kumlipa kidogo kidogo kama inavyosema Katiba ya Zanzibar Kifungu 43(5)

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mohammed Said (Dimwa) swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimjibu Mhe. Dimwa kwamba serikali haina majibu yenye ukakasi, serikali mara nyingi inakuwa inatoa majibu ya usahihi ya uhakika na wakati mwengine tunatumia hata sheria kama mlivyoeleza mwanzo kwamba tuna sheria ambazo zinatufanya tuwe na umiliki na kujivunia kwa maeneo yetu haya ya kihistoria.(*Makofi*)

   Lakini Mhe. Spika, naomba pia nimjibu Mhe. Dimwa kwa kipindi ambacho kimepita cha mwaka wa fedha tumetengewa jumla ya Shilingi bilioni moja kwa ajili ya matengenezo ya maeneo yetu ya kihistoria.

b) Nalichukua swali lake kwamba bado tutaendelea na kushirikiana na taasisi husika kuhakikisha kwamba maeneo haya ya kihistoria tunayapima na kuyapatia hatimiliki na ikiwezekana wakati mwengine pale panapostahiki kulipa fedha tutaendelea kuwalipa kwa sababu kila mwaka inapofika wakati wa bajeti tunatengewa fedha hizi kwa ajili ya shughuli hii. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar:Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha wahai na wazima, lakini pia kunipa fursa kuuliza swali la nyongeza.

Nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyajibu lakini naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza

a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ameeleza kwamba maeneo 85 yameorodheshwa ya kihistoria Unguja na Pemba. Nilitaka kujua je, eneo la Msikiti Chooko liliopo Kaskazini Pemba nalo ni miongoni mwa maeneo hayo lipo. Lakini pia vile vile nikitaka kujua maeneo muhimu yaliyomo katika msitu wa Ngezi kama yale makaburi ya Masharifu ambayo kuwa yanahistoria. Je, nayo yameorodheshwa katika sehemu hizo ili watalii wetu watakapokuja kuweza kutoa historia nini yalitokea hapo.

b) Kwa kuwa Wizara yake inashuhulika na Mambo ya Kale na mambo haya yana umuhimu wake. Je, maswali gani ambayo kwa jitihada gani wamechukua kuona kwamba ile michezo ya asili ambayo ilikuwa ikiwaleta wananchi karibu katika kukaa kujenga udugu na ufahamiano zaidi ya ng'ombe, kama vile Kirumbizi, ngarawa hii wanachukua juhudi gani kuona kwamba wanaiendeleza ili wananchi waweze kukaa pamoja katika kujenga uhusiano mwema.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza lenye kipengelee (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, katika maeneo ambayo nimeyataja Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi maeneo haya aliyoyataja ya Msikiti Chooko yaliyopo Tumbe lakini pia na msitu wa Ngezi kwa kuwa ni eneo ambalo lina historia nalo, pia ni maeneo kati ya maeneo ambayo tumeyapima tayari nayo yamo katika orodha hiyo.

b) Kuhusu michezo ambayo ameitaja najua kwamba michezo hii pia inavutia watalii wakati wanapokuja wakiona zile tamaduni zetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda nikiri kwamba bado tutashirikiana na Wizara ya Vijana ili kuona kwamba michezo ile yote ya asili na wao ndio wasimamizi wakuu bado tutaendelea kuwaambia wananchi wetu waendeleze na tamaduni zetu ili kuhakikisha kwamba utamaduni wetu haipotei.

Nam. 19

Kukithiri kwa Utoro kwa Skuli ya Ukutini Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Skuli ya Ukutini Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kukithiri vitendo vya utoro kwa wanafunzi.

(a) Nini chanzo cha kukithiri kwa utoro katika skuli hiyo.

(b) Je, hatua gani madhubuti zimechukuliwa kukabiliana na vitendo hivyo vya utoro.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwalikilishi swali lake Nam 19 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Wizara inakiri kuwa upo utoro wa wanafunzi katika Skuli ya Ukutini. Utoro mkubwa wa wanafunzi katika skuli hiyo ulijitokeza wakati wa msimu wa mavuno ya karafuu ya mwaka huu kutokana na baadhi ya wanafunzi kushiriki katika uchumaji wa zao la Karafuu au kuokota mpeta. Hali hiyo ilichangiwa na vishawishi vya makundi rika na baadhi ya wazazi kutofuatilia nyendo za watoto wao wanapokuwa skuli. Hivi sasa hali ya

utoro wa wanafunzi katika skuli hiyo umepungua na ninawashauri sana wazazi wafuatilie nyendo za watoto wao wanapokwenda skuli ili kukomesha vitendo vya utoro.

(b) Wizara ilifanya mazungumzo na Walimu Wakuu na Kamati za Skuli, Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wawakilishi na Madiwani katika kulipatia ufumbuzi tatizo hili. Pia, ziara za Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Mkoani katika skuli mbali mbali zilizomo katika Wilaya zimesaidia sana katika kuwaelimisha wazazi na Wajumbe wa Kamati za Skuli kutatua tatizo hil.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu marefu ya Mhe. Naibu Waziri ambapo taratibu za Kanuni zetu zinatukataza Kanuni ya 37, kujibu kwa urefu na wizara hii inaongoza sana kwa kujibu maswala kwa urefu.

a) Je, kwa nini Wizara hamrudishi utaratibu kama ule wa zamani wa kufunga skuli ili wanafunzi wakenda kuokoa zao la karafuu ambalo ndio uti wa mgongo wa nchi hii.

b) Naibu Waziri unatoka Mkoani, Wilaya ya Mkoani. Je, umechukua hatua gani kukutana na walimu wa skuli hii na wazee pamoja kuwa unasema humu katika majibu Mwakilishi wa Bunge na lini kikao hichi cha Wawakilishi na Wabunge kilikaa siku gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Utaratibu wa kufunga wa skuli ili kuokoa zao la karafuu baadhi ya nyakati ulikuwepo, lakini baadae baada ya kuonekana kwamba nguvu kazi ya kuchuma karafuu bila ya kuhusisha wanafunzi na karafuu hizo zikaweza kuchumwa kwa ukamilifu wake baada ya kupatikana nguvu kazi hiyo (baada ya watu kuchangamkia fursa hiyo), ikaonekana hakuna haja ya kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hizi na ndio maana hata katika bima ambayo imewekwa kwa ajili ya kuwalinda wachumaji karafuu watoto hawakuingizwa kutokana na kwamba hakuna sababu hiyo

(b) Ni kweli mimi ni Mwakilishi kutoka Jimbo la Mkoani na nimekuwa nikifanya ziara pamoja na wenzangu pia kuzungumzia makusudi suala hili la utoro, tumezungumza na Kamati za Skuli mara nyingi, tumezungumza na Masheha mara nyingi tumezungumza na tumezungumza na baadhi ya viongozi ili kuona tunapambana vipi na suala la utoro. Katika mazungumza hayo tulipata kuelekeza kwamba katika hatua ya awali walimu wakuu waorodheshe majina ya wanafunzi pamoja na wazazi wao wapi wanatoka na wapi wanakaa, baadae wawaite wazazi wawakumbushe wawaelimishe, ikiwa itashindikana hatua hiyo pia tukaeleza kwamba taarifa za hawa wanafunzi watoro na wazazi wao wazipeleke kwa Mkuu wa Wilaya na kwa kweli baadhi ya maeneo Wakuu wa Wilaya walifanya kazi kubwa ya kuwarejesha baadhi ya wanafunzi ambao walikuwa wametoroka na kuhusu tarehe gani vikao hivi vilifanywa kwa sasa sikumbuki.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza lakini nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu fasaha ya swali mama.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri anakiri kwamba kuwashirikisha watoto katika kazi hizi ni makosa na swali na uchumaji wa karafuu ni suala endelevu linafanyika kila baada ya msimu Fulani. Je, wizara imechukua hatua gani au imejipanga vipi ili tatizo hili la utoro wa wanafunzi lisiendelee kutokea katika msimu inayokuja.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Rashid Shamsi swali lake kama ifuatavyo.

Suala la utoro ni suala ambalo ni la kielimu, kukiwa na msimu kusiwe na msimu linaweza likajitokeza. Kwetu sisi basi Wizara ya Elimu kama nilivyosema hapo awali kwamba tutaendelea kushirikiana na wazazi kupitia Kamati za Skuli, Masheha, Madiwani, Wawakilishi na Wabunge ili kuwaeleza wazazi umuhimu wa kutilia mkazo masuala ya kwenda skuli vijana wetu. Hili suala tunaendelea na tutaendeleza na matokeo mazuri yameaanza kupatikana kwa kushirikiana na wadau mbali mbali katika suala hili.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Bismillahi Rahmani Rahim. Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali maswali yenye (a) na (b)

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri mshaanza kazi ya kukaa na wazee kwa kuweza kuelimisha watoto waweze kusoma na kuacha kufanya kazi ambazo kama zilizotajwa na kuna wazee ambao wasikivu lakini kuna wazee ambao watakuwa sio wasikivu. Sasa kwa wale wazee ambao si wasikivu mtawachukulia hatua gani za kisheria ili waweze kukomesha suala la kuwafanyisha kazi watoto na kukosa elimu.

(b) Kwa kuwa walimu siku za maskuli za Serikali zikiwa wazi wanalipwa nauli lakini wakauliza kwa nini siku ambazo skuli zikifungwa wanafunzi hawendi lakini wao walimu wanaambiwa waende maskulini, lakini zile fedha za nauli hawalipwi. Sababu ni zipi Mhe. Naibu Spika, naomba nipate jibu kwa niaba ya walimu wa Chaani na walimu wote Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri majibu. Mhe. Naibu Waziri swali la kwanza (a) nafikiri linahusiana moja kwa moja na swali la (b) sio la msingi. Kwa hivyo lakini kama unaweza kumjibu mjibu Mhe. Mjumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu ni Wizara ya taaluma mara nyingi hupenda kwanza kuwaelimisha wazazi umuhimu wa elimu na wanapopata kuelewa umuhimu wa elimu wanakwenda hatua ya pili wanapata mwamko, wanapopata mwamko wanakwenda hatua ya tatu ya kuweza kutoa maamuzi sahihi. Mara nyingi huwa tunapenda kuwaelimisha, lakini pale ambapo tutashindwa kuwaelimisha kwa maana ya kwamba pale ambapo watashindwa kufuata maelekezo Sheria ya Elimu ya 1982 ipo na inalazimisha mzazi kumpeleka mtoto wake skuli na asipofanya hivyo hatua za kisheria zipo. Lakini kwanza tunaendelea kuwaelimisha ikishindikana tutachukua hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika: kuhusu swali la (b) Mheshimiwa una maelezo yoyote. Sasa useme hapo kwamba utajibu japokuwa kwa maandishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ulisema kwamba halihusiani na swali mama.

Mhe. Naibu Spika: Halihusiani na swali la msingi lakini limeulizwa na Mjumbe wajibu wako ku- *respond* kwa kusema kwamba utalijibu kwa maandishi au alete jibu la msingi..

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Aah! tunaweza tukalijibu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu swali lake (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli wakati skuli zinapofungwa baadhi ya walimu wanatakiwa kwenda katika maskuli yao lakini wanakwenda kwa zamu, inawezekana katika wiki mbili za kufungwa skuli ama wasende kabisa au akenda siku moja. Sasa niseme kwamba endapo mwalimu atapangiwa kwenda skuli wakati skuli zimefungwa, akenda siku moja au mbili hizo Wizara ya Elimu italizipa.

Lakini si kwa walimu wote ambao wanaweza kupewa hapana, wale ambao wamepangiwa kazi, na Mhe. Mwakilishi ni shahidi aangalie wakati skuli zimefungwa na aende skuli kama atakuta mwalimu.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana tunaendelea

Nam. 225

Kuwatambua na Kuwathamini Wanamichezo Nchini

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Kwa kuwa michezo, utamaduni na sanaa, huitangaza nchi kwa fani hizo, na pia wanamichezo hujulikana nchi mbali mbali kwa fani zao hizo na kwa kuwa tuna wanamichezo mbali mbali nchini, ambao wameitangaza nchi yetu ndani na nje ya nchi.

Je, Wizara ina mpango gani wa kukutana nao wanamichezo hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 225 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa kutambua mchango wa wanamichezo katika jitihada za kuitangaza nchi yetu, Wizara imejipangia utaratibu wa kukutana na wanamichezo wa aina mbali mbali wakiwemo wanamichezo wakongwe pamoja na wasanii ili kubadilishana mawazo na kutoa

michango yao katika jitihada za kuendeleza michezo na sanaa kwa ujumla. Aidha, kupitia vikao hivyo pia Wizara inapata fursa ya kufahamu changamoto zinazowakabili na kushauriana utatuzi wake.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ijapokuwa fupi sana jibu lake lakini nampongeza sana kwa jibu hilo.

Swali langu Mheshimiwa kwa bahati nzuri tulifanya ziara katika sehemu mbali mbali katika Kamati ya Maendeleo, ya Wanawake Habari na Utalii kwa kuwajali na kuwathamini wazee wetu ambao wanamichezo kwa michezo mbali mbali, wasanii mbali mbali na tulikutana nao na moja ambalo lilituuma katika mioyo yetu hali mbali na duni sana katika maisha yao waliyokuwa nayo. Je, kwa kuzingatia hilo Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri yupo tayari kufanya ziara maalum kuwatembelea baadhi ya wale wagonjwa ambao hivi sasa tunawahesabu kama wagonjwa akina Bi. Fatma Issa, Bi. Njiwa pia kuna Bi. Mwanaacha na wengineo utakapokwenda kuwatembelea Mheshimiwa huruma zitakujia.

Je, wizara ina mpango gani kwa kufanya ziara makusudi kuwatembelea hao na wengine ambao hali zao duni sasa hivi katika maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi kama Naibu Waziri nipo tayari lakini nakuomba sana tushirikiane katika ziara hii pamoja na wewe uwepo, twende pamoja mguu kwa mguu kwa ajili ya kuwatembelea wanamichezo hawa shukrani.

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea kuna swali jengine la nyongeza niliona watu wamesimama Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza lakini kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Naibu Waziri labda katika kuendeleza hilo kwa mwaka 2017/2018.

a) Wizara imekutana na wanamichezo na wasanii wangapi wakogwe.

b) Kama alivyotangulia kusema Mhe. Ali Suleiman Ali kwa kuwa wanamichezo na wasanii hao wakongwe wengine wana maradhi mbali mbali. Je, katika kipindi hichi cha 2017/2018 wizara imewasaidia kimatibabu na kifedha wasanii gani na wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, karibuni tu tumepitisha bajeti na tumesema ni wasanii wangapi kwa sasa hivi ile hesabu yake imenipotea nitaomba nimjibu kwa maandishi suala hili na vile vile kuhusiana na pesa za matibabu pia nitaomba nimjibu kwa maandishi. Ahsante sana nashukuru.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa utaratibu wetu kutokana na *Order paper* ambayo tuliyonayo tumetakiwa tuwe na swali la 186 ambao ni la Mhe. Asha Abdalla Mussa. Sasa kutokana na dharura waliyonayo Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake Wizara ya Biashara na Viwanda swali hili nitalisogeza mbele ambalo ni swali 35 ili waweze kufanya, wana shughuli na Mhe. Rais ili waweze kwenda kufanya shughuli yao halafu baadae tutaendelea.

Nam. 36

Utekelezaji wa Sheria Nam. 4 ya Mwaka 1983

Mhe. Ali Khamis Bakar – Aliuliza**:**

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweze kuuliza swali Mhe. Naibu Spika naomba swali kangu namba 36 jilibiwe.

Kitengo cha vipimo na mizani kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya Mizani na Vipimo ya mwaka 1983. katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2017 ilifanya ukaguzi Unguja na Pemba na ilikusanya jumla ya Tshs. 23.7 milioni.

(a) Je, mligundua nini katika ziara hii ya ukaguzi.

(b) Je, Sheria namba 4 ya mwaka 1983 ni ya zamani, ni lini Sheria hiyo itafanyiwa marekebisho.

(c) Ni mara ngapi kwa mwezi Wizara inafanya ukaguzi ili kubaini bidhaa mbovu madukani na kukagua mizani hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo) swali lake Nam. 36 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Kitengo cha Mizani na Vipimo ni moja ya Vitengo vilivyopo ndani ya Wizara ya Biashara na Viwanda na ukuzaji masoko katika Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar. Kitengo hichi kimeundwa na kinafanya kazi zake kwa Sheria Nam. 4 ya Mizani na Vipimo ya 1983. Miongoni mwa majukumu yanayosimamiwa na Kitengo hichi kwa hapa Zanzibar ni pamoja na:-

i) Kuhakikisha Zanzibar inatumia vipimo vinavyoendana na *"System of International Unit (S.I. Unit)"*

ii) Kuulinda umma na kusimamia mwenendo sahihi wa matumizi ya vipimo vya biashara;

iii) Kuweka uwiano ulio sahihi baina ya pande mbili za biashara (Muuzaji na Mnunuzi);

iv) Kusimamia uhalali kwa kiasi cha bidhaa zinazoingizwa nchini pamoja na zile zinazozalishwa katika viwanda vyetu ili kuisaidia Serikali katika makusanyo halisi ya mapato yake.

Kazi kubwa inayofanywa na Kitengo cha Vipimo kwa hivi sasa ni kuhakikisha vipimo vyote vinavyohusiana na matumizi ya biashara hapa Zanzibar ili kuhakikisha vinaendana na usahihi unaotakiwa.

a) Katika kazi zake za kawaida, kuanzia mwaka wa fedha ulioanzia Julai hadi kufikia Disemba 2017, Kitengo cha Vipimo kilifanya kazi za uhakiki wa Mizani zinazotumiwa na wafanyabiashara wa madukani pekee. Katika ukaguzi huo ulikagua jumla ya Mizani za kawaida 1451, Mizani 2 *(Weight Bridge*) zinazotumiwa kupimia uzito wa mizigo inayopakiwa katika magari makubwa, matangi ya kuhifadhia mafuta 4, pamoja na mita kubwa 3 za kuuzia mafuta *(Flow Meter)* katika Bohari. Katika utekelezaji wa kazi hizo tuligundua jumla ya mizani zisizo sahihi zipatazo 169 ambazo zilizuiwa kutumika (kupimiwa) hadi yalipofanyika marekebisho yake na kuhakikiwa tena.

b) Wizara ya Biashara inakubali kuwa Sheria ya Mizani na Vipimo imekuwa ya muda mrefu na haiendani na hali halisi ilivyo hivi sasa. Wizara ya Biashara na Viwanda imejipanga kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kuifanyia kazi Sheria hii pamoja na Kanuni zake ili kukidhi mahitaji ya hali halisi ya sasa.

c) Kama nilivyotangulia kusema hapo awali, kazi za ukaguzi wa mizani zinazotumika katika mazingira ya biashara ni kazi ya kila siku kwa Kitengo cha Mizani na Vipimo ambapo pamoja na ukaguzi wa mizani pia Kitengo kinafanya kazi za uhakiki wa vipimo vyengine vya kibiashara kama ilivyoelezwa hapo awali.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa amekiri kwamba kuna mizani 169 ambazo hazina usahihi wa kuwapimia au ya vipimo ambavyo wanatakikana watu hawa wapime kwa mujibu wa sheria. Kwa kuwa Dini yetu ya Kiislamu inasisitiza *"Almudhan Haki"* kwamba jambo hili lina usawia baina ya anayenunua na anayeuza. Je, mizani hizi 160 ambazo mumezigundua ni hatua gani za watu hawa ambazo mumezichukua za kisheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba atambuwe kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Biashara kupitia Kitengo cha Mizani na Vipimo kwamba kazi hii ni endelevu na ni kazi ya kila siku. Kilichotufanya tugundue ni kwamba tunafanya kazi yetu ya kuzitafuta hizo mizani ambazo zipo na hazifanyi kazi kwa usahihi kwa mujibu wa sheria, ndio maana tukagundua mizani 169 hazipo sahihi, tumezizuwia na hatuziruhusu kufanya kazi mpaka tukazihahiki tena. Kwa hivyo sasa hivi zimezuwiwa na haziruhusiwi kufanya kazi mpaka zikahakikiwe tena.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika nashukuru kwza kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri lakini nilikuwa na swali la kumuuliza kwa kuwa kitengo mumesema mumekagua hizo mizani 1,400 za kupimia chakula tu na bila shaka utaratibu huo uko tokea zamani sambamba na ukaguzi wa *Weight Bridge* na *Flow Meter* ambazo zinahitaji kukaguliwa mara kwa mara. Lakini nilitaka nijue kupitia kitengo chako ni mizani ngapi ambazo mumezihakiki ambazo mnajua zinapaswa kukagukiwa mwaka hadi mwaka sambamba na *Weight Bridge* na *Flow Meter* ambapo ukitilia maanani kwamba *Weight Bridge* ni kipimo muhimu kinachotakiwa kitumike ili kuzuwia magari yasibebe uzito mkubwa ambao unaweza kuziharibu barabara zetu. Ni *Weight Bridge* ngapi ziko Unguja, ngapi ziko Pemba, ngapi zimekaguliwa na ngapi hazikukaguliwa sambamba na *Flow Meter,* ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya mizani za kawaida ambazo tumezikagua kama nilivyosema ni 1,451. Mizani mbili *Weight Bridge* na za kupimia mafuta ni nne. Kwenye swali langu (a) linajieleza wazi wazi kitu gani tumekagua na vingapi na hatua gani tumechukua.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika. kwa kunipa fursa hii nimpongeze kwa majibu mazuri mwanana Mhe. Naibu Waziri alojibu, lakini katika majibu yake alisema kwamba wizara inafanya ukaguzi wa kila siku ni kazi ya kila siku katika kuhakikisha maduka yanatimiza wajibu wao.

Je, Mhe. Naibu Waziri serikali yetu mpaka hivi sasa ina mpango mzima wa kuzuwia udhalilishaji na vitendo ambavyo kuwa ni vibaya vinavyofanyiwa wananchi wetu. Je, unaelewa kwamba kuna bidhaa zinazoingia nchini ambayo kuwa ni peremende (pipi) ndani ya karatasi ile kuna matangazo ya kuonesha watu jinsi ya kulawitiana. Vipi, unaliekewa hilo na kama hulielewi kitengo chako kitachukua hatua gani kuwatafuta wafanyabiashara hawa ambao kuwa wanaingiza bidhaa hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mheshimiwa arejee swali sijalisikia vizuri tafadhali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe rejea swali.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nchi yetu tunapinga udhalilishaji na vitendo vibaya ambavyo kuwa vimeenea vya kulawitiana, lakini kwa kuwa sasa hivi kuna wafanya biashara wameingiza peremende (pipi) ndani yake ile karatasi kuna picha ya

kuhamasisha vitendo hivi tunavyovipinga. Je, kitengo chako kinaelewa hili, kama hakielewi inachukuwa juhudi gani ya kuvitafuta nani wanazoingiza bidhaaa hizi nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza la kwamba katika peremende (pipi) zinazoingizwa nchini kuna vitendo vya udhalilishaji vimetiwa picha zake wakati kuwa serikali yetu inapinga vitendo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba swali hilo tumelichukua na tunalifanyia kazi *with succefully* ahsante.

Nam. 255

Uendelezaji wa Viwanda vya Nguo na Soda Zanzibar

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza**:**

Katika Hotuba ya Bajeti. ya mwaka 2017/2018, Waziri alieleza kwamba mazungumzo yanaendelea kuona kwamba Kiwanda cha Soda na Kiwanda cha Nguo cha Cotex tutaweza kuviendeleza na kurudi katika hali yake au kuweza kufanya uzalishaji mwengine.

a) Je, Wizara imefikia hatua gani.
b) Je, Wananchi wategemee nini juu ya viwanda hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Musa Foum Mussa swali lake Nam. 255 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Serikali inatambua na kusisitiza haja ya kuona raslimali za kiwanda cha Soda na *Cotex* zinatumika kwa shughuli za uzalishaji kama ilivyokusudiwa au zitumike kwa shughuli nyengine zenye tija zaidi kuliko ilivyo sasa. Juhudi za kuona matumizi bora ya raslimali hizo zinasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa Kiwanda cha Soda na Wizara ya Biashara na Viwanda inaongoza mazungumzo na mmiliki wa Kiwanda cha *Cotex*.

b) Mwisho wa mazungumzo yanayoendelea inategemewa kupatikana kwa mwafaka wa matumizi bora ya raslimali za viwanda hivyo viwili ambayo vinapelekea kupatikana nafasi za ajira na mapato zaidi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa viwanda hivi vimekaa muda mkubwa sana havifanyi kazi na kwa kuwa kila mara tunaambiwa mazungumzo yanaendelea. Je, wananchi wategemee muda gani ili viwanda hivyo vitaanza kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza naomba kumjulisha kwamba viwanda vinavyozungumzwa hapa ni viwanda viwili. Kiwanda cha *Cotex* na Kiwanda cha Soda. Kiwanda cha Soda kinafanya kazi kikamilifu. Hivi nilivyokuwa nakuija huku nilipishana na magari manne ya soda yakitoka Maruhubi Kiwanda cha Soda kuja zake huku, hiyo ni kuonesha kama kinafanya kazi. Lakini Kiwanda cha *Cotex* mheshimiwa ni kiwanda kinachomilikiwa na mtu binafsi na ni mali yake na mpaka hivi leo analipa kodi zote za serikali zinazotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile mmiliki wa kiwanda hicho analipa kodi kama inavyotakiwa na hakifanyi kazi serikali ipo mazungumzoni katika kuhakikisha kiwanda kile kinatumika kwa matumizi mengine, lakini ni mali yake mwekezaji na bado analipa kodi zote lakini kwa vile hakifanyi kazi serikali ina mazungumzo naye kuhakikisha kuona kiwanda kile kinatumika kwa matumizi mengine.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya serikali lakini naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

a) Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri umekiri kuwa Kiwanda cha Soda kinafanya kazi zake kama kawaida na kiliacha kazi zamani. Huoni kama unalidanganya Baraza la Wawakilishi sasa hivi.(*Makofi*)

b) Ikiwa upo tayari kufatana na mimi mara tu baada ya kumaliza kipindi cha maswali na majibu tukaone uhalisia wenyewe kama kinafanya kazi au laa.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Nafikiri Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) Mhe. Naibu Waziri nafikiri hili halina haja ya kujibu isipokuwa amesema kwamba mkaone. Kwa hivyo mimi ningeshauri mkitoka hapa sio leo kwa sababu una shughuli nyengine, lakini mwende mkaone kama hicho kiwanda kinafanya kazi au hakifanyi kazi, nafikiri ndio lengo lake hasa la kwamba anataka mwende pamoja.

Mhe. Hamza kaa kitako sijamaliza kusema *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Waziri umemfahamu Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa)

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, nimemfahamu na nipo tayari kufuatana naye tukaone Kiwanda cha Soda pale, tutakwenda asiwe na wasi wasi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii nilitaka kupiga utaratibu lakini umeninyanganya umenipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Kanuni zetu za Baraza zinatukataza kulidanganya Baraza la Wawakilishi na kulidanganya Baraza la Wawakilishi ni kosa kubwa sana, anapaswa Mhe. Naibu Waziri aliombe radhi Baraza.

Sasa kwa kuwa nina uhakika kwamba suala alilojibu Mhe. Naibu Waziri kwamba Kiwanda cha Soda kinafanya kazi ni suala ambalo sio sahihi na kwa sababu Baraza hili wananchi wanalisikiliza. Huoni kwanza Mhe. Naibu Waziri akafuta ile kauli yake ya kusema kwamba Kiwanda cha Soda kinafanya kazi ili wananchi waone kwamba Mawaziri wao wanafanya kazi na wanajibu maswali kwa uhakika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma hilo swali umeniuliza mimi sio Mhe. Naibu Waziri, ilivyoelekea kama unanielekezea mimi sio Mhe. Naibu Waziri. Sasa mimi nafikiria kwa sababu Mheshimiwa unasema afute kauli lakini Mheshimiwa hajui pengine kama hicho kiwanda kinafanya kazi au hakifanyi kazi, hana taarifa kwa alivyojibu hana taarifa ya kwamba hakifanyi kazi. Sasa ndio maana nikashauri nikasema kwa sababu Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kashauri waende atakaporudi sasa atafuta hiyo kauli yake aliyoisema kwamba hakifanyi kazi, nafikiri twende hivyo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa ruhusa naomba nimfahamishe Mhe. Mjumbe tunapouliza maswali tutumie Kiswahili kilicho sahihi. Naomba kusema nimeulizwa je, kinafanya kazi au hakifanyi kazi. Ninarudia kusema Kiwanda cha Soda kinafanya kazi lakini hakizalishi. *(Makofi)*

Sasa hiyo ndio hoja.

Wajumbe: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Hakizalishi kinafanya kazi lakini kinafanya kazi na soda zinauzwa kama kawaida na magari yanapelekwa na ushahidi ukienda pale Kilimani awamu utazikuta soda zinatoka Maruhubi zinapelekwa pale.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Kiswahili hicho ambacho kimeulizwa nafikiri kila mmoja anakifahamu kinafanya kazi, maana yake kwamba je, kinazalisha? Ndio maana ya Kiswahili. Mheshimiwa usijizonge mimi nafikiria sana kwamba ukubali na ushauri wa Mhe. Mohammed Said Mohammed mwende mkatizame kiwanda kama hakifanyi kazi halafu mengine yatafuata baadae. Naomba ukubali tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa maelekezo yako mazuri, vile vile nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake na nimshukuru Mheshimiwa muuliza swali hili Mhe. Mohammed Said Mohammed na nyongeza ya Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa swali liliulizwa na majibu ya Naibu Waziri yalitolewa, kwa hivyo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe watuachie suala hili tulifatilie na kama ulivyoagiza Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Mwakilishi watakwenda wakaone hali halisi halafu taarifa kamili iletwe hapa ili Waheshimiwa Wajumbe waipate na wananchi kwa ujumla wake.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 186

Upungufu wa Matrekta ya Serikali

Mhe. Asha Abdalla Mussa – Aliuliza:

Wananchi wa Zanzibar asilimia 90 ni wakulima wa mpunga na unapofika wakati wa kilimo kutumia matrekta ya serikali ambapo ni bei nafuu, lakini kumekuwa na changamoto kubwa juu ya matrekta hayo hali inayowafanya wananchi hao kutumia gharama kubwa kutafuta matrekta binafsi au kukosa kulimiwa kwa wakati.

(a) Je, kwa Unguja na Pemba kuna matrekta mangapi ambayo yanafanya kazi.

(b) Je, ni lini tatizo hilo litaondoka ili wananchi waondokane na kadhia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.186 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, matrekta yanayofanyakazi kwa Unguja na Pemba kwa msimu huu wa mpunga 2017/2018 ni 47 (Unguja 33 na Pemba 14).

(b) Mhe. Naibu Spika, katika jitihada za kuondoa tatizo la upatikanaji wa matreka, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeingia Mkataba na Kampuni ya MAHINDRA&MAHINDRA kutuletea matreta 100 ambayo yatakidhi mahitaji ya Zanzibar. Kwa muda huu tayari matrekta mapya 20 na yale 10 kutoka Ubalozi wa Libya Dar es Salaam yamepatikana na kutumika katika msimu huu wa ukulima wa mpunga. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa hii niweze kumuuliza maswali ya nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kwa mwaka 2017/2018 kuna matrekta 47 na wananchi wetu kwa mwaka huu hawakuweza kulimiwa mashamba yao kwa wakati.

a) Je, ni sababu zipi ambazo zilipelekea wakulima hao wakakosa huduma hii ya matrekta kama matrekta haya yapo.

b) Je, ni utaratibu gani ambao unatumika katika kupeleka kwenye vituo vya kilimo matrekta haya. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Sababu zilizopelekea kuchelewa kwa matrekta kwanza ni hali ya hewa, unajua matatizo ya tabianchi wakati matrekta yako tayari kuingia mashambani wakati mwengine kulikuwa na mvua kubwa sana hayawezi kuingia. Kabla ya hapo kulikuwa na jua kali sana matrekta yalikuwa hayaingii kwa sababu ya ugumu wa ardhi, kwa hivyo kidogo yalichelewa. Pia tatizo kubwa lilikuwa ni kwa wakulima wenyewe hawakujitokeza mapema kutoa zile fedha walikuwa wanasubiri labda kutakuwa na maamuzi mengine ya kupatikana matrekta yale pengine kinyume na yale matajirio ambayo yalikuwepo.

Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi tunapenda kumwambia kwamba kuchelewa kwa kulima mwaka jana kulitokana na sababu hizo tatu ambazo nimezieleza. Pia napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba hali hii ya upatikanaji wa matrekta tutaitatua pole pole. Kwa mwaka huu unaofuata wa 2018/2019 tunategemea kununua tena matrekta mapya 30 ambayo yatasambazwa Unguja na Pemba. Lengo la matrekta 100 hili nililolitaja tunategemea tutakwenda pole pole mpaka ifikapo 2020 tutakuwa tumekamilisha matrekta hayo 100, kutakuwa hakuna tena tatizo la kulima kwa kutumia matrekta na tunategemea wakulima wetu watajitokeza kwa wingi sana kulimiwa kwa matrekta hayo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na mimi nikaweza kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake na kuwapa moyo wakulima wetu kwamba baada ya muda hivi karibuni watakuwa hawana shida tena na matrekta. Mhe. Naibu Spika, lakini kutokana na majibu yake Mhe. Naibu Waziri katujibu kwamba wana mpango wa kuleta matrekta 100, lakini na hiki kipindi cha karibuni watanunua matrekta 30 ambayo yataweza kuwasaidia wakulima wetu walioko Unguja na Pemba.

a) Mimi ningemuuliza Mhe. Naibu Waziri je, wanatumia vigezo gani kuhakikisha kwamba haya matrekta ambayo wataletewa kwa huo msaada wa hilo shirika na haya ambayo 30 watayanunua wao kama wizara. Ni vigezo gani watavizingatia vya ubora na uimara wa matrekta haya kutokana na kuangalia ardhi yetu tuliyonayo hapa, kwa sababu kasema kwamba ardhi inategemea na hali ya hewa. Je, ubora gani watakaouzingatia.

b) Tunafahamu kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hapo nyuma ilikuwa ina matrekta mengi ambayo yalikuwa yanatumika kwa wananchi wetu na matrekta hayo tayari sasa hivi mengi yao ni mabovu hayafanyi kazi. Je, kama wizara itachukua jitihada gani kwa sasa ambapo haya matrekta waliyoagiza hayajafika kuhakikisha kwamba yale ambayo yalikuwepo yanafanyiwa ukarabati na kuweza kufanya kazi ili kuweza kuwasaidia wakulima wetu kulimiwa kila baada ya muda unapofika na kuondokana na ile kadhia ambayo inawakuta wakulima baada ya misimu na kukosa yale mahitaji yanayotakiwa.

   Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwanza umadhubuti wa matrekta kwa sababu duniani kuna kampuni nyingi sana za matrekta ambazo zinauza matrekta. Sasa tumetumia vigezo kwanza vya umadhubuti wa matrekta wenyewe, halafu na hata *economy* namna yanavyotumia mafuta, kwa sababu kuna matrekta mengine yanatumia mafuta mengi kwani mashine zake ni kubwa sana. Kwa hivyo vigezo hivi ndivyo tunavyotumia. Pia tunatumia vigezo aina ya udongo wetu yanaweza yakafanya kazi vizuri kuliko kwengine.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana kwamba matrekta yaliyopo lazima yakarabatiwe. Sasa naomba kumjibu kwamba lengo letu ni kuyakarabati yale matrekta yote ambayo yapo na kama umesikia katika matangazo ya redio hivi karibuni ilikuwa tunataka kupiga mnada matrekta chakavu tumezuia ili tufanye uhakiki kwamba pengine kuna *spares* tunaweza tukazitumia kutoka pale tukaziingiza kwenye matrekta mengine. Kwa hivyo asiwe na wasi wasi Mhe. Mjumbe kwamba ukarabati wa matrekta yaliyopo na hata ukarabati wa matrekta yanayokuja yanapoharibika utakuwa unafanyika ipasavyo, hatutakubali kabisa trekta likae mwaka mzima halijatengenezwa likitoka shambani litafanyiwa *service* ili kuona liko vizuri na kama kitu kimeharibika basi tutakitengeneza ili liweze kufanya kazi kwa msimu unaofuata vizuri zaidi.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wengi wanalima mpunga kwa matrekta na kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri kwamba mwaka huu ilikuwa mvua nyingi wananchi wale walipolimiwa na kupanda mpunga ule umeharibika kwa maji. Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wale.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kweli swali lake zuri kweli wakulima wamepoteza nguvu tunaamini hivyo wamepoteza nguvu na sisi tuna uchungu sana, serikali ina uchungu sana kuona kwamba wananchi wamelima lakini bahati mbaya kutokana na haya matatizo ya tabianchi na mengine mpunga umeharibika. Mimi na Mhe. Waziri tulitembea mabonde yote mpaka Pemba tumefika kuangalia hali hii. Kwa kweli tunasema kwamba tutafikiria namna gani tutawasaidia wale wakulima ambao wamepata mkasa huu wa kuharibikiwa na mazao yao, kwa kweli tunawahurumia sana na tunawapongeza kwa juhudi zao zote walizozichukua na serikali iko pamoja nao.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 250

Uboreshwaji wa Huduma za Matrekta Zanzibar

Ali Khamis Bakar – Aliuliza:

Naipongeza serikali kwa kuiboresha Sekta ya Kilimo kwa kuanzisha Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria Nam.2 ya mwaka 2011, kwa ajili ya kusimamia na kuimarisha shughuli za matrekta na kilimo.

Na kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar alitoa agizo kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuwapatia Wakala huyo jumla ya matrekta (20) kutoka Kampuni ya (Mahindra) ili kuzidi kuongeza nguvu kiutendaji na kuinua hali za wakulima wetu. Na kwa kuwa Wakala huyu alipokea jumla ya matrekta (10) mapya kutoka Ubalozi wa Libya ambayo yameshindwa kufanya kazi mara tu baada ya kufika kutokana kutolewa baadhi ya vifaa huko yalipohifadhiwa.

(a) Je, ni lini vifaa hivyo vilivyoibiwa vitanunuliwa vipya ili kutoa huduma matrekta haya kama ilivyokusudiwa.

(b) Wizara ya Fedha na Mipango ina mpango gani wa kuipatia fungu lake la matumizi (*vote*) kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake Wakala huyu.

(c) Je, lini agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar litatekelezwa ili kufikia lengo na dhamira yake aliyokusidia kwa kilimo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.250 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, napenda kumuarifu Mhe. Mjumbe kwamba vifaa vilivyotajwa kwenye maelezo yake ambavyo viliibiwa wakati matrekta hayo yalipokuwepo Dar es Salaam tayari vimeshanunuliwa na matrekta yote 10 yameshiriki katika kilimo cha mwaka huu wa ukulima wa mpunga 2017/2018.

(b) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeshachukua hatua kama tulivyoahidi suala kama hili liliulizwa katika Baraza hili hili mwanzo wa kipindi cha Baraza hili, walituuliza kuhusu matrekta na suala hili tukalijibu kwamba tutawasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kupata *vote* ya matrekta, na vote hiyo napenda kuwaambia kwamba tumeshaingiza kwenye bajeti hii na wameshapata *vote* yao. *Vote* yenyewe tunaweza kusema kwamba mkifanya *reference* kwenye mabuku yetu yale makubwa ni PL0101 tuangalie hapo maendeleo ya kilimo, halafu kuna huduma za matrekta na zana za kilimo ni SL010105 na huduma za matrekta kwa jamii ni HL01010502.

Kwa hiyo, tunawahakikishia kwamba ile kazi mliyotupa kwamba tufatilie ili *vote* ipatikane tumeshaifanya na Wizara ya Fedha na Mipango tunaishukuru imeturuhusu na hawa wakala wetu wa matrekta Mbweni tayari imeshapatiwa sub vote yake. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

(c) Mhe. Naibu Spika, wizara inaomba kumjuilisha Mhe. Mjumbe kwamba agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kununua

matrekta 20 mapya imeshatekelezwa kama alivyoagiza na maelezo zaidi ni kama yale niliyoyatoa kwamba tuna lengo la matrekta 100 na tutaendelea kununua 30 kwa mwaka huu, tutaendelea kununua hadi yatimie 100 ifikapo 2020. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwanza nimpongeze sana kaka yangu Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yaliyo na ufasaha.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba matrekta haya yaliwahi kuibiwa vipuri hivi na kusababisha kuchelewa kutoa huduma kama ilivyokusudiwa. Naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Je, vifaa hivi ambavyo viliibiwa kwenye matrekta haya ni kabla hamjakabidhiwa vikiwa mikononi mwa kampuni ama kwenye mamlaka ya bandari na kwa kuwa ni muda mrefu suala hili limechukua muda. Je, kwa nini watu hawa mamlaka au kampuni isihusike na kuvinunua vifaa hivi kuweza kukamilisha matrekta haya na badala yake serikali iweze kupata hasara au kuchukua gharama hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi ambalo ametaka kujua vifaa vilivyoibiwa nani *responsible*.

Ni kwamba tuseme ule ukweli kwamba tulichelewa kwenda kuyachukua yale matrekta kwa sababu ambazo pengine za kifedha au vyenginevyo. Lakini kwa sababu matrekta yale yangekaa muda mrefu Mhe. Mwakilishi napenda kukwambia kwamba tulilazimika kuyatengeneza sisi wenyewe kwa sababu yangeendelea kukaa miaka mingi pale yangezidi kupotea vifaa. Kwa hivyo, tumeamua kuyatengeneza sisi wenyewe na matrekta yale tayari tumeshayaleta hapa na tayari yanafanya kazi. Kwa hiyo, jukumu la kuyatengeneza matrekta yale na kwenda kuyachukua Dar es Salaam lilikuwa letu sisi na kuyatengeneza pia tumeyatengeneza wenyewe. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu aliyojibu Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Kwa kuwa ana mpango wa kununua matrekta mpaka 100 kwa alivyosema ifikapo mwaka 2020, lakini kwa kuwa serikali ina mpango mzima wa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji na matrekta haya ambayo wamepanga ni moja kwa moja haya mengine mashamba yao hayataweza kuingia katika mabonde hayo. Je, kwa nini haifanyi mpango wa kuagiza matrekta ambayo yataweza kutumika katika mabonde ya umwagiliaji maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua ukulima huu wa *irrigation* unakwenda kwa misimu, kuna wakati panakuwa pakavu pale. Kwa hiyo, wakati huo ndio ambao tutayatumia matrekta yale.

Lakini pamoja na kwamba kutakuwa na *irrigation* pia yatakuwepo maeneo ambayo ni ukulima wa juu wa mpunga. Kwa hivyo tutayatumia matrekta yale kwa ukulima wa juu wa mpunga na

mazao mengine yakiwemo pengine wale watakaopanda mahindi, watakaopanda mihogo na mazao mengine ambayo trekta hili litaweza kuingia. Kwa hivyo, lengo letu ni kuendeleza kilimo cha mazao ya chakula, hivyo matrekta haya yatakwenda kwenye ukulima wa mpunga na hata kwenye vipando vya juu mule ambamo mtakuwa mnalimika kwa matrekta.

Nam. 65

Taasisi za Serikali Zinazochelewesha Kulipa Madeni *ZECO*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, hili swali lina mitihani lakini wacha nijibiwe, nipo tayari kusikiliza majibu lakini lina mitihani.

Kumekuwa na kilio cha Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) kuhusu Taasisi za Serikali ambazo zinachelewa kulipa madeni yao ya umeme kwa muda mrefu, tofauti na taasisi binafsi na wananchi ambao wakichelewa kidogo tu wanakatiwa.

(a) Je, ni Taasisi zipi za Serikali ambazo ni wadaiwa sugu wa deni la umeme la *ZECO*.

(b) Kuna hatua gani kabambe za kudai madeni hayo.

(c) Kwa nini taasisi hizo hazikatiwi umeme zinapochelewa kulipa deni.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Taasisi za Serikali zenye madeni ya muda mrefu ni Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*), Jeshi la Polisi Tanzania na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme bado inaendelea na jitihada za mazungumzo na viongozi wa ngazi za juu wa taasisi hizo ili kuzitaka taasisi hizo zikamilishe malipo ya madeni yao.

(c) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inakiri kwamba upo uwezekano wa kuzikatia huduma ya umeme taasisi hizo. Hata hivyo ni dhahiri kuwa kuzikatia umeme taasisi hizo ni hatua ya mwisho ambayo inatarajiwa kuchukuliwa endapo taasisi hizo hazitofikia muwafaka na Shirika la Umeme katika mazungumzo yanayoendelea hivi sasa. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Naibu Waziri kutokujibu swali langu la msingi. Kanuni yetu ya Baraza ya 59 inatukataza humu na Waheshimiwa wanapiga kelele sana kama Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Naibu Waziri nikikupa ushahidi, sina nia ya kumwambia ajiuzulu. Nikuombeni kabla ya kujibu haya maswali yafanyiwe utafiti kwanza. Hawa watendaji wao watafika pahali watatuchonganisha na wananchi kwa majibu namna hii.

Je, atachukua hatua gani nikizitaja baadhi ya taasisi hapa ambazo zinadaiwa madeni sugu, tena na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hapa zimetajwa za Muungano tu, moja tu imetajwa *ZAWA*, zipo taasisi za Zanzibar atachukua hatua gani na humu ndani zimo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza.

Ukiangalia swali lake hakutaka deni la ujumla kwamba labda *ZECO* wanazidai taasisi ngapi, ama kiasi gani wanadai kwa ujumla wake, angetaka hivyo basi tungempatia jawabu. Lakini anachokitaka ni kwamba zile ambazo zimechukua muda mrefu ndicho ambacho tumemwambia *ZAWA* na hizi taasisi ambazo nyengine tumezitaja ndizo ambazo kwa muda mrefu tumekuwa tukizitaja. Lakini kwa ujumla wapo na wengine wanadaiwa lakini wanalipa. Ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwanza taasisi nimezitaja humu katika swali langu la msingi aliangalie.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri kama una majibu naomba uyajibu kutokana na swali linavyoulizwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, lugha aliyotumia ni wadaiwa sugu bado hatuna watu wa namna hii, tunao watu ambao wamechukua muda mrefu lakini hawa ambao tumewataja tuna mazungumzo nao na tumefikia hatua nzuri, wale wengine wanadaiwa lakini wanalipa. Sasa kama kuna kitu sijakielewa basi akiweke wazi.

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea na swali Nam. 174 Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Nam. 174

Kuharibika kwa Pampu katika Vituo vya Maji Safi

Mhe. Asha Abdalla Mussa – Aliuliza:

Imekua desturi kwa vituo vya maji safi na salama Unguja na Pemba mara kwa mara huharibika pampu ambazo matengenezo yake huchukuwa muda hadi kukamilika na kupelekea usumbufu kwa wananchi kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea kuharibika mara kwa mara mashine hizo.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha tatizo hilo halijitokezi mara kwa mara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 174 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mhe. Naibu Spika, sababu zinazopelekea kuharibika kwa mashine za maji mara kwa mara ni uwepo wa:

- Mahitaji makubwa ya maji yanayopelekea mashine kutembea kwa muda mkubwa bila ya kupumzika kunakotokana na kukosekana kwa matangi ya kuhifadhia maji katika baadhi ya maeneo,

- Mfumo huo unatumia msukumo wa maji moja kwa moja *(direct pumping)* kutoka kwenye mashine za kusukumia maji, lakini pia

- Utumiaji wa transfoma za umeme pamoja na wateja wengine kunakosababisha kutokea kwa hitilafu za umeme (*current unbalance*) kunakosababisha mashine kutokutembea vizuri.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia *ZAWA* kwa kuliona hilo imeamua kutafuta msambazaji (*supplier*) atakayeweza kusambaza pampu zenye vifaa maalum zitakazoweza kukinga kuungua pampu mara kwa mara, na kuwa na *guarantee* ya mwaka mmoja wa kusimamia ufanyaji kazi wake ambayo hii itasaidia kwa kiasi kikubwa tatizo la kuungua mara kwa mara kwa pampu zetu. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amejibu kwamba Wizara yake kupitia *ZAWA* wameliona suala hilo lakini pia wameamua kutafuta msambazaji ambaye atakayeweza kusambaza pampu zenye vifaa maalum. Je, msambazaji huyo atapatikana lini lakini pia hizi pampu ambazo zina vifaa maalum zitasambazwa kupitia visima ambavyo vipo hivi sasa au visima vile vitakavyochimbwa baadae. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake la nyongeza.

Ni kwamba tayari huyu msambazaji tunaye nayo ni *REMI* na tuna kampuni ambayo tunachukua hizi pampu India inaitwa *CRI*, tayari sasa tumeshaanza naye hiyo kazi. Ni kwamba tunashirikiananao katika kuzifunga na *guarantee* ya mwaka, ikiharibika ndani ya mwaka mmoja basi wao watakuwa *responsible* kwa hilo. Lakini juu ya lile la visima vingapi ama vipi ambavyo vinakusudiwa kufanyiwa hivi *target* yetu hali itakavyokuwa inaruhusu kwenye visima vyote, lakini tutakwenda kadri kisima pampu inapoungua basi *replacement* yake tunahitaji hiki ndio tuweke hivi kusudi mpaka tumalize hiyo kazi. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniona ukaweza kunipa ruhusa kuweza kuuliza swali la nyongeza. Pia nichukue fursa hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake lakini na mimi nimuulize swali. Kwa kuwa maji ndio uhai wetu na kwa kuwa

yanapokosekana maji tunaoathirika ni wanawake ambao ndio tunaohangaika sana kuyatafuta maji.

Je, ni kwa nini serikali isijikite katika ujengaji wa matangi ili pampu iweze kupandisha maji na baadae ipumzike yasambae maji yale kwa wananchi. Lakini pia katika vituo vyetu hivi upo ulinzi wa kutosha ambao walinzi wanalinda uendaji wa mashine ile katika mzunguko wake wa kupeleka maji, kwamba kukitokea hitilafu yoyote angalau mlinzi yupo katika kituo pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla swali lake la nyongeza.

Umuhimu wa kuwa na ma-*tanks* tunauona na tunaujua na kwa kulielewa hilo ndio maana hata ukizingatia kwenye mradi wetu wa India tumeweka *scheme* saba, kuna matangi saba ambayo tutayajenga katika mradi ule kusudi yaungane na yaliyopo katika kueneza hii huduma. Hatutosita kufanya hivyo kila nguvu itakapoturuhusu kufanya hivyo.

Kwa upande wa ulinzi ni kwamba tumeanzia katika yale maeneo makubwa. Kwa mfano Mtoni, Mwanyanya katika zile chemchem na maeneo mengine tutakwenda taratibu, lakini umuhimu wa kuwa na walinzi katika maeneo yetu ni jambo la msingi na inazingatiwa. Ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona tena ukaweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza tu nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini nimwambie kwamba tunafahamu kuwa hawa wafanyakazi wa usambazaji wa hizi pampu wapo, lakini na hata katika Jimbo la Nungwi hilo tatizo la *tank* pia si tatizo ila tunafahamu kwamba uzorotaji wa matengenezo ya hizi pampu unasababishwa na wizara yenyewe au hawa watu wa *ZAWA.*

Je, kama wizara wanachukua hatua gani au wanawajibu nini wananchi wa Wilaya ya Kaskazini hususan Jimbo la Nungwi kwa kuimarisha hizi pampu ambazo kila siku, kila wakati ni mbovu na kusababisha hali mbaya ya upatikanaji wa maji hususan ndani ya Jimbo la Nungwi. Mhe. Naibu Waziri naomba majibu wananchi wa Jimbo la Nungwi wamechoka juu ya masuala ya maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza.

Kama tulivyosema katika jibu la msingi kwamba hili tatizo la kuungua pampu mara kwa mara *solution* yake ni huyu *supplier* ambaye tunaye sasa na hivi vifaa ambavyo vitaingizwa. Lakini lile la kuchukua muda mrefu wananchi wanaona linachukua muda mrefu lakini inategemea na ile pampu ilivyokuwa imeharibika, ni sawa sawa na gari lako likipasuka mpira tofauti na kuharibika vitu vyengine inategemea na usimlaumu fundi.

Mamlaka ya Maji Zanzibar wanajitahidi kutengeneza na kuchukua muda mfupi kabisa katika kutengeneza huko, kwa sababu wanafahamu ukosefu wa maji unasababisha tatizo sana kwa wananchi wetu. Lakini tuwaombe tu tushirikiane katika kulinda lakini pia tutoe taarifa pale

ambapo inaharibika kusudi watendaji wa Mamlaka ya Maji wafike waweze kutengeneza na huku tunavuta *speed* ya kuhakikisha kwamba tuna-*replace* hizi pampu zilizo bora zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe nadhani mtaona kwamba bado tuna maswali ya kujibu lakini hata hivyo, muda wetu wa maswali na majibu tayari umemalizika. Kwa hivyo maswali mengine yataulizwa kesho tukijaaliwa na wale wote ambao walipata barua za kuwa maswali yao yatajibiwa leo na hayakujibiwa, basi mpango utapangwa kwa ajili ya kuuliza aidha kesho au siku nyengine. Lakini kabla ya kuondoka hapa nataka nimpishe Mwenyekiti aendelee na utaratibu unaofuata, pia naomba kwanza niwakaribishe wageni wetu waliohudhuria hapa leo.

Wageni wenyewe ni wageni wa makundi mawili. Lakini kundi la mwanzo ni wageni wa Mhe. Naibu Spika anayeitwa Mgeni Hassan Juma ambapo wageni hawa ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi.

Wageni wenyewe ni:
1. Ndugu Amin Salmin Amour
2. Ndugu Cassian Gallos Nyimbo

Karibuni sana ndani ya Baraza letu ni faraja yetu nyinyi kuwepo hapa leo. *(Makofi)*

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mhe. Salma Mussa Bilal pamoja na Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis na Mhe. Wanu Hafidh Ameir. Hawa wote ni Wawakilishi wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini Unguja.

Wageni wenyewe ni Makatibu wa Jumuiya ya UWT Mkoa wa Kusini Unguja jumla yao wakiwa ni saba. Wageni wenyewe ni:

1.	Ndugu Stahamili Omar Dendegu	- Katibu wa UWT Mkoa wa Kusini Unguja
2.	Ndugu Zakia Mussa Chum	- Katibu wa UWT Wilaya ya Kusini
3.	Ndugu Sihaba Fadhil Pandu	- Katibu wa UWT Wilaya ya Kati
4.	Ndugu Asha Juma Haji	- Katibu wa UWT Jimbo la Chwaka
5.	Ndugu Atendae Saleh Moh'd	- Katibu wa UWT Jimbo la Tunguu
6.	Ndugu Lela Hamad Makame	- Katibu wa UWT Jimbo la Uzini na
7.	Ndugu Subira Moh'd Ali	- Katibu wa UWT Jimbo la Paje *(Makofi)*

Karibuni sana wote mliohudhuria hapa na sisi tunawapenda sana na tunatamani kila siku muje hapa kuona kazi zetu tunazozifanya ndani ya Baraza la Wawakilishi. Karibuni sana.

Baada ya kusema hayo sasa naona Mwenyekiti hajawa tayari naomba tuendelee mpaka atakapokuja tutaendelea nae. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2018/2019

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Kabla ya kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Waheshimiwa sasa nimpishe Mwenyekiti wa Baraza ili aweze kuja kuendelea na shughuli yetu hii ya leo. Mhe. Mwenyekiti karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mhe. Asha Abdalla Mussa (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti naomba kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Bajeti inayohusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu aliyetujaalia afya na uzima tukaweza kuhudhuria katika Baraza lako tukufu na kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza hili ili kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na Mapitio ya Hali ya Uchumi mwaka 2017 na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018; na Mwelekeo wa Uchumi 2018 na Mpango wa Maendeleo 2018/2019 kama Kanuni ya 94(9) Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016 inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ambao tulishirikiana katika kutekeleza majukumu yetu, pamoja na watendaji mbali mbali ambao tulikutana nao katika kufanikisha majukumu yetu.

Aidha, shukrani za dhati ziwafikie Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambao nao waliwasilisha maoni yao katika Kamati ya Bajeti mnamo tarehe 20/04/2018.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2016) inayohusu Utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu Mambo ya Fedha, katika Kanuni ya 92(3) inaeleza wazi kuwa, Mapendekezo ya Muelekeo wa Mpango wa Taifa yatawasilishwa kwenye Kamati ya Bajeti kabla ya kujadiliwa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti iliwasilishiwa waraka huo na Wizara ya Fedha na Mipango mnamo tarehe 18/04/2018. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 92(4), Kamati ina uwezo wa kuwaalika wadau kuja mbele yake na kutoa maoni yao kuhusiana na Muelekeo wa Mpango wa Taifa na Bajeti ya Serikali, kamati iliitumia fursa hiyo kwa kuwaalika wadau kuwasilisha maoni yao mnamo tarehe 20/04/2018 ambayo yamesaidia sana katika kuipatia ufahamu zaidi kamati na kuendelea kuibua hoja mbali mbali za kibajeti ambazo ni muhimu kwa mustakbali na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Wakati Kamati za Kisekta za Baraza la Wawakilishi zilipokuwa zikipitia Mapendekezo ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kulijitokeza changamoto kadhaa kwa

baadhi ya Kamati hizo, ikiwemo kutofautiana kwa vifungu baina ya vitabu vya Wizara ya Fedha na vitabu vya Sekta husika, hali iliyopelekea baadhi ya Kamati kulazimika kuakhirisha kazi ili kuruhusu Wizara kufanya marekebisho. Changamoto hiyo sio tu imepelekea kuongezeka kwa muda uliopangwa wa kupitia bajeti lakini pia imepelekea kuongezeka kwa gharama za matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa sababu za msingi zinazopelekea mapungufu hayo ni pamoja na muda mchache unaotengwa kwa ajili ya kazi ya utayarishaji wa Bajeti, ikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango kuchelewa kutowa ukomo wa bajeti. Hali ambayo hupelekea kukosekana kwa umakini unaostahiki wakati wa kuandaa bajeti. Aidha, kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara kwa maafisa wanaoandaa bajeti pia ni sehemu ya sababu zinazopelekea mapungufu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Ili kupunguza tatizo hilo, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango iweke mikakati thabiti itakayohakikisha kuwa, matayarisho ya bajeti yanaanza mapema sambamba na kuanza kuzitafutia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza kwa mwaka huu wa fedha, ikiwa ni pamoja na kutoa ukomo wa Bajeti kwa wakati ili kuwapa muda wa kutosha maafisa wa bajeti katika kuandaa bajeti za taasisi zao kwa umakini zaidi. Aidha, Kamati inapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango itenge fedha kwa ajili ya mafunzo ya mara kwa mara kwa maafisa wanaohusika na uandaaji wa bajeti kwa taasisi zote za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa utekelezaji wa pendekezo hili ni mgumu kutokana na changamoto ya uchache wa fedha, Kamati inaishauri wizara iangalie uwezekanao wa kupunguza fedha kidogo kwa kila fungu kwa utaratibu kwa ili fedha hizo zitumike kuwapatia mafunzo maafisa wanaohusika na utayarishaji wa bajeti kwa tasisi zote.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya changamoto mbali mbali ambazo Kamati za Kisekta zinakabiliana nazo, Kamati ya Bajeti pia inakabiliwa na changamoto ambazo kwa uzito wake imeziingiza katika Hotuba hii, ili ziweze kufahamika na kupatiwa ufumbuzi kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa changamoto za Kamati ya Bajeti ni kutokuwepo Sheria ya Bajeti pamoja na Ofisi ya bajeti kwa ajili ya kuisaidia Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu unaonesha kuwa, katika mabunge mengi Kamati ya Bajeti inawekewa Sheria ya Bajeti ambayo inatoa Mamlaka kwa Kamati juu ya kuongeza au kupunguza fedha katika mafungu ya bajeti kutokana na mapendekezo ya Wajumbe na Kamati za kisekta katika mijadala ya Bajeti. Aidha, mabadiliko ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2016 hayajajitosheleza katika kuipa nguvu na kuiwekea utaratibu mzuri wa kazi Kamati hii juu ya kushughulikia masuala ya bajeti. Hivyo, kuna haja pia ya kuzingatiwa umuhimu wa Kamati hii kwa kuekewa misingi madhubuti ya kanuni katika mabadiliko yatakayofanyika ili malengo ya kuundwa kwake yaweze kufikia.

Mhe. Mwenyekiti, Kupitia marekebisho hayo, kumeanzishwa mfumo mpya wa upitishaji wa bajeti pamoja na kuunda Kamati ya Bajeti ambapo kwa sasa bajeti kuu hupitishwa mwisho baada ya mijadala ya wizara zote, tofauti na ilivyokuwa awali. Hata hivyo, mabadiliko hayo hayajawasaidia Wajumbe wako pamoja na Kamati ya Bajeti kuweza kufanya mabadiliko ya

vifungu baada ya Kamati ya Matumizi kuidhinisha. Hivyo, kuna kila sababu ya kujifunza zaidi kupitia mabunge ya nchi mbali mbali, ili dhamira ya kuanzisha mfumo huu iweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya maelezo hayo ya jumla sasa naomba nitumie Kanuni ya 94(9) ambayo inaniwezesha kutoa maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Bajeti. Aidha nitatumia fursa hii pia kutoa maoni juu ya Waraka wa Mapitio ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Uchumi katika maeneo tofauti ya waraka uliwasilishwa mbele ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, Ni matumaini ya Kamati kuwa, maoni yatakayotolewa yatasaidia sana katika kuweka misingi bora ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Uchumi na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa lengo la kuhakikisha utaratibu wa kupitia Bajeti unakuwa shirikishi na wenye ufanisi zaidi, kwa mara ya kwanza Baraza lako tukufu lilipokea Mapendekezo ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Mkabala wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 kupitia Kamati ya Bajeti, na Wajumbe walipata fursa ya kujadili nyaraka hizo muhimu na kwa kina. Hii inaonesha namna Baraza linavyoimarika siku hadi siku kupitia mabadiliko mbali mbali yanayolenga kuleta ufanisi wa Bajeti ya serikali na kuwa bora zaidi.

MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2017 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO (JULAI 2017 – MACHI 2018) NA MWELEKEO WA UCHUMI 2018 NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2017

Mhe. Mwenyekiti, Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2017 yanaonesha kuwa uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2016, ambao ulichangiwa zaidi na Sekta za Huduma, Viwanda na Kilimo. Kamati haijaridhishwa na ukuaji huo, kwa kuwa ukuaji huo bado ni mdogo ukilinganisha na malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020 ya kufikia ukuaji wa uchumi endelevu wa asilimia 8 – 10 kwa mwaka katika kipindi cha miaka kumi.

Mhe. Mwenyekiti, Ongezeko la ukuaji wa uchumi halijaweza kutatua baadhi ya changamoto za wananchi ikiwemo ukosefu wa ajira hususan kwa vijana wenye umri wa miaka 15-24.Vijana wengi wanaendelea kutafuta fursa za kuajiriwa serikalini au katika Sekta Binafsi kutokana na kushindwa kujiajiri wenyewe kunakosababishwa na kukosa mitaji. Hivyo, Kamati inaisisitiza serikali iendelee kupanga mipango madhubuti ambayo italenga kukuza fursa za ajira na uchumi ili kustawisha hali za wananchi.

Mfumko wa Bei

Mhe. Mwenyekiti, Kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini umeshuka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2016. Napenda kuliambia Baraza lako tukufu kuwa, kushuka kwa kasi ya mfumko wa bei bado hakujamsaidia mwananchi, kwani hali halisi inaonesha kuwa, bidhaa za chakula nchini bado zinaendelea kupanda kila siku, kiasi cha kumfanya mwananchi kutumia sehemu kubwa ya kipato anachokipata kwa chakula na kushindwa kujiwekea akiba kwa matumizi mengine.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imefarijika na mkakati wa serikali wa kupunguza kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2018/2019 kwa kutoa punguzo maalum katika ushuru hasa katika bidhaa muhimu kama vile mchele, sukari na unga wa ngano.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuwa bidhaa za chakula ni bidhaa za msingi ambazo kila mwananchi anazihitaji kwa matumizi ya kila siku, imefika wakati sasa kwa Serikali iweke mikakati ya muda mrefu itakayohakikisha uzalishaji wa chakula nchini unaongezeka, kwani athari ya kutopata chakula kwa kiwango kinachostahiki hudumaza nguvu kazi ya nchi, afya na hata maendeleo mengine kwa ujumla.

Uingizaji wa Bidhaa

Mhe. Mwenyekiti, Uingizaji wa bidhaa nchini unaojumuisha bidhaa kutoka nje ya nchi na uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umeimarika, ambapo kwa upande wa bidhaa zinazohaulishwa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umefikia thamani ya TZS bilioni 206.5 mwaka 2017 kutoka thamani ya TZS bilioni 138 mwaka 2016. Kwa upande mwengine uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umepungua kutoka thamani ya TZS 84.7 bilioni mwaka 2016 na kufikia thamani ya TZS 33.6 bilioni mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati haijaridhishwa na hali hiyo ambayo haileti taswira nzuri katika ustawi wa uchumi wa Zanzibar. Hivyo, kamati inaishauri serikali kutatua changamoto zinazopelekea kushuka kwa uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Aidha, serikali ishajihishe wafanyabiashara kutafuta fursa za masoko mapya katika nchi za jirani, kwani kutegemea soko moja kiuchumi sio jambo sahihi.

Uwekezaji Binafsi Kupitia *ZIPA*

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Uwekezaji na Ukuzaji Vitega Uchumi *ZIPA* kwa jitihada mbali mbali inazozichukuwa ili kuhakikisha uwekezaji nchini unaimarika kwa lengo la kukuza pato la taifa pamoja na soko la ajira. Kamati inaishauri serikali kuitekeleza vyema Sera ya Uwekezaji ya Zanzibar kwa kuweka vivutio zaidi vitakavyo wavutia wawekezaji wengi ambao watawekeza kuekeza katika nchi yetu na kuhimili ushindani na mataifa mengine hususan katika sekta ya viwanda. Aidha, kamati inaishauri serikali iongeze jitihada ya kujitangaza katika matamasha na maonesho ya kimataifa, ili kuvutia wawekezaji na kupata masoko mapya kutoka nchi za Asia na nchi za Mashariki ya mbali hususani katika Sekta ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, Uwekezaji binafsi kupitia *ZIPA* umepanda hadi kufikia thamani ya Dola za Kimarekani 437.7 milioni mwaka 2017 kutoka thamani ya 150.5 milioni mwaka 2016. Kuongezeka kwa uwekezaji binafsi nchini kumechangiwa na ukuaji katika sekta za Hoteli za kitalii na mikahawa, kilimo, uwindaji, uvuvi na ukodishaji majengo na biashara. Aidha, kuongezeka kwa Miradi binafsi ya uwekezaji kumepelekea ongezeko la ajira kufikia 1,557 mwaka 2017 kutoka ajira 1,071 mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, Kimsingi ongezeko hilo ni faraja katika uchumi wetu, hata hivyo kamati inasisitiza kubainishwa vyema idadi hizo za ajira kwa kuainishwa wazi idadi ya waajiriwa na jinsia zao na pia mgawanyo wa ajira hizo kwa sekta. Kufanya hivyo kutaweza kutoa taswira kwa

kiasi gani wawekezaji wameweza kusaidia ukuaji wa ajira kwa kila sekta ili kufahamu ni sekta zipi katika uchumi zinahitaji kufanyiwa jitihada na msukumo zaidi kwa kuondosha mapungufu yaliyopo. Aidha, kwa kuzingatia matumizi sahihi ya rasilimali ya ardhi, kamati inaishauri *ZIPA* izingatie aina za wawekezaji wanaokuja kuwekeza kwa kuangalia ubora wa miradi inayoombwa kuwekezwa na faida zinazoweza kupatikana kiuchumi, badala ya kuruhusu miradi mingi ambayo ina tija ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kutanua wigo wa uwekezaji, Kamati inaishauri *ZIPA* kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika sekta ya afya na elimu. Katika kulifanikisha hilo, Kamati inapendekeza serikali kupitia *ZIPA* kufanya mazungumzo na vyuo vikubwa na mashuhuri duniani juu ya kufungua matawi yake Zanzibar. Mkakati kama huo pia unaweza kutumika kwa sekta ya afya ambayo nayo kimsingi ikifanyiwa kazi ipasavyo inaweza kutoa fursa za biashara na ajira nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuzingatia ushauri huu, *ZIPA* itaweza kutanua wigo wa uwekezaji katika sekta ya utalii Zanzibar kwa kuanzisha aina nyengine za utalii ambazo ni utalii wa kimatibabu na utalii wa elimu.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango huo sio tu utakuza sekta ya utalii lakini pia utaimarisha upatikanaji wa huduma za afya na elimu zenye kiwango bora ambazo wananchi hutumia fedha nyingi kuzifuata nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa vivutio vya wawekezaji ni pamoja na mazingira tulivu ya kiuchumi, Sera nzuri za Fedha na Uchumi na utulivu wa bei pamoja na kuwa na sarafu ambayo haishuki thamani mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inatowa wito kwa serikali kupitia wataalamu wake wa uchumi kuhakikisha inayafanyia kazi maeneo hayo ya viashiria vya kiuchumi, ili kuwavutia wawekezaji na kuhimili ushindani mkubwa wa kibiashara na uchumi uliopo katika nchi zilizoendelea.

Mchango wa Sekta Binafsi katika Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika maendeleo na utoaji wa huduma mbali mbali nchini kama vile usafirishaji, uingizaji wa bidhaa, elimu na hata matibabu. Kwa kulitambua hilo, serikali inapaswa kuipatia mashirikiano makubwa sekta binafsi kwa kuiweka mazingira mazuri, ili kuzidi kuimarika na hatimae wananchi waweze kufaidika na huduma hizo. Aidha, serikali ifanye kazi kwa karibu na sekta hii na kupata maoni yao wakati wa kupanga na kufanya maamuzi juu ya masuala yanayohusu sekta binafsi.

Maendeleo ya Uchumi na Kijamii

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa Maendeleo ya kiuchumi na Kijamii kwa mwaka 2017, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 376,242 mwaka 2016 hadi kufikia watalii 433,474 mwaka 2017. Ongezeko hili la idadi ya watalii ni ishara kuwa, Zanzibar ina mazingira mazuri ambayo ni kivutio kwa watalii. (*Makofi*)

Kwa msingi huo, kamati inaisisitiza serikali iendelee kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini, ili iweze kusaidia katika kukuza sekta ya Utalii ikiwa ni moja ya maeneo ya vipaumbele kwa bajeti ya mwaka 2018/2019. Aidha, Kamati inasisitiza kuimarishwa kwa miundombinu ya barabara ambayo imeharibika kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyoambatana na mvua, kwani Ubovu wa barabara hizo hautoi taswira nzuri kwa wageni, lakini pia unaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaotumia usafiri wa vyombo vya moto, na wanaotembea kwa miguu.

Utekelezaji wa Vipaumbele kwa Mwaka 2017/18

Mhe. Mwenyekiti, Utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2017/2018 ulijumuisha uimarishaji wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama. Kwa upande wa elimu, ujenzi wa skuli 9 za ghorofa kwa Unguja na Pemba umefanyika na unaendelea kwa hatua mbali mbali. Skuli hizo ni Muembeshauri, Bububu, Kinuni, Fuoni na Chumbuni kwa upande wa Unguja, na Chakechake, Micheweni, Kizimbani na Muwambe kwa Pemba. Katika ujenzi wa skuli za ghorofa ambazo zilijengwa katika kipindi cha nyuma kumebainika mapungufu mbali mbali ikiwemo kuvuja kwa skuli hizo kama vile Skuli ya Madungu na Skuli ya Wawi kwa upande wa Pemba. Kasoro hizo zimepelekea serikali kuingia gharama kubwa ya matengenezo ambayo hayakuwa ya lazima iwapo kungekuwa na umakini katika hatua za awali za ujenzi wa skuli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuwa Baraza limeridhia kuundwa kwa Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza kasoro zilizojitokeza katika ujenzi wa skuli hizo, tunaamini kwamba kamati itakayoundwa itafanya kazi kwa ufanisi mkubwa kwa kuibua sababu zilizopelekea kutokea kwa kasoro hizo, pamoja na kuja na mapendekezo yatakayosaidia changamoto kama hizo zisijitokeze tena, sio tu kwa miradi ya ujenzi wa skuli lakini hata pia katika miradi ya ujenzi wa majengo mengine ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika kuimarisha huduma za afya kupitia Mradi wa Kupadisha Hadhi Hospitali za Vijiji kuwa za Wilaya na za Wilaya kuwa za Mkoa, miongoni mwa maeneo yaliyofanyiwa kazi ni ujenzi wa jengo la ghorofa mbili katika Hospitali ya Kivunge ambalo litakuwa na wodi ya wazazi, huduma za watoto na chumba cha upasuaji. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa paa la Hospitali ya Chake Chake yamekamilika na ujenzi wa nyumba za madaktari katika Hospitali ya Makunduchi unaendelea katika hatua za mwisho.

Mhe. Mwenyekiti**,** licha ya hatua hizo, kamati inasisitiza kwamba, upandishaji hadhi wa hospitali uende sambamba na upatikanaji wa madaktari pamoja na huduma bora zitakazoendana na hadhi ya hospitali hizo. Kamati inasisitiza hilo kutokana na changamoto zilizojitokeza katika hospitali ya Mkoani ambapo licha ya serikali kutumia fedha nyingi katika kuipandisha hadhi hospitali hiyo, imebainika kwamba baadhi ya vifaa havitumiki kutokana na kukosekana kwa wataalamu.

Mhe. Mwenyekiti**,** kiujumla katika utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2017/2018, baadhi ya maeneo hayakuweza kuainishwa vizuri utekelezaji wake kama vile eneo la kuimarisha viwanda vidogo vidogo ambalo lilikuwa na lengo la kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio. Katika eneo hilo, Kamati iliarifiwa kuwa utekelezaji uliofanyika ni ujenzi

wa jengo moja la Taasisi ya Viwango Zanzibar ambao unaendelea na umefikia hatua ya ghorafa ya pili.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kuwa bajeti inayotumika ni ya mfumo wa programu (*Program Based Budget*) ambayo utekelezaji wake umejikita katika kupata matokeo (*result*), Kamati inashauri katika maeneo ya vipaumbele ni vyema utekelezaji ukajikita katika kuonesha matokeo yaliyopatikana kulingana na malengo yaliyopangwa.

Utekelezaji wa Vipaumbele kwa Mwaka 2018/19

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati inapongeza juu ya maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 kwani maeneo hayo ni muhimu kwa kuwa yamegusa sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya utalii, miundombinu na kilimo ambazo kwa namna moja au nyengine zina mchango mkubwa katika uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti**,** miongoni mwa maeneo ya vipaumbele ni pamoja na eneo la kuendeleza utafiti ambapo halijaekwa wazi aina ya utafiti utakaofanyika, gharama zitakazotumika na walengwa wa utafiti huo. Aidha, kipaumbele chengine ni kukuza uwezo wa watu ambapo pia hakijazingatia maeneo yaliyokusudiwa katika kukuza uwezo wa watu hao. Ni dhahiri kuwa vipaumbele vya aina hiyo ni vigumu kuvipima ufanisi wake, na hivyo Kamati inashauri vipaumbele vinavyoekwa viwe ni vyenye kupimika ufanisi wake.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa namna ambavyo maeneo ya vipaumbele yalivyoanishwa, kamati inaishauri serikali inapopanga maeneo ya vipaumbele kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo, ni vyema kukaainishwa uchanganuzi wake kwa kuweka wazi maeneo yanayotarajiwa kutekelezwa kwa kipindi husika kuliko kuorodhesha vipaumbele hivyo kiujumla jumla bila ya kuonesha hatua zitakazochukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kuwa utekelezaji wa vipaumbele kwa mwaka uliotangulia (2017/18) haujatekelezwa kwa ukamilifu wake, Kamati inashauri juu ya kukamilisha utekelezaji wa maeneo hayo kwa muda uliokusudiwa na pia kuzingatia utekelezaji wa ufanisi kwa maeneo mapya ya vipaumbele ikiwemo kuendeleza utalii, ajira kwa vijana na kuendeleza utafiti kwa mwaka 2018/19 ili malengo yaweze kufikiwa.

Rasilimali kwa Ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2018/19

Mhe. Mwenyekiti**,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 unategemea rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji ambapo jumla ya TZS bilioni 613 zitatumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ikilinganishwa na bajeti ya TZS bilioni 496.6 kwa mwaka 2017/2018 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 23.6. Kiujumla kuna ongezeko la fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka huu wa fedha ukilinganisha na mwaka uliotangulia. Hivyo, kamati inaishauri Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinatolewa kwa ukamilifu na kwa wakati, ili kukuza ajira na rasilimali fedha kwa wananchi ambayo ni muhimu kwa kuondoa wimbi la umasikini nchini.

Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi na Programu kwa Mwaka 2017/18

Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii

Mhe. Mwenyekiti**,** Utalii ni miongoni mwa maeneo ya vipaumbele katika Bajeti kwa takribani miaka mitatu mfululizo kama inavyoonekana kwa Bajeti za mwaka wa fedha wa 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019. Kupitia Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii ambayo imekuwa ikiongezewa fedha kama ambavyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa wakishauri, bado Bajeti ya Serikali haijazingatia sekta hii kama ni moja ya kipaumbele katika utekelezaji wake kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti**,** mradi wa kuendeleza utalii kupitia Programu Mjumuisho kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 ilitengewa jumla ya Tsh. 600, 000, 000 lakini kwa kipindi cha miezi tisa ni Tsh 200,885,000 zilizopatikana ambazo ni sawa na asilimia 33.5 tu ya lengo. Kwa mwaka 2017/2018 programu hii iliongezewa fedha na kutengewa jumla ya Tsh. 1,000,000,000 lakini kwa kipindi cha miezi tisa ni Tsh. 300,000,000 tu zimeingizwa kwa ajili ya programu hii ambazo ni sawa na asilimia 30 ya malengo ya Bajeti iliyotengwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na kuimarika kwa mapato ya ndani yaliyokusanywa na serikali kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 na mwaka wa fedha wa 2017/2018 lakini upatikanaji wa fedha kwa programu mjumuisho kwa ajili ya maendeleo ya utalii ambao ni moja ya vipaumbele umekuwa wa kusuasua. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya utalii kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa msingi wa kuwa utalii ni miongoni mwa kipaumbele katika Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za uendelezaji utalii zinapatikana kwa ukamilifu, ili kuhakikisha Bajeti iliyopangwa kwa kuendeleza utalii inafikia malengo yaliyokusudiwa.

Mradi wa Ujenzi wa Mahkama Kuu

Mhe. Mwenyekiti**,** katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Mahkama kuu ilipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mahkama Kuu Tunguu ambapo fedha zilizokadiriwa ni TZS 900,000,000 na fedha zilizopatikana na kutumika ni TZS 500,000,000 hadi kufikia Machi 2017. Kamati ya Bajeti ilipatiwa ufafanuzi na Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu ufanisi wa mradi huu kwa kuzingatia fedha iliyotumika na kazi iliyofanyika ambapo iliarifiwa kuwa licha ya fedha nyingi kutumika hakuna maendeleo yoyote yaliyofanyika katika eneo hilo la mradi. Hali hii inatia hofu juu ya nidhamu ya matumizi ya fedha za serikali hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo wajumbe wamekuwa wakiilalamikia mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati inaendelea kuisisitiza serikali isimamie vyema matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ili thamani halisi ya fedha (*value for money*) iweze kupimika na kuleta tija iliyokusudiwa.

Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Miezi Tisa (2017/2018)

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Baraza lako tukufu liliidhinisha Jumla ya Tsh. bilioni 1087 sawa na Bajeti nzima ya serikali. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) ya

utekelezaji wa bajeti, matumizi ya serikali yamafikia jumla ya Tsh. bilioni 676.9 ambazo ni sawa na utekelezaji wa asilimia 62 ya bajeti nzima ya mwaka. Utekelezaji huu ni sawa na nakisi ya asilimia 38% ambayo bado haijatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** nakisi ya asilimia 38 ya utelekezaji wa bajeti kwa mwaka 2017/18 ni ndogo ukilinganisha na nakisi ya mwaka 2016/17 kwa kipindi kama hicho ambayo ilikuwa asilimia 47. Hii ni ishara njema kwa taasisi za ukusanyaji wa mapato na serikali kwa ujumla na inaashiria kuwa serikali inafanya vizuri katika kuhakikisha inafikia malengo ya bajeti zinazopitishwa kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka 2017/2018 kama ilivyokuwa kwa Bajeti ya mwaka 2016/2017 mapato kutoka nje yanaonekana kuzorota kwa kiasi kikubwa kulinganisha na mapato ya ndani ya serikali. Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS Bilioni 151 za mapato kutoka nje kati ya makadirio Tsh. bilioni 380.5 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 39.7 tu. Hii ina maana kuwa sehemu kubwa ya nakisi ya utekelezaji wa bajeti inatokana na kutokupatikana kwa fedha kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati inatambua na inathamini juhudi za serikali katika kuhakikisha utegemezi wa Bajeti ya Serikali unapungua mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, kamati inaishauri serikali kuendelea na juhudi hizo kwa kuwa upatikanaji wa fedha kutoka nje umekuwa wa kusuasua na kimsingi unaathiri utekelezaji wa Bajeti. Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kuwa mapato kutoka nje hulengwa kutumika katika shughuli za maendeleo, kutokupatikana kwake kunaashiria kuwa utekelezaji wa miradi utakuwa si wa uhakika, na kwa maana hiyo wananchi walio wengi hawatonufaika na utekelezaji wa shughuli za miradi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi 2017/2018) mapato halisi ya ndani yalifikia jumla ya Tsh. Bilioni 506.6 sawa na asilimia 98 ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa ambayo ni Tsh. Bilioni 515.1. Makusanyo hayo yalichangiwa zaidi na mapato yasiyokuwa ya kodi ambayo yaliyofikia jumla ya Tsh. Bilioni 41.4 sawa na asilimia 113 ya makadirio ya miezi tisa ambayo ni bilioni 36.6. Mhe. Mwenyekiti**,** kufanya vizuri kwa mapato yasiyokuwa ya kodi kunaashiria ni kwa kiasi gani serikali haikuelekeza nguvu za ukusanyaji wa mapato kupitia kodi pekee ambazo kimsingi zinamgusa kila mwananchi, lakini pia ilielekeza nguvu zake katika kuhakikisha inasimamia vyema vyanzo mbadala vya mapato kwa lengo la kuhakikisha Bajeti ya Serikali inatekelezeka kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati ina imani kuwa, mapato yasiyokuwa ya kodi yanaweza kuongezeka zaidi iwapo usimamizi wa maeneo ya makusanyo hayo yatapangiwa utaratibu ulio wazi na rafiki zaidi na kuondoa mianya ya kutoa au kupokea rushwa kwa wasimamizi katika maeneo hayo. Kamati inashauri kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, pamoja na mikakati mengine ambayo serikali imejiwekea katika ukusanyaji wa mapato, ni vyema ikaimarisha pia mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya serikali yasiyokuwa ya kodi kwa lengo la kuhakikisha mapato ya serikali yanaimarika bila ya kumuathiri mwananchi kupitia kodi ambazo hupunguza kipato na kumuongezea gharama ya maisha.

Deni la Taifa

Mhe. Mwenyekiti**,** hadi kufikia Machi 2018 deni la taifa limefikia TZS Bilioni 519.7 kutoka TZS Bilioni 377.1 ambalo ni sawa na ukuaji wa asilimia 37.8 wa deni hilo na pia ni sawa na asilimia 16.8 ya pato la taifa kwa mwaka 2017. Mhe. Mwenyekiti**,** ingawaje deni hili ni himilivu kulingana na uchumi wetu, hata hivyo Kamati inasisitiza iwekwe mikakati ya itakayohakikisha kuwa deni hilo haliogezeki kwa kasi. Aidha, sababu za kukopa na kupelekea kuogezeka kwa deni la taifa ni kitu cha kupewa uzito wa kipekee kwa kuwa kuongezeka kwa deni la taifa kunaweza kuwa na athari kubwa kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti**,** miongoni mwa sababu zilizotajwa na serikali zilizochangia kuongezeka kwa deni la Taifa ni pamoja na kuanza tena kutolewa fedha za mkopo kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria *Terminal II*. Ni imani ya kamati kuwa, serikali itajifunza juu ya namna gani inapaswa kuwa makini na miradi mikubwa kama hii ili iweze kukamilika kwa wakati. Aidha**,** Kamati inashauri utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo inatumia gharama kubwa ya uwekezaji na kuchangia katika kuongezeka kwa deni la taifa, iwekewe usimamizi mzuri na kuhakikisha inafanya kazi kwa ufanisi na kuipatia serikali mapato yanayolingana na gharama iliyotumika katika uwekezaji ili serikali iweze kurejesha gharama za uwekezaji na kupunguza mzigo mkubwa wa madeni ya ndani na ya nje.

Mwelekeo wa Bajeti 2018/2019

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka 2018/2019 Bajeti ya Serikali inakadiriwa kufikia Jumla ya Tsh. Trilioni moja Bilioni mia tatu na kumi na tano nukta moja (1315.1). Kiwango hichi cha bajeti ni sawa na ongezeko la asilimia 21 ya Bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa ujumla bajeti ya serikali imeendelea kukua kutoka bilioni 841.5 mwaka 2016/2017, trilioni moja bilioni themanini na saba nukta nne (1,087.4) mwaka 2017/2018, hadi kufikia Trilioni mojo bilioni mia tatu kumi na tano nukta moja (1,315.1) mwaka 2018/2019. Hii inaashiria ni kwa kiasi gani mipango ya serikali inaimarika siku hadi siku kwa lengo la kuhakikisha inagusa kila sekta ya uchumi wa nchi na kufikia malengo ambayo tumejiwekea kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya 2020 pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza umasikini (*MKUZA III*).

Mhe. Mwenyekiti**,** kutokana na kuongezeka kwa bajeti ya Serikali, hatua mbali mbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato zinatarajiwa kuchukuliwa kwa lengo la kuhakikisha bajeti ya Serikali inafikia malengo. Moja wapo ya hatua hizo ni pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya mwaka 2017, yenye lengo la kufuta ushuru wa stempu kwa usambazaji na uuzaji wa bidhaa za mchele na unga wa ngano nchini, ili kuleta unafuu zaidi wa bidhaa za chakula.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na kufuta ushuru huo kwa bidhaa za chakula (mchele na unga wa ngano), Kamati inaishauri serikali iandae mikakati madhubuti ya usimamizi ili kuhakikisha dhamira hiyo sio tu inawanufaisha wafanyabiashara lakini wananchi ambao ndio walengwa wakuu. Hii ni kutokana na uzoefu kwamba, mara nyingi baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu hutumia fursa kama hiyo kujinufaisha na kumkandamiza mwananchi ambaye ni mnunuzi wa mwisho wa bidhaa hizo. Aidha, kwa lengo la kuimarisha na kuleta ufanisi zaidi wa ukusanyaji wa mapato, kamati inaisisitiza serikali juu ya kuharakisha na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato (*EFD*) kwa lengo la kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati inaipongeza Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) kwa kushirikiana na Kampuni ya Mawasiliano Zantel kuanzisha mfumo wa ulipaji kodi kwa njia ya simu kupitia huduma ya *Ezy-Pesa,* ili kuongeza ufanisi, kuwarahisishia na kuwapunguzia usumbufu walipa kodi pamoja na kupunguza tatizo la msongamano wa wateja wanaohitaji huduma za kibenki. Hata hivyo, kamati imearifiwa kuwa, kuna changamoto kwa baadhi ya taasisi za serikali kutojiunga na mfumo huo. Aidha, wananchi wengi bado hawajahamasika kutumia mfumo huo sambamba na kutokuwa na uelewa wa kutosha. Kamati inaisisitiza serikali kuzitaka taasisi ambazo bado hazijajiunga na mfumo huo kujiunga haraka, ili kuwarahisishia wananchi kulipa kodi bila ya usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati pia inaishauri Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) iendelee kutoa elimu kwa wananchi pamoja na Taasisi za Serikali, kuhusu namna ya kutumia mfumo huo katika kufanya malipo na kuongeza idadi ya mawakala sehemu mbali mbali ili wananchi walio nje ya mji waweze kufanya malipo katika maeneo yao.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti**,**kwa utekelezaji bora wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati inaisisitiza serikali kupitia watendaji na taasisi zake, kuhakikisha fedha zinazopatikana zinatumika kwa mujibu wa shughuli na programu zilizopangwa na kuidhinishwa na Baraza. Aidha, serikali ijifanyie tathmini juu ya utekelezaji wa bajeti kila baada ya muda kwa kuzingatia matokeo badala ya kuangalia shughuli zilizotekelezwa pekee, ili kuhakikisha malengo yaliyopangwa yanafikiwa kama yalivyo malengo ya bajeti inayotumia programu (*PBB*).

Mhe. Mwenyekiti**,** ningependa kumaliza hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kwa kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati ambao kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha 2017/2018 wamekuwa wakifuatilia kwa umakini mkubwa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na kuichambua kwa kina, ili kuishauri vyema serikali kupitia taasisi zake juu ya utekelezaji bora wa bajeti yake kwa maslahi ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa heshima na ridha yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa majina kama ifuatavyo:-

Mhe. Mohamed Said Mohamed	Mwenyekiti
Mhe. Bahati Khamis Kombo	Makamo Mwenyekiti
Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe
Mhe. Abdallah Ali kombo	Mjumbe
Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Mjumbe
Mhe. Asha Abdallah Mussa	Mjumbe
Mhe. Shehe Hamad Mattar	Mjumbe

Pia napenda kuwatambua makatibu wa Kamati hii ambao ni:

Ndg. Abdallah Ali Shauri	Katibu
Ndg. Kassim Tafana Kassim	Katibu
Ndg. Asha Said Mohamed	Katibu

Mhe. Mwenyekiti**,** mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kwa michango yao makini waliyoitoa wakati wakichangia wizara mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha tunapata bajeti iliyokuwa bora zaidi na inayoleta athari kwa wananchi ambao tunawawakilisha. Ni imani ya kamati kuwa Wizara ya Fedha na Mipango na serikali kwa jumla imeyasikia haya maoni ya kamati na michango mbali mbali ya Wajumbe na itayazingatia kwa ajili ya utekelezaji uliyo bora.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nakushukuru Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa kwa umahiri wako na usomaji mzuri wa kuwasilisha hotuba hiyo. Lakini pia kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Naomba niwakumbushe Kanuni 58(6) ambayo ndiyo inayotuongoza kuhusiana na majadiliano hayo, "Kila Mjumbe anayejadili ataruhusiwa kusema kwa muda wa dakika 15 wakati wa mikutano ya kawaida na dakika 20 wakati wa mikutano ya bajeti. Lakini pia Spika akiona inafaa anaweza kumuongeza msemaji dakika si zaidi ya 10".

Waheshimiwa Wajumbe nilitaka niseme hili kabla ya kuwaita wachangiaji kwa siku ya leo, wachangiaji wetu, Kiti kimeona inafaa kwa kutumia Kanuni hii kila Mjumbe atachangia kwa dakika zile 20 kwa siku ya leo. Kwa hivyo kama nilivyosema pia Kiti kina mamlaka, isizoeleke kuwa tunakwenda hivyo kwa dakika 20 lakini pia Kiti kikiona inafaa basi kinaweza kupunguza au inaweza ikamzidishia Mjumbe jinsi ya kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea mchangiaji wetu wa mwanzo sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata na Mhe. Simai Mohamed ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kuwa mchangiaji wa mwanzo katika wizara hii muhimu lakini nijue tu pamoja na mawaziri leo kuwa na shughuli kwa Mhe. Rais, lakini kuna Mawaziri muhimu walikuwa angalau wabaki humu, hasa kama Waziri wa Afya. Najua kuna shughuli muhimu ya Mhe. Rais lakini kuna umuhimu wake Waziri wa Afya ilikuwa muhimu kubaki humu na hata Naibu Waziri wake humu simuoni hii ni wizara muhimu ambayo inawagusa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 9 mwenendo wa uchumi wa Zanzibar. Uchumi wa Zanzibar unaendelea kuimarika kwa pato la hali halisi ya taifa kwa asilimia 7.5. Nipongeze suala hilo na Mhe. Waziri alitaja kama mambo sita katika kitabu hichi kimesaidia kukua kwa mapato. Juhudi kubwa za kujenga umoja na ya mwanzo alitaja kuongezeka kwa idadi ya watalii, ya pili kuongezeka kwa usafurishaji wa bidhaa nje, ya tatu kuongezeka kwa kiwango cha uwekezaji, nne kuongeza kwa uzalishaji wa mazao, tano kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la biashara, sita kuendelea kuwepo kwa hali ya amani.

Hoja yangu iko hapa kwenye hoja kuwepo kwa hali ya amani ndio hoja yangu hapa. Mhe. Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu juzi Waziri tarehe 20 mwezi 6 naomba ni-*quote* kidogo. Baraza la Wawakilishi lilifanya jambo zuri na kupigiwa mfano kwa kuwaalika mabalozi ndani ya chombo hichi, wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, viongozi wa vyama vya siasa, lakini cha kusikitisha wawakilishi wa vyama vya upinzani viti vilibaki vitupu, naomba nivitaje ambavyo vilikuwa juu.

Chama cha Jahazi Asilia hakuonekana mwakilishi wao, *AFP* mwakilishi wao hakuonekana, *NCCR* Mageuzi mwakilishi wao hakuonekana *TADEA*, *CHADEMA* na *TLP* sijui nini. Ofisi yako Mhe. Mwenyekiti, ilimefanya jambo zuri sana na hii ndio moja ya amani, imealika hawa watu lakini hawakuonekana. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi akiwemo Mwenyekiti wangu Ramadhani Abdalla Kichupa alikuwepo juu huku na viongozi wengine Mwenyekiti wa Mkoa wa Mjini/Magharibi, Sheikh Talib alikuwepo naye juu niwapongeze. Sasa sijui muelekeo huu ulikuwa wa nini na niwaeleze tu viongozi tunapozungumza amani na umoja wa kitaifa tusizungumzie ndani ya Baraza pekee lakini vile vile tuzungumze ndani ya vyama vyetu kuna umuhimu wa aina yake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia ukurasa wa 35. Mhe. Waziri hapa naomba tusikilizane uzuri kweli kweli ukurasa 35, “kupunguza unafuu wa kodi ili kulinda viwanda vya ndani”.

naomba ninukuu Kifungu cha 83;

kifungu cha 83

> "Mhe. Spika Serikali imekuwa ikitoa unafuu wa ushuru wa forodha na kodi nyengine kwa uingizaji wa bidhaa muhimu za chakula kama vile mchele, unga wa ngano na sukari. Hata hivyo, kufuatia kuimarika kwa uzalishaji nchini kupitia Kiwanda cha Ngano cha *Zanzibar Milling Cooperation* na kufufuliwa kwa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda, najitokeza haja ya kupunguza unafuu unaotolewa kwa uingizaji wa bidhaa hizi muhimu ili viwanda vyetu viweze kuhimili ushindani wa serikali".

Hapa Kiswahili, serikali inakusudia kupunguza unafuu unaotolewa sawa sawa na ushuru na uingizaji katika dhamira ya kupunguza au kuondoa kabisa. Kwa hivyo niombe Mhe. Waziri hili neno "serikali inakusudia" lifutwe isikusudie. Historia zipo na hazitaki tochi na zitajukumu Waziri wa Biashara na Viwanda hayumo humu, lakini Mhe. Mohamedraza Hassanali yumo humu ndani. Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze ku-*declare* siwezi kudharau dafu kwa embe ya msimu. Dafu kama mnazi utapata tu, muembe mwaka hata mwaka ndio uzae. Naanza ku-*declare* mimi ni mfanyabiashara baada ya hii siasa naweza kurudi tena uraiani kufanyakazi, huwezi kudharau dafu kwa embe ya msimu. Muembe mwaka hata mwaka ndio uzae, dafu ukiwa kwenye mnazi unavuna tu dafu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, kuna mambo kabla ya kuyaamua ni muhimu sana kuyafanyia utafiti wa hali ya juu kabisa, maslahi ya wananchi wake wa Zanzibar. Serikali hii isingekuwepo madarakani bila ya kuwepo wananchi wake, wananchi ndio waliyoiweka serikali hii madarakani. Niipongeze sana serikali chini ya Rais Dkt. Ali Mohammed Shein na Waziri wa Fedha na

Mipango nikupongeze sana kwa hili. Ukweli tutasema ukweli, moja utasema moja na mbili utasema mbili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, umeondosha mwezi huu wa mtukufu wa ramadhani na rekodi zipo huku nyuma mchele, unga wa ngano na sukari ili kuwapa nafuu wananchi ambapo jambo hili Tanzania Bara halipo, na niliwaambia Tanzania Bara msione aibu kuiga Zanzibar ndani ya Bunge niliwaambia. Mmeiga mambo mengi kutoka Zanzibar, yakiwemo matumizi ya dola. Zanzibar mmeanza kutumia dola mwanzo, *PBZ* kulikuwa na akaunti baadae wakaiga walipoona kuna maslahi, biashara ilianza Zanzibar wameiga, lakini hata vyama vingi vilianza Zanzibar, ndio wakafuata Tanzania Bara. Hili ni jambo la kusikitisha sana, pamoja na kuondosha kodi hizo Mhe. Waziri basi wananchi wa Zanzibar wanakula mlo mmoja tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema sana Rais nimpongeze kwa dhati kabisa. Leo hii mnafikiria mmetumia maneno ya kupunguza au kuondosha kabisa lengo la madhumuni ya kununulia viwanda. Mhe. Mwenyekiti, kama mnalinda viwanda kweli, nikuambie itabidi na mimi nifunguwe kiwanda sasa, Kiwanda cha Sukari nitaleta nzima nitasaga na cha mpunga nitaleta nzima hapa nisage, kama kweli. Leo hii mnafikiria *Zanzibar Milling Cooperation* kabla haijafika lengo gani. Mhe. Mohamedraza Hassanali alikuwa kaleta unga kutoka Ufaransa *quality* namba moja, Batashi Marehemu Mwenyezi Mungu amrehemu alikuwa kaleta unga *Oman Flower*. Wakafika pahali akataka kulindwa kiwanda hiki hiki, poli ilipanda shilingi 15,000, Waziri wakati ule ni Mhe. Amina Salum Ali hayupo hapa angesema. Leo tunalinda kiwanda hiki hiki kinaleta *material* yote nzima kodi hailipwi, inaleta *material* zero. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan alizungumza hapa kuhusu Kiwanda cha Maziwa, msamaha uliotoka mpaka leo maziwa yanaingia anajua Mwenyezi Mungu. Tusiseme kwa mdomo tu tuwaone huruma wananchi. Leo huu mkate wa boflo huu ndio uliotulisha sisi tukafika hapa huu hapa, hata Mhe. Balozi nimekwenda kwake anakula mkate wa boflo huu, leo mwananchi tutawagomboa vipi wapiga kura wetu hawa. Mkate huu shilingi 250 na huu shilingi 350. Serikali hii imekaa kwa ridhaa ya wananchi leo mkate huu ndio uliotulea, tunafanya kitu gani sisi, vichekesho huu hapa mkate wa boflo, hakuna asiyekula mkate huu, duniani kote haupatikani mkate kama huu isipokuwa Zanzibar, una hadhi yake. Tusifike pahala tukapandisha bei unga ngano kutaka kuwaumiza wananchi, tuwe wakweli tusiwe na huruma ya mdomo tu tuwe kwa vitendo. Huu unga ukipanda bei nani ataugomboa, huu unakula hata kwa sukari tu, ukachovya ukala kwa sukari au kwa supu, leo mnataka kupandisha kumlinda mtu mmoja, watu milioni moja wakaumie humu ndani haiwezekani kwa kumlinda mtu mmoja au watatu haiwezekani, tusiwe na huruma ya mdomo tu iwe ya vitendo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kesho kutwa kuna uchaguzi wa mwaka 2020, tunataka tushinde kwa kishindo kuliko tulivyoshinda mwaka 2015. Tunataka tushinde kwa kishindo kuliko kile cha mwaka 2015, lazima tuwalinde wapiga kura wetu, mkate una hadhi yake huu na ndio uliotulea sisi, shilingi 250 tu pale unakwenda kununua unalala, hata muuza mkate anaweza kukufikiria akakukopesha. Lakini unga wa ngano huu analindwa mtu huyo, hicho kiwanda kina wafanyakazi wangapi. Mawaziri mmeshafanya utafiti kwanza. Ndio sisi wengine hatukusoma hatujapata Uwaziri wala Unaibu Waziri kutokana na elimu yetu ndogo, lakini nyinyi msitutie changa la macho, huu ni mchanga wa macho. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitafungua kiwanda nina-*declare interest* kabisa kama kiwanda kile kitalindwa, nitafungua kiwanda Mwenyezi Mungu akinijaalia hapa,

ijapokuwa mkopo wa *PBZ* Kiwanda cha Sukari na cha mpunga nitaleta mpunga mzima nisipate kulipa kodi. Huku mnataka kuongeza pato, halafu cha kusikitisha unga ule wa *Zanzibar Milling Cooperation* unauzwa shilingi 48,000, hao wanaoagiza wengine *import* wanauza shilingi 54,000. Sasa vichekesho hivyo, anauza shilingi 48,000 na hao wengine wanauza shilingi 54,000 kuwa bado maslahi anayo ndio akauza chini. Sasa humu haielekei, yakhe "*shuu hadha". (Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, serikali hii ipo madarakani kwa ajili ya wananchi na kesho kutwa ni uchaguzi tunataka tushinde kwa kishindo tena kuliko mwaka 2015. Leo mchongo huu unakuwa vipi, kiwanda kinaleta mali nzima hapa, inashushwa pale hata mchukuzi hanufaiki, inashushwa kwenye meli inakwenda kwenye gari moja kwa moja inakwenda kumwaga, lakini hawa wanaoleta ana watu zaidi ya 600, mchukuzi anafaidika na kuna mtu ana mkewe nyumbani na mtoto, gunia anabeba na kwengine anabeba.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri suala hili nikuombe sana hapa tupo kwa niaba ya wananchi hili kalizingatie, hii haielekei mkate huu utapanda na ulipanda baada ya kuuliza Mhe. Raza huyu hapa mkate uliweza kupanda. Dkt. Karume aliweka formula maalum baada ya mgogoro huu akasema ngano nzima ilipiwe asilimia 10. *Sorry Hansard* niweke sawa, ngano nzima iwe *zero*, wafanyabiashara wa ngano walipe aslimia 10 na ndio kipimo tulichonacho mpaka muda huu. Ngano nzima zero, wafanyabiashara wanaolipa ngano waweke asilimia 10 ndio mfumo tunaokwendanao, tusiwe na huruma ya mdomo tu na vitendo tuvifuate. Wananchi watakuja kuumia, mkate wa boflo nakuambieni tena mara ya tatu haupatikani popote huo na mnyonge ndio kimbilio lake hili. Nilikuwa nikiwatetea siku zote wauza mikate, Manispaa wasiwabughudhi hawachafui mazingira. Lakini leo ngano inataka kulindwa kiwanda hiki, aah! hapana. Mimi hili historia itanikumbuka na itajiandika au itatukumbuka sisi Wawakilishi humu ndani, hili halielekei.

Mhe. Mwenyekiti, tufuate *formula* ile aliyoanzisha Rais Mstaafu Dkt. Karume. Ngano nzima iwe zero ushuru wake na wanaoagiza unga iwe asilimia 10.Vyenginevyo hapa, yeye anauza polo *Zanzibar Mini Cooperation* shilingi 48,000 na uthibitisho ninao wa risiti na huu wengine wanauza shilingi 54,000. Leo huo unga wa maziwa unaoletwa hata wewe Mhe. Mwenyekiti, unaweza kufungua kiwanda nyumbani, unakuja ngano ni nzima ukamwaga ukatia jiti ukakoroga tu uka-*pack,* haina haja ya kufungua kiwanda nini faida, wafanyakazi wangapi. Kwa hivyo Mawaziri kabla ya kuamua mngetafakari kwanza na mjipime nini kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, hii hali ndio ipo hivyo Mhe. Waziri utakuja kutueleza na mimi kama nilivyosema nitafungua kiwanda, nitafungua kiwanda kweli kwa hali kama hiyo. Maana yake huku mnataka kodi na huku kodi tunaifukuza aa! hapana. Mhe. Mwenyekiti, niseme kama nitasikilizwa sawa na nisiposikilizwa sawa, lakini historia itakuja kutukumbuka sote humu ndani katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, jengo la jengine nije katika jengo la *ZSSF* pale lililojengwa *Train building* la Darajani. Kuna watu wana sehemu mule ramani zao kwenye Muzammil hatukuoneshwa kile kipenu na kipo historia kabla ya Mji Mkongwe kuanza. Sasa nini sababu tunaheshimu Mji Mkongwe, kipo kile kipenu kule njia ya Muzammil pale kabla Mji Mkongwe haujaanza hakikurejeshwa, kule mbele sokoni kimerejeshwa sijui sababu gani, tunalinda Mji Mkongwe au

tunakwenda wapi. Kuna watu wamekosa maduka yao sijui utaratibu utakuwa vipi, kwa hivyo na wao wafikiriwe.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, hili ukalifikirie sana la Kiwanda cha Sukari cha Mahonda. Mhe. Mwenyekiti, tuna nia nzuri jamaa haki yake tuseme, jamaa anastahiki pongezi sana kwa kufufua kiwanda kile, kafanya kazi kubwa. Kama kulindwa alindwe yule, hapa hatuzalishi ngano sisi, yule angalau kuna miwa. Lakini hata tukimlinda yule bado tutawaumiza wananchi kwa hiyo bei ya shilingi 90,000 ni bei gani itakuja kwa kilo sasa hivi fanya hesabu. Hali ya maisha ni ngumu, tusione sisi humu tunapigwa na *AC*, tukitoka huko hali ni tete, pamoja na nia ya Rais, kazi kubwa kafanya Mhe. Rais kwa wananchi hawa. Lakini mshaurini vizuri Mhe. Rais. Kiwanda kile kinastahiki kulindwa lakini na sisi Mawaziri tuwe wakweli wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, leo mali inatoka Tanzania Bara inakuja hapa, yetu sisi isiende kule kwa sababu gani, tumeungana vipi. Mali ya Zambia inaingia Bara haina tatizo, inayotoka Uganda ikaingia Tanzania Bara haina tatizo, inayotoka Kenya na hata juzi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alikaa nao akasikiliza tatizo. Kulikuwa kuna bidhaa za Kenya haziingii Tanzania Bara na za Tanzania Bara, wakafika wakatatua. Leo tulioungana hapa hatutatui tatizo, kwa nini tusitatuwe tatizo hili. Tunalinda viwanda vya Tanzania, Mahonda haiko Tanzania jamani. Mimi sijui Geografia nisaidieni. Kiwanda cha Mahonda hakiko Tanzania jamani au tunalinda viwanda vya Tanzania Bara tu. Wao bia watuletee, saruji watuletee, nondo watuletee, maji watuletee, mbatata na vitunguu watuletee.

Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Raza alizungumza na historia itasema bado cheti cha ndoa tukachukue Tanzania Bara, ndio huo mwelekeo tunaokwenda. Bado cheti cha ndoa tukachukue Tanzania Bara ndio kilichobaki, nakumbuka mimi Mhe. Raza alizungumza vizuri sana kabla hujaingia kwenye siasa. Sasa tufike pahali tuseme ukweli jamani. Tukilinda kiwanda hiki cha ngano basi mkate wa boflo *total* utapanda, itakuwa hakuna *monopoly*. Tumeona kwenye *speed boat*. Tunajua watu watakasirika, wataumia na watanung'unika lakini hali ndio ilivyo, tumekula viapo humu ndani, tusimlinde mtu mmoja tukawakera watu milioni moja, tusilinde watu kumi tukawakera watu milioni moja au laki saba. Tufanye njia ni namna gani sukari ya Mahonda itakwenda Tanzania Bara ili kiwanda kile kiweze ku-*survive*. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachangia huku Baraza tupu hakuna Mawaziri badala ya Waziri wa Fedha na Mipango tu, angalau na huku kuwe na Mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye sekta hii hii *ZRB*, wanafanyakazi nzuri niwapongeze lakini kidogo watumie lugha ambazo zinaweza kumtoa nyoka pangoni, sio kila kitu kutumia nguvu, elimu ya busara ya siasa inatakiwa na maneno mazuri ni sadaka. Mhe. Mwenyekiti, wamekuwa wakifunga magari wakati mwengine, gari inaweza ikatembea ikafanya ajali yakaja yakatokea mengine, kwa hili nalo lifikiriwe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais ana nia nzuri na wananchi wake na sisi sote ni mashahidi. Rais kafanyakazi kubwa kwa wananchi hata sisi Wawakilishi humu ndani tumeshuhudia juzi tu nini kafanya. Basi tusigombanishe serikali na wananchi, kapapatua akanunua meli ya kileo ile. Lakini masikitiko makubwa meli juzi sijui Euro ngapi imetumia sijui laki tisa, au sijui laki saba zilizotiwa hakuna kitu. Tena Waziri anatoka anakuambia suala la kuharibika mashine ni jambo la kawaida. Aka! mbona ile gari yako mpya haijaharibika, suala la kuharibika mashine ni jambo la

kawaida, ile meli ukaitaja mimi naogopa hata kuchangia, maana kama naugusa moyo wa Mhe. Rais, naogopa kuzungumza mengi hasa kuhusu habari za meli, naogopa kabisa kuzungumza kuhusu ya meli, meli maana yake utataka kulia. Leo unatoka unasema kuhusu mashine kuharibika jambo la kawaida, mbona gari yako mpya haijaharibika.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ninakukumbusha una dakika 5.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo meli ile inataka kuongezewa gharama, inatiwa mafuta ikifika jioni haijulikani inakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nije na suala kidogo la Manispaa. Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri kwa ziara walioifanya ile juzi, kutembelea masoko na wameona ukweli wenyewe ulivyo na hatua wameziona, sio tunazungumza hapa kuja kubahatisha. Ukweli wanaona ukweli ukoje, wametembelea karibu na mimi nimeona na hali wameiona ya uhalisia, nafikiri hata msimamizi mmoja wa soko kasimamishwa. Kweli ndio hali ilivyo, wananchi wanahitaji usafi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya maelezo hayo Mhe. Waziri nikushukuru sana, nikutakie kila la kheri, lakini hili hali ya kiwanda kulinda mmoja kwa watu milioni moja au laki saba, aah! hili litakuwa vichekesho.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kidogo na suala la mwani, hii sekta kidogo inakwenda kama Wizara nne na mimi nimeguswa kidogo au nimezungukwa na bahari. Mhe. Mwenyekiti, wanahitaji vitendea kazi vilivyokuwa bora, kwa kwenda kina kirefu cha maji kufuata mwani. Mwani huu uliokuwa hauna tija, nao wafikiriwe wananchi wangu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naamimi nisipoteze muda nikushukuru, na hii mikate yangu ya boflo nayo niondoke nayo itanisaidie kwa supu.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoun kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, Lakini pili, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mpinduzi, yeye pamoja na Mawaziri wote kwa kuangalia hali halisi ya wananchi wetu wa Zanazibar, juu ya maisha yao ya kila siku. Kwa hivyo nimpongeze Waziri wa Fedha na watendaji wake wote kwa kuangalia kubwa zaidi kwamba bajeti yetu hii haikuongezwa kodi yoyote kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo pongezi hizi nazitoa kwa dhati juu ya maendeleo kwa jamii ambayo inatutegemea kwa serikali yetu hii tuliyokuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii ina sehemu nyingi, naamimi wizara zote ni tegemezi kwa wizara hii bila ya Wizara ya Fedha hakuna wizara yoyote itakayofanyakazi. Kwa hivyo mimi namtakia sana kheri Mhe. Waziri na watendaji wake wote kuanzia Katibu Mkuu na wengine wote, kuhakikisha kwamba Taasisi zinazohusika na fedha zikusanye fedha hizi kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme kwamba katika zingatio kubwa lilionekana katika bajeti hii, mimi nampongeza sana Mhe. Rais kwa kuona kwamba elimu na afya ni jambo muhimu katika nchi. Elimu na afya, kwa hivyo bajeti yake ya mwaka huu naweza kusema kwa mara ya kwanza imepindukia asilimia 30. Hivyo niseme hili ni ongezeko hili ni zuri na linafaa kupewa mfano na kuigwa katika sehemu zake zote ili kwamba taasisi hizi za elimu na afya zifanye kazi zake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya elimu hakuna maendeleo katika nchi yoyote duniani na bila ya afya huwezi hata kuipata hiyo elimu. Kwa hivyo ushirikiano wa wizara mbili hizi ni muhimu kuhakikisha kwamba elimu inapatikana na madaktari wanapatikana, lakini nyezo zinazostahiki kwa wananchi dawa na mambo mengineyo zinapatikana vilivyo kuondoa usumbufu ambao huko nyuma ulikuwa mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nampongeza sana Mhe. Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha na watendaji wake wote kuliona hilo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Tumeshuhudia sasa hivi, pamoja na mambo mbali mbali yanayoendelea katika mazingira yetu haya mawili, kwenye elimu serikali inajitahidi, inaongeza masekondari na vyuo mbali mbali, lakini na ukija afya imeingia katika ugatuzi, ugatuzi maana yake, umetusaidia wizara mbili kwa pamoja. Kuna Wizara ya Afya wenyewe na Wizara ya Tawala za Mikoa na Idara maalum. Kwa hivyo niseme kwamba changamoto za Wizara hizi mbili tunaamini vituo vyetu ambayo tunavyo katika maeneo yetu vitasimamiwa vyema kupata huduma zote zinazostahiki madawa na mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala ambalo linasikitisha *tender*. Hizi *tender* zinapotokea katika sehemu zetu hizi za mawizara mbali mbali, maana sisemi elimu wala afya tu na kwengineko, mara nyingi huwa ni kero na baadae kupata usumbufu, inaweza kutolewa *tender* nzuri kwa ujenzi wa maskuli mbali mbali, lakini inaweza kutolewa *tender* hiyo kwa mawizara mengine mbali mbali, majengo yao hayastahiki. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Hamza Hassan Juma baada ya kutoa taarifa nzito ambayo taarifa ile ni muhimu kwetu sisi tuliokuwemo humu kwa faida ya serikali yetu kuilinda na baadhi ya wabadhirifu, kwa sababu *Tender Board*, *tender* yote haisimamiwi na waziri au *tender* haisimamiwi na Rais, *Tender* inasimamiwa na watendaji, mara nyingi watendaji ndio wanaorudisha nyuma maendeleo haya, labda kwa bahati mbaya kwa tamaa yao ya hapa na pale, baadhi yao sio wote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo niseme suala la *tender* liangaliwe kwa hali na mali ili kunusuru pato la nchi yetu na kinachojengwa kidumu angalau miaka thamanini au mia moja. Mhe. Mwenyekiti, leo katika majengo yetu mengi ukiacha nyumba yangu mimi au yako wewe au yeyote aliyekuwepo, inaweza kuishi miaka kumi nyumba ya mtu lakini jengo la serikali lililojengwaa halizidi miaka miwili au mitatu linavuja na linaleta uharibifu. Kwa hivyo hii inaonesha dhahiri kwamba hakuna udhibiti, hakuna imani kwa baadhi ya watendaji, na hii ndio

changamoto ambalo mimi huwa naona ajabu na huwa sipendi Mheshimiwa, katika bajeti za wizara mbali mbali utasikia wizara fulani inafanya ukarabati wa kitu fulani mwaka huu na mwaka ujao unafanya ukarabati tena. Hizi karabati karabati zinaumiza pesa zeu, kwa hivyo tuseme kwamba ukarabati ufanywe angalau udumu miaka mitano au miaka kumi lakini ukarabati wa kila siku Mheshimwa baada ya kwenda mbele tunarudi nyuma, fedha zina mambo mengi, tunataka madawa, tunataka elimu, tunataka maji safi, tunataka barabara na mambo mengineyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri wakati wa *Tender* hawa watendaji wetu wawe waadilifu na waangalifu kwa maslahi ya wanachi wetu wanchi hii.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Suala la madawa yaani dawa za hospitali sio za kulevya, za kulevya yatazungumzwa baadae. Mhe. Mwenyekiti, tumesema kwamba Mhe. Rais kwa kuongeza bajeti hii wameangalia sana tatizo la madawa katika vituo vyetu vya afya na hospitali zetu. Kwa hivyo mimi naipongeza serikali kwa kuona kwamba bajeti iliyoongezwa ni suluhisho la kuondoa matatizo ili kupata dawa katika maeneo yetu mbali mbali na wananchi wetu kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, tukiri kwamba wafanyakazi wetu wa Bohari Kuu wapo na wanafanyakazi mbali mbali, ni vyema watembelee katika taasisi mbali mbali, vituo vya afya na hospitali mbali mbali kukagua na kuona je, dawa zinapatikana kiasi gani na zimepungua kiasi gani, kwa sababu wakati imeshaambiwa dawa zinatoka bure, leo mwananchi anakwenda pale ana imani kwamba anapata dawa na shilingi 100 hana, anaondoka pale anaambiwa kanunue Darajani, kanunue Muembeladu, ile Mheshimiwa haileti imani. Kwa hivyo niwaombe wafanyakazi wa Bohari Kuu watembelee vituo mbali mbali kuona je, kuna upungufu gani wa dawa hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye Shirika la *ZAWA.* Mimi nampongeza sana Mhe. Rais na nilisema siku ya Wizara ya Ardhi, Maji Nishati na Umeme. Nimesema sana nampongeza Mkurugenzi mpya, tena namponge kwa asilimia 300 au 400, ni muungwana ana imani na nchi hii ana imani na wananchi wanyonge wa nchi hii. Nampongeza sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hakuna jambo baya katika maisha ya binaadamu kuliko kuliona zuri ukalikejeli, Mwenyezi Mungu hayupo na wewe, zuri litaje zuri na liseme zuri, la mashaka lielekeze. Kwa hivyo nasema toka kuja Mkurugenzi wetu huyu mpya, mabadiliko katika sekta ya maji imebadilika, tena imebadilika kwa asilimia kubwa Mheshimiwa. Mimi jimboni kwangu napiga kelele kila siku katika Jimbo la Kijitoupele lina matatizo ya maji na toka ilipojengwa barabara yetu ya Mwanakwerekwe hadi leo kuna maeneo mpaka leo hayajapata maji, lakini kwa maeneo mengine wanapata, lakini niseme tu kwamba mabadiliko hata katika utendaji wao wa kazi na watendaji wake wale wasaidizi wake wako bega kwa bega, tumemshuhudia Mkurugenzi huyu kwa macho yangu yuko kwenye *field,* bomba kubwa limepasuka kaacha ofisi yupo kule na watendaji wake ile ndio inavyotakiwa.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi nampongeza na nitazidi kumpongeza kila panapostahiki, na mimi nasema tu kwamba imani yake aliyotuonesha, tuna imani ya muda mfupi ujao tatizo la maji litaondoka sehemu mbali mbali. Kwa hivyo tuseme katika utendaji Mheshimiwa mwalimu mzuri mzuri mwanafunzi anakusifu, na akikija mwalimu pale hafahamiki anaanza kuchukiwa. Kwa hivyo mimi nampongeza imani yangu safi na tuko bega kwa bega, na tunahakikisha wengi tuliokuwemo humu tumejenga imani na yeye. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu amzidishie imani, amzidishie uwezo afanyekazi zake kwa manufaa ya wananchi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nitalozungumza hapa ni suala la Shirika la Bandari. Mheshimiwa katika nchi yeyote duniani inategemea maeneo yake ya kupitisha uchumi au bidhaa kwa ajili ya uchumi wa nchi. Mimi nawapongeza sana Shirika la Bandari kwa kazi zao nzuri wanazozifanya na bidii yao tunaiona usiku na mchana, Lakini pia tuseme kwamba tegemeo letu la nchi yetu ni bandari. Kwa hivyo bandari yetu tukitaka tusitake imeshapitwa na wakati kuwa ndogo. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, yeye na Wajumbe wa Baraza la Mawaziri, kwa kufanya ziara maalum ya kuangalia Mpigaduri. Je, kunastahiki, kwa hivyo ile ishara moja wapo kusema tu kwamba bandari yetu ikifanyiwa upembuzi yakinifu, imeshafanyiwa lakini ikijengwa upya hiyo mpya tunayoitegemea basi maendeleo ya uchumi yataongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nilikuwa na rai nyengine kwa serikali ili kuongeza mapato. Mhe. Mwenyekiti, serikali inategemea mapato lakini tukisema tuna Uwanja wa mpira wa *Amaan Stadium* tu peke yake, hatufiki ukipeleka *Mao-Tse-Tung*, ukipeleka Uroa, ukipeleka Makunduchi. Sasa ile ni kutanua bidhaa, kwa sababu wachezaji wanakwenda katika maeneo mbali na timu zinakwenda mbali mbali, hapa yataingia mapato na hapa yataingia mapato. Maana yake nataka kutoa ushauri ufuatao.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Tanzania Bara kila Mkoa una Uwanja wa Ndege Viwanja vya Ndege. Kwa hivyo yale ni mapato ya nchi, lakini pia bandari ndogo ndogo ziko nyingi zinazotoa huduma, ukenda Lindi, Mtwara, Tanga, ukenda hata maziwa mbali mbali unazikuta bandari, ile ni ufanisi wa ajira na ufanisi wa kuingiza fedha. Kwa hivyo huko mbele tunakokwenda labda serikali ifikiri tufanye nini ili vijana wapate ajira ili pato la nchi liongezeke.

Mhe. Mwenhyekiti, mimi ushauri wangu kama itawezekana Nungwi au Mkokotoni, ikajengwa bandari kubwa sio bandari ndogo iliyoko sasa hivi, najua watu wanaotoka Pemba wanaweza wakenda mara tatu kutoka pale Nungwi kwenda Pemba na kurudi bidhaa zikawa rahisi kuingia pale, na bidhaa zikiingia Nungwi wenye magari wanafaidika na biashara na ongezeko la ajira linaongezeka, lakini pia ukiende Kusini, ikiwa Kizimkazi, mawazo yangu, ikiwa Kizimkazi panafaa kujengwa bandari pajengwe bandari, anayetoka Dar es Salaam pale kutwa mara tatu, nne anakwenda hiyo ni kutanua biashara lakini tukin'gang"ani bandari kuu ya Zanzibar, mjini Unguja tu hatufiki.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanataka ajira, ikijengwa bandari Kizimkazi vijana wengi watapata ajira, ikijengwa bandari Nungwi, maana wanaotoka Mkoani tutapigana vikumbo umo kwa umo. Kwa hivyo Mheshimiwa tubadilike tusin'gan'ganie mjini tu, mjini hapatoshi sasa hivi. Lakini nakwambia kama kutakuwa na bandari Nungwi, Kizimkazi kwa wakwe zangu, nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira litaongezeka kwa vijana na bidhaa zitaongezeka katika nchi yetu na yale aliyoyazungumza Mhe. Jaku akasema tu kwamba mimi naungana naye biashara asiachiwe mtu mmoja, biashara kuachiwa mtu mmoja fitna, kwa sababu mwisho atafanya anavyotaka na hiyo iliwahi kutokea.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafanya biashara Mwenyezi Mungu amrehemu kaka yangu Ali Macho, alikuwa anaagizia bidhaa mbali mbali, unga ngano, sembe na vitu vyengine vinaletwa hapo Gulioni. Mhe. Mwenyekiti, kufika yule bwana mkubwa mmoja simtaji, akasema bidhaa

yote naleta mimi sasa hivi, alipoleta yeye, kwa kuwa yeye kaleta kwa kuwauwa wale, ilikufa moja kwa moja na akabadilisha *clinic* yake ile pale ya kituo cha afya, hakufanya tena biashara hiyo, aliwauwa watu wetu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hakuna nchi inayokubali mfanyabiashara akawa mmoja na ndio maana uhusiano mwema na utawala bora, kila mtu awe rafiki yako na wafanyabiashara ndio tunaowategemea kuongeza pato la nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, tukiri kwamba kama mfanyabiashara mmoja anaachiwa kila kitu alete yeye hapa, ule mkate tunaonunua Shs. 250/-, shs.300/- utafika shs.500/- na shs.1000/- kwa muda mfupi ujao, ameshakuwa huru. Mhe. Mwenyekiti, mimi siungi mkono hilo, nataka lazima twende kutokana na wakati tuliokuwa nao, biashara huru, sekta binafsi huru, kila mtu mwenye uwezo alete mchele. Kama Mhe. Jaku alisema yeye atajenga sijui Kiwanda cha Unga na mimi sijui nitafanya nini, lakini na mimi ninafikiri nitamtafuta mhisani yeyote, tuweke ili bidhaa yetu tuilindie sisi, haielekei Mhe. Mwenhyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, tukiri kwamba wananchi wetu ni wanyonge na wananchi wanategemea kila pakiwa na ushindani wa biashara au wafanyabiashara ile kuongezeka bei ya bidhaa haiongezeki, kwasababu wewe utauza bei ya chini iishe uagizie vyengine. Ombi langu tu kwa Mhe. Waziri namuomba sana tuangalie usalama wa bidhaa zetu, tuangalie usalama wa mambo yetu tuliyokuwanayo katika nchi yetu. Nawaomba wafanyabiashara wote waitikie wito huu kuhakikisha kwamba bidhaa zinaingia kwa wingi, bidhaa zenye heshima na bidhaa zinazolinda usalama wa wananchi wetu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nawaomba tuendelee na tufanye hivyo, lakini jengine nakuja kwenye kukusanya mapato. Mimi niwashukuru sana *ZRB* na *TRA* kwa kazi nzuri wanayofanya na kuhakikisha kwamba katika kazi zao wanaongeza pato la nchi yetu kwa usalama na kuhakikisha kwamba uwezekano wa serikali zake inafanya vizuri, tunahakikisha kwamba wao tunawategemea na serikali inawategemea. Lakini mpaka sasa hivi tuseme tu kwamba tunashukuru Mhe. Waziri katika bajeti yake amesema tu kwamba safari hii katika ukuaji wa pato la Zanzibar, pato letu Inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie twende vizuri, hali ya hewa iwe nzuri, tusimamie vizuri, tuna asilimia 7.7 ambayo ni asilimia nzuri tunahakikisha kwamba tutakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine niseme tu kwamba pamoja na yote serikali tuwe kitu kimoja kuanzia Mhe. Rais jitihada zake tunaziona na Mawaziri tunawaona na wasaidizi wao tunawaona, kama tunavyowaona sasa hivi hawa akina *ZAWA* na wengineo. Mhe. Mwenyekiti, nasifu na tuwasifu kweli kweli, lakini kubwa zaidi tushirikiane na tuwe na uchungu na tuwe na imani na nchi yetu na hakikisha tutafanikiwa kwa muda mfupi ujao.

La mwisho, nakuja kwenye ushauri serikali narudia tena kila leo inajenga barabara kwa kutumia mabilioni ya fedha, lakini bahati mbaya tunapopatana kujenga barabara vikuta vile vya pembeni kuzuia mmomonyoko hatuviingizi. Barabara zetu za ajabu na zinakatika siku hadi siku, kila mvua zikija pembeni zinamong'onyoka zinakatika ukipitisha gari kama msumeno unaua barabara lakini kama tunajenga vile vikuta. Labda nimuombe Mhe. Waziri wa Miundombinu ipo barabara ya Kajima iliyojengwa kutoka Kinazini mpaka Bububu aitembelee. Toka miaka ya sabiini mpaka leo iko hai barabara imara, lakini barabara zetu mimi hiyo yangu ninayojisifu

ninayotaka kumwambia Mhe. Waziri suala lile silitoi anijengee matuta na yeye twende pamoja wananchi alau waridhike, maana hapa pahala pananiuma sana Taveta watu wanakufa ovyo, watoto wanakufa kwa ajili ya mwendo kasi madereva wanaokwenda katika barabara hiyo.

Kwa sababu alama zipo lakini Mhe. Waziri alama hizo utazaijua wewe na mimi, vijana wa leo hawajui alama hawajui chochote, siku nyingine weshapachika vitu vyao kichwani ndiyo zaidi wanahatarisha amani. Kwa hivyo nimetoa ushauri barabara zijengewe vikuta Mheshimiwa kama tumejenga barabara bilioni nane mfano au bilioni mia mbili si ajabu kujenga milioni mia tatu ukaweka vile vikuta ikawa kazi imekwisha, barabara inachukua muda mrefu inaishi. Lakini baada ya hayo Mheshimiwa niseme tu kwamba tukiri katika hii historia ya bajeti yetu na mimi nimekaa Barazani itakuwa hiki kama kipindi changu cha nne, bajeti ya mwaka huu nzuri na bajeti ya mwaka huu ni ya wananchi kama wanaelewa wanatuelewa imewaondolea adha, imewaelekeza vizuri kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu, Wizara ya Kilimo na mambo mengineyo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuliona hili, ombi langu tulisimamie vyema ili tupate faida kwa manufaa ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Baada ya hayo Mheshimiwa niliyozungumza machache niseme mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wote wa jimbo la Kijitoupele ambao wanaonipenda na wasionipenda maana kuna wengine watakupenda wengine hawakupendi, lakini wanaonipenda asilimia kubwa tu naunga mkono asilimia 100 na sina tatizo na Mhe. Waziri, lakini niliyoyazungumza yafanyiwe kazi kwa manufaa ya wananchi wetu wa Zanzibar ambao wanaitegemea serikali yao hii ya Chama Cha Mapinduzi.

Baada ya hayo nasema ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatiwa na kama muda utaruhusu basi Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nianze kuchukua fursa hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu ili na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu niweze kutoa mawazo yangu kuhusu mapendekezo ya bajeti ya serikali na makadirio ya mapato ya matumizi ya mwaka 2018 kuelekea 2019. Lakini nichukue nafasi hii pia kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake aliyoisoma wiki iliyopita na niseme kama msemaji aliyepita kwamba bajeti hii na hotuba aliyosoma ni kweli ni hotuba au bajeti hii ni kwa ajili ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nikiwa Mwenyekiti wa Jumuiya za Mabunge za Nchi ya Madola au *Commonwealth Paliamentary Association,* nachukua nafasi hii kuwapa pole wafanyakazi wa Shirika la Bima Zanzibar kwa kufiwa na Mhasibu wao ambaye mwaka huu katika sherehe zetu za Bunge la Vijana walituunga mkono. Kwa hivyo *inshallah* Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema, Amiin.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niseme katika bajeti hii kuna mambo kadhaa nimefurahiwa nayo. Moja ni suala zima la kuanzishwa kwa *Industrial Park.* Pili kuongeza muda wa kulipa au kupeleka kodi kuanzia tarehe 15 sasa itakuwa tarehe 20, lakini pia usimamizi mzuri wa kodi ya

majengo, suala la mishahara, kuendeleza ujenzi wa bandari ya Mangapwani, lakini pia nitazungumza suala la mafuta na gesi lakini pia juu ya kuongeza bajeti katika sekta ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nianze katika eneo la kwanza ni kuhusu barabara ya kutoka Mkokotoni kuelekea zake mpaka Bububu, na kama msemaji aliyepita Mhe. Suleiman Ali Suleiman leo amezungumzia suala lile amependa kulikumbushia juu ya barabara na usimamizi na fedha tunazotumia. Na mimi nataka niseme kwamba tunapojenga barabara hizi ambazo kwa fedha nyingi tunazotumia basi mbali ya kuingiza suala la *pavement* au *pedestrian walk* ili wananchi waweze kutumia, basi tuweke zile bomba kabisa ambazo kwa ajili ya *utility.* Ninaposema *utility* tunaangalia kwa ajili ya umeme, bomba za maji, *fiber optic* kwa ajili ya *internet* na kwa ajili pia kuweka maeneo pia ya kupitisha gesi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani au *domestic consumption.*

Mhe. Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu tunapotayarisha hii mambo ya kuvunja na kujenga tena, tumeona lilizungumzwa hapa kwa ukali sana mwaka 2016 kwamba hapa tumerarua mawaya kibao ya mtandao, tumetandika waya kutoka Mwanakwerekwe wa *internet fiber optic* mpaka kwenda Fuoni umerarurirwa, na sasa hivi huu pia tunakwenda kurarua na Wizara hiyo hiyo ya Mawasiliano ndiyo itakayosimamia. Na maeneo mengine yatakuwa ndiyo hali kama hiyo. Sasa tuanze kuweka bomba chini ili wataalamu wetu waweze kuweka na naomba sana hili Tume ya Mipango walichukue kabisa ili tuhakikishe kwamba hizi bomba zinawekwa vizuri kwa ajili ya matumizi ya baadae na itakuwa tena hakuna haja ya kuvunja vunja.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie katika bajeti ya Mhe. Waziri mwaka 2016. Naomba nisome ukurasa wa 41 nanukuu haya alisema, "Aidha tunaomba Baraza liidhinishe matumizi ya bilioni 841.5 ikiwa 445 bilioni kwa matumizi ya kawaida na bilioni 355 kwa ajili ya kugharamia mpango wa maendeleo".

Hii ilikuwa mwaka 2016 kuelekea mwaka 2017, ukiangalia mwaka 2018/2019 kwenye ukurasa wa 59 anasema kwamba. "Kwa upande wa matumizi wa mwaka 2018/2019 nina heshima ya kuliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya shilingi trilioni 1 bilioni 315 na milioni 100, yaani *1.3 trillions*, matumizi hayo ni Tshs. Bilioni 700.2 kwa ajili ya kazi za kawaida na 613,000 bilioni kwa ajili ya mpango wa maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri sana la kheri nampa Mhe. Waziri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pongezi, Wazungu wanasema *Congratulations*, na kwa nini nasema hivyo. Kwa sababu sasa hata ukiangalia katika ile sekta ya afya, ukiangalia kutoka fedha ambazo zile za mwaka jana na ambazo mwaka huu zinaingizwa bilioni 12. Basi naamini Hospitali ya Mnazi Mmoja sasa mambo mengi na mageuzi ya wananchi wetu hata kule Pemba kwa Hospitali ya Abdalla Mzee, naamini sasa Mhe. Suleiman Sarahan na wengine wote Wajumbe kutoka Pemba wataanza kuona tofauti katika sekta ya afya ambacho pia siasa yote ipo pale lakini pia ni kilio cha wananchi wetu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine nataka niseme kumshauri Mhe. Waziri ni shamba la Bagamoyo. Mhe. Mwenyekiti, kasi ya watu kuzaliana kwa upande wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ukiangalia kwa wilaya zetu tunaongezeka kwa wingi. Lakini pia matumizi ya serikali kutumia

fedha kuwasomesha wananchi wake katika hasa suala la elimu bure, maji kuchangia kwa kiasi fedha ndogo lakini pia katika sekta ya afya, sasa lazima tuangalie katika upande wa sekta ya kilimo tunatafuta njia mbadala, tumeangalia masuala ya *irrigation*, lakini hili shamba hasa la Bagamoyo ambalo lipo chini ya Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuliangalia jinsi gani tunaweza tukalitumia. Wapo watu tunaoweza kuunganisha nguvu zetu kwa upande wa vikosi vyetu, tukaangalia tukaingia na ubia tukaanza kulitumia hili eneo ili tuweze kuzalisha, tukiweza kujenga ku-*link* biashara ya sekta ya utalii na kilimo, tunasema *value change analysis*, ukiangalia ile karoti ile inapotoka kule Lushoto Tanga mpaka inafika kwa mlaji Zanzibar unakuta imeshauzwa zaidi ya mara saba.

Sisi kazi yetu kuonesha kwamba wale madalali wa kati kati tunawapunguza *atleast* twende kwa watatu, ina maana utakuta karoti sasa bei yake na maeneo mengine yatashuka. Sasa katika kulinda mlaji na katika sekta hii tutakuta watu wetu sasa unapokwenda sokoni au Marikiti unapata vyakula kwa bei nafuu. Sasa tuangalie na vile vyakula ambavyo wananchi wetu wanataka wale, tusilime vitu kwa mazowea tuangalie vitu ambavyo wananchi wetu wanapenda kula. Kwa mfano mbaazi, zamani watu wengi walikuwa wanapenda kula mbaazi, wazee wetu walikuwa wanapenda kula mbaazi lakini mbaazi tumeacha tumekwenda kwenye maharage. Sasa ukiangalia leo Kusini mwa Tanzania mbaazi zimeshuka bei, lakini ukiangalia kwa upande wa Zanzibar kwa nini hizi mbaazi basi hatuendelei kuona kama ulivyokuwa tunaziona kwa wingi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo tuangalie maeneo kama haya lakini ukienda katika vitabu vyake hasa kile ambacho kinazungumzia juu ya muelekeo wa uchumi anazungumza kwamba suala la amani na utulivu limewekwa namba 7. Mhe. Mwenyekiti, hakuna nchi ambayo inayoweza kuendelea katika suala la uchumi wake bila ya kuwa na amani na utulivu. Kwa hivyo nashauri masuala kama haya yawe nambari moja katika kitabu chake, lakini pia kwenye idadi ya watalii nimefurahia sana haya yanayozungumzwa, lakini pia tunataka tutambue katika tathmini ya matumizi yanayokwenda katika masuala ya mafuta hasa tukiangalia mafuta ya taa, dizeli na petrol, *demand* yetu inaongezeka, vituo vyetu vinaongezeka. Ukiangalia sasa hivi Zanzibar kwa mfano gari aina ya *Noah* ambazo zinapakia wageni au *taxi* kama *Private hire* unakuta matumizi yake wanaotumia petroli ni mara kumi kuliko mimi ambaye ninaetumia kawaida. Kwa nini nasema hivyo, kwa sababu mtu anapoendesha gari anatia mafuta ya elfu hamsini au arobaini kutoka hapo mjini mpaka Nungwi, kwenda Paje, Kiwengwa, Michamvi ambapo ni katika eneo mbali kabisa kutoka Unguja Mjini zaidi ya kilomita sabini mpaka unafika kule maeneo ya karafuu.

Sasa utakuta *consumption one hundred and fourth kilometers* itakuwa ni kubwa zaidi, sasa unakuta sasa hivi matumizi ya petroli na dizeli yapo juu, sasa tuweze kutofautisha baina na tupate hizi takwimu nani anatumia zaidi ni wananchi wa kawaida au wanaotumia zaidi ni madereva ambao wanaotumia hizi *private hire.* Nashauri katika Tume yetu ya Mipango watuletee hizi takwimu ili na sisi tuweze kutoa ushauri mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *with holding tax* katika hotuba yako, mimi naunga mkono sana suala hili na nilienda kwa makini na katika watu ambao ni Wazanzibari najua tuna *fixed ratet* za *with holding tax*, lakini uangalie Mhe. Waziri pia katika hali za kawaida hasa wananchi ambao wanafanya biashara ndogo ndogo na wao pia wapewe elimu ya kutosha wasiumizwe, serikali hii ipo kwa ajili ya wananchi kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kwa hivyo tuwaangalie

watu wa chini zaidi katika mpango mzima wa *with holding tax* ili isiende sasa katika moja kwa moja tukaanza kuwaumiza watu tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze katika suala moja ambalo ni muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, unapozungumzia suala la uchumi wa nchi lakini pia unaangalia na sura ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, bado tuna changamoto ya suala la usafi wa nchi yetu. Ukiangalia mjini maeneo unayopita bado suala la taka taka zimeongezeka mjini kwetu na tunaona kuwa serikali inajipanga katika mambo mazuri sana mbele yetu, lakini suala la usafi ni suala moja ambalo la kulizingatia kwa umakini sana. Sasa unapopata jina baya ina maana linakupelekea sifa mbaya, naunganisha hapo kwamba unaweza kuona mipango mikubwa mikubwa lakini mtu anaandika vibaya katika mitandao kuhusu nchi yetu. Sasa naunganisha na hapo kuna suala la *FBME*. Mhe. Mwenyekiti, tuna wananchi wetu wengi sana wanadai fedha zao katika Benki ya *FBME* ambayo zamani ikiitwa *Federal Bank of Middle East* na kwa nini *BOT* wanachukua muda mrefu kuwalipa watu wao. Mimi nashauri Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika mipango yako inawezekana benki ya *FBME* inakuumiza wewe bila ya kujua.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mwananchi kila siku asubuhi saa 3.00 anakwenda pale kusubiri kama ni leo au kesho atapata fedha zake. Sasa hawa wananchi hao hao wanafanya biashara, wananchi hao hao wanatakiwa wende wachangie. Mimi nina jamaa yangu mmoja pale ana fedha nyingi ameweka ambazo amekuja hapa kuja ku-*retire* au kuunga mkono sera ya DIASPORA ambayo inayopigiwa debe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini kutokana na maisha yake sasa anafikiria kuondoka. Sasa kiasi gani cha fedha ambazo zimekwama za wananchi *FBME* zitachangia katika kuuimarisha uchumi wetu. Sasa lazima Mhe. Waziri usimame ufuatilie haya ukazungumze na Gavana wa Benki Kuu ili tuweze kujua nini tunafanya na wananchi wana hamu ya kuyasikia. Najua ulijibu swali hapa Barazani lakini suala la fedha benki ya *FBME* inatosha, tunaiomba sasa serikali ikaze buti juu ya *BOT* watupe majibu sahihi kabla sisi hatujaunda Kamati Teule kufuatilia hili suala na ninaamini Mhe. Hamza na wengine huku nyuma wataunga mkono haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo langu la Tunguu ukianza kutoka Kisiwa cha Uzi unakuja zako Unguja Ukuu mpaka unapita Kikungwi, Bungi mpaka unakuja upande wa Kibele, Mhe. Mwenyekiti, kuna simu inalia na inaniingilia, baada ya hapo unakuja zako moja kwa moja mpaka Kibele, ukiangalia maeneo haya yote kuna kasi ya ujenzi mkubwa sana na Jimbo la Tunguu lipo *South Centre*, maana lipo kati kati, limepakana majimbo karibu sita, kama Fuoni unaangalia Chwaka, Uzini, Paje, Dimani.

Sasa ukiangalia kwa mfano kwa jinsi ambavyo ni muhimu kwa nchi yetu hii hasa kwa Kisiwa cha Unguja ni muhimu Mhe. Waziri katika suala la miundombinu ukaangalia na kutupa kipaumbele katika maeneo ya kilimo, kuwasaidia wananchi katika sekta hasa ya vijana wetu katika kuwaendeleza na kuangalia ni pengine katika maeneo yote. Magari yanapita mengi wanatumia barabara zetu ambazo zinapita pale ni za Zanzibar, natambua kwamba kwa upande wa Jimbo la Tunguu tuna changamoto katika uchangiaji wa fedha hasa katika Serikali Kuu. Lakini pia nashasuri basi ili kuwasaidia vijana wetu Halmashauri ya Wilaya ya Kati waanzishe kuweka takwimu juu ya fani za vijana ambazo wana uwezo ili tuweze kuwaunganisha katika sekta tofauti. Kizungu wanasema *Job Center* nimezungumzia mwaka 2016 hadi leo hakuna maendeleo yoyote, narejea tena kusema *issue* ya *Job Center* kwa vijana wetu ili tuweze kujua

vipaji vyao na tuweze kuwaunganisha, sio kwa kutegemea sekta ya ajira serikalini lakini lazima tujenge utamaduni kwamba ajira pia tunaweza tukawasafirisha vijana wetu kwenda kutafuta kazi katika maeneo ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nizungumze suala la meli, ukiangalia bajeti au suala la biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara mwaka 2016 tulikuwa tunapeleka bilioni 84.7 kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Mwaka 2017 tumeshuka mpaka bilioni 33.6. Sasa tuangalie ni kitu gani kinachofanyika lakini ukiangalia biashara kutoka upande wa Tanzania Bara kuja Zanzibar imeongezeka ni tatizo hapa kama alivyosema Waziri wa Biashara Mhe. Balozi Amina Salum Ali amekiri ni kwamba kutokana na tofauti ambazo zilizokuwepo za kibiashara ambazo hasa katika masuala ya kodi. Sasa mimi nashauri binadamu kumtegemea cha ndugu hufa maskini lakini katika biashara ni ushindani.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kwa upande wa Zanzibar na upande Tanzania Bara tuna chumi zetu hizi tofauti, sisi ni *service oriented* tunategemea *tourism, trade and business,* lakini kwa upande wa Tanzania Bara wana *agro,* wana *banking* wana *telecom* wana *mining,* wana biashara nyingi sana. Sasa na sisi lazima tu-*divert* ili kwa kufanya hivyo tuanze kuangalia upande wa Mombasa, tuanze kufanya biashara na Kenya. Kwa hivyo mimi nashauri jambo la mwanzo kama Mhe. Said Bakhersa amejitolea kujenga bandari Mombasa, mimi kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Tunguu namuomba basi Mhe. Waziri a-*facilitate* hiyo *process* kama mtu yuko tayari kujenga bandari Mombasa, SMZ isimamie na kumshika mkono ili tuanze kufanya biashara baina ya sisi na Kenya na kwa vile biashara na *goods* ambazo zitakuwa zinatoka Kenya zitakuwa *VAT exempted,* basi Wazanzibari watakuwa wanaweza kufanya biashara baina ya pande zote mbili Unguja, Mombasa, Tanga pamoja na Dar-es-Salaam, lakini leo huwezi kutegemea eneo moja kila siku, leo takwimu zinaonesha hizi siyo takwimu zangu ni takwimu za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa leo unatoka mtu kutoka Tanzania Bara unapigwa 19 *parcent VAT* unafika Zanzibar *ZRB* anakusubiri unakiangalia tayari mfanyabiashara anaanza kuuza bidhaa yake ameshalipa *VAT 36 parcent, is too much. K*wa hivyo lazima tuangalie mbadala. Hivyo Mhe. Waziri kwa hisani yako nakuomba uliangalie hilo ili tu-*check* tunaweza kufanya biashara vipi na hao ndugu zetu pembeni.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukisoma ukurasa wa 64 wa kitabu cha muelekeo wa uchumi nimeona humu kwamba tayari upande wa Pemba zitanunuliwa zile *land craft* hasa kuunganisha watu katika visiwa vidogo vidogo kama mfano Fundo, Uvinje, Kokota, Makoongwe, Kisiwapanza, Kojani na Tumbatu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, na mimi jimboni kwangu ninacho Kisiwa cha Uzi na kisiwa cha Uzi Mawaziri wengi hawajafika pamoja na watendaji na kule wananchi wanaunga mkono Chama Cha Mapinduzi kwa upande hasa wa Ng'ambwa ijapokuwa kwa upande wa Uzi wapo wengine ambao hawana uhakika na chama chetu. Lakini mwisho wa siku serikali inayokaa madarakani ni kwa ajili ya wananchi wote. Mimi naomba sana kwa upande wa barabara kutoka Ungujaukuu kuelekea Uzi imekuwa ni balaa kwa wananchi, hasa ukizingatia mbali ya usafiri lakini upande wa maji. Kwa hiyo, moja ya kaya maskini katika jimbo langu ni hilo. Lakini nayo maeneo ya Mwera/Pongwe, barabara ya Jumbi/Koani wafanyabiashara najua kwamba utaratibu umeshaanza lakini wananchi wanapata tabu. Sikukuu upande wa Mwera kwenda Pongwe wameshindwa kufika mjini na

hili eneo haliko mbali, kutokana na usafiri barabara imeharibika, barabara mbovu kwa hiyo changamoto zinakuwa nyingi kama hizi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni *issue* ya *Skill Development Levy (SDL).* Mhe. Mwenyekiti, ukienda kwenye suala la *SDL* kwenye *Educational Institution* au taasisi ambazo zinasaidia na zinaunga mkono suala la elimu. Ukiangalia wanalipa upande wa *TRA*, upande wa Tanzania Bara *SDL* wameshaondoa katika sekta ya elimu hasa katika hizi *private schools*, lakini Zanzibar bado wanachangia *SDL*. Lakini hawa wa *private schools* wanatakiwa wao waunge mkono. Sasa ni kwa nini *SDL* isiondolewe katika hizi *private institution* ambazo zinachangia katika suala la elimu, ili ile fedha tutakayoipata iweze kuwasaidia wananchi. Kwa hiyo, mimi nashauri Mhe. Waziri hilo jambo ulibebe ili uangalie ni njia gani tunaweza kufanya kazi kwa pamoja.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme suala la elimu katika maeneo ya Zanzibar, ili tukitaka kuwasaidia wananchi wetu, tukitaka tuwaendeleze tuangalie *trend* ya Zanzibar ni maeneo gani ambayo tunasomesha, changamoto zilizokuwepo kwenye suala la elimu ni Kiingereza na Hesabu. Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu ambayo iko makini itoe nafasi kwa wazee pia ipige debe ifuatilie, isimamie kwamba *parental guidance* kusimamia watoto wao hata katika kuzungumza Kiingereza majumbani mwao, ikawapa nafasi pia na kuwajengea *confidence* watoto wetu ili wanapokuwa wakubwa waweze. Lakini leo unakuta mtu ana-*cram photosynthesis* ana-*cram chloroform* ana-*cram digestion* lakini maana yake hajui tayari yupo *form II*. Kwa hiyo, lazima wanachokisoma wakielewe.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kutumia muda mrefu sana ili na wenzangu wapate nafasi, nafikiri baada ya mchango huu nilioutoa kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi kuweza kutoa mchango wangu huu, niombe sasa kwamba Mhe. Waziri katika maeneo ambayo nimeyazungumza atayafanyia kazi, pamoja na serikali nzima kwa ujumla.

Lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu nashukuru sana kwa mahusiano ambayo nayapata kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mawaziri wote, hasa katika maeneo tofauti elimu, afya, maji pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango. Niseme kwamba bajeti hii kama alivyosema awali ni bajeti ya wananchi, mimi naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu asilimia mia na sina tatizo. Namtakia Mhe. Waziri, kila la kheri katika utekelezaji wa hili na usimamizi mzuri na *inshaallah* fedha hizo trilioni 1.3 atakuwa nazo. Kama tulivyoondoka kwamba tunaondoka na utegemezi wa *General Budget Support (GBS)* sasa tutakuwa tunafanya mambo sisi wenyewe kama SMZ inavyotaka kuyafanya.

Baada ya hapo nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekit: Ahsante na mimi nakushukuru Mhe. Simai Mohammed Said kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma, atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo kuweza kusimama mbele ya Baraza

lako hili, ili kuweza kuishauri serikali, lakini vile vile kuchangia baadhi ya maoni ya serikali katika bajeti yetu kuu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla sijaingia katika mchango wangu nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuteua Tume ya Uchaguzi ambayo ni tume yenye wajumbe ambao ni makini sana. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wale kwa kweli ni watu ambao hatujawahi kusikia dosari yao hata moja, ni watu ambao wameitumikia serikali kwa muda mrefu, kwa hiyo naamini wataendelea kulinda ile heshima yao ya uadilifu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nataka tena nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Khalid Salum Mohamed, lakini vile vile na Katibu Mkuu Ndg. Khamis Mussa, pamoja na timu yao yote ya Wizara ya Fedha. Mhe. Mwenyekiti, leo tunazungumzia Bajeti Kuu ya Serikali tunajaribu kuyaboresha na kuyatolea msisitizo na miongozo yale yote ambayo tuliyoyapitisha katika bajeti za wizara mbali mbali. Kimsingi ukiangalia mazingira bajeti tayari tulikwisha kuipitisha leo tunakuja kupitisha ule ujumla wake, kwa hiyo kwa kweli baada ya kusoma vitabu hivi viwili vya Mhe. Waziri, kuwasilisha mwelekeo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2018/2019, lakini vile vile na kitabu chake cha mapendekezo ya Bajeti ya Serikali katika mwaka huu wa 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nataka niseme kwamba Dkt. Khalid Salum Mohamed ni Waziri ambaye msikivu sana, na nataka niseme ni msikivu kwa sababu wakati mwengine wengine tulikuwa tunaonekana wakorofi sana. Lakini ukorofi wetu leo sasa hivi Mhe. Waziri hapa ameonesha katika kitabu chake ni namna gani serikali yetu walivyoweza kuongeza mapato kuanzia yale ya kodi, lakini mapato yasiyokuwa na kodi, lakini mpaka mapato ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwapongeze Mawaziri wote kwa kuweza kusimamia vizuri watendaji wenu na mpaka sasa hivi wakawa wameleta nidhamu ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato, mpaka leo kwa kweli serikali yetu bajeti hii tunajivunia sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze moja kwa moja katika bajeti hii kuhusu suala la mfumo. Mimi naungana na hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya kusema kwamba bado kiti chako tuangalie kanuni zetu, ili sasa baada ya kuletwa hizi bajeti za wizara kwenye kamati, lakini wajumbe tuwe na nafasi ya kuweza angalau kurekebisha japo mambo machache. Lakini bado kama hotuba ya Mwenyekiti ilivyosema mfumo wetu huu inakuwa ni vigumu kuleta mapendekezo kwa sababu kama ukiangalia bajeti ya mwaka huu namna mapato ya serikali yalivyokuwa, ukenda kiasilimia karibu maeneo mengi wamekwenda zaidi ya asilimia mia moja. Sasa tulitegemea kile ambacho kilichopatikana kirudi moja kwa moja kwa wananchi kiende kikawasimamie. Tunajua kinarudi kwa wananchi lakini tulipendekeza kwamba katika lile suala zima la mfuko wa jimbo *atleast*, maana yake hili tulikubaliana na Mhe. Rais alilikubali kwamba kila mapato yatakapoimarika basi na mfuko wa jimbo tutakuongezeni ili mkarekebishe yale mambo madogo madogo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tumeshindwa kufanya hivyo kwa sababu kutokana na mfumo wetu ambao tunakwenda nao kwamba ukishapitisha bajeti za wizara zile ina maana huwezi ukafanya nyongeza nyengine katika yale maeneo ambayo mnahisi. Kwa hiyo, hili naliomba kiti chako likifanyie kazi, lakini pia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango akisikie hichi kilio chetu na kwa

sababu yeye mwenyewe ni Mwakilishi wa Jimbo la Donge. Tunaamini ndani ya jimbo lake kuna miradi mingi ya wananchi, kuna mambo mengi ya wananchi yanataka kufanyiwa kazi, lakini bado ile keki aliyoipata ya milioni ishirini yeye mwenyewe katika ule mgao kichwa kinamuuma. Kwa hiyo, kwa kuwa hichi ni kilio chetu cha pamoja naamni ataweza kukisikia na atakipeleka kunako husika, naamini Mhe. Rais ni msikivu ataweza kutuelewa katika hili.

Lakini kupitia hilo Mhe. Mwenyekiti, leo Makamu wetu wa Pili wa Rais hayupo, lakini Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa atatuchukulia kilio chetu hichi atupelekee kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ili sasa tupate kumuona bosi wetu Rais wetu Baraza la Wawakilishi kipindi kirefu hatujamuona. Sasa hivi leo tupo kati na kati tunataka tumpongeze kwa mambo mengi aliyoifanyia nchi, lakini vile vile tumpongeze kwa mambo mengi aliyotufanyia sisi.

Kwa hiyo, pia tutapata nafasi angalau ya kuonana nae kupeana mkono na kupenyeza maombi yetu mengine. Kwa hiyo, nafikiri Mhe. Waziri umenisikia, lakini Naibu Waziri hapa yupo salamu zetu atatupelekea kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, naamini Mhe. Rais zitamfika salamu zile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na ukurasa wa 24 kifungu cha 26 katika kitabu ambacho Mhe. Waziri ametuletea. Kwa sababu hapa tuna vitabu viwili kwa hiyo nakusudia hichi kitabu cha mapendekezo ya hii bajeti. Jambo ambalo nataka kulizungumzia Waheshimiwa Wajumbe naomba hebu tupitie ukurasa wa 24 kuanzia hii *paragraph* ya 59 mpaka ukurasa wa 25.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho ninachompongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango kulikuwa kuna kadhia kubwa ya deni la umeme Zanzibar baina ya *TANESCO* na *ZECO* na kwa kweli suala hili lilifika pahala likatuletea seke seke kidogo katika nchi mpaka wananchi wakataharuki. Lakini tunamshukuru sana Mhe. Rais wetu kwa busara zake aliwaagiza Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Mhe. Waziri wa Ardhi wahakikishe kwamba deni la *TANESCO* linalipwa tena katika kipindi kifupi.

Mhe. Mwenyekiti, umahiri alioutumia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango mimi nataka niseme kwamba sijui ana shahada gani, lakini kama hana PhD mimi nafikiri hapa tumpe PhD, kama hana, maana ana vitu vingi mwenzetu, Dokta ana kila kitu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ni kitu ambacho mimi mwenyewe nilikuwa najiuliza deni hili tutalilipa vipi katika kipindi kifupi. Lakini ukisoma na nikieleza maelezo mengi kwa sababu alikwisha kuyasoma na wajumbe waliyasikia hii *formula* aliyoitumia kwa ajili ya kulipa deni la umeme, naamini serikali yetu hapa itakuwa tayari imeshaumaliza mzigo wa deni la umeme kabla ya mwaka 2020.

Sasa hapa alitoa mapendekezo kwa wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango haya yasiwe maombi, haya yawe ndio malipo, kwa sababu Bara tunawadai pesa nyingi, kwa hiyo Dkt. Khalid Waziri wa Fedha amechukua madeni tunayowadai wao akawaambia basi haya ndio yatakuwa malipo yenu. Na madeni kwa kweli yako wazi ni fedha zetu ambazo zilikuwa ziingie Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazijaingia, tunawaambia sasa hizo pesa mlizokuwa nazo ndio tumeshakulipeni. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na tunakuombea sana kwa Mwenyezi

Mungu hizo hekma ulizokuwa nazo uendelee kujitahidi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akupe makubwa zaidi kuliko uliyokuwa nayo sasa hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu huu wa bajeti katika ukurasa wa 9 ameeleza Mhe. Waziri kwamba Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuja kulizindua Baraza la Tisa alituahidi kwamba anataka kuhakikisha tunataka kutengeneza na kumarisha nidhamu ya mapato na nidhamu ya matumizi, lakini vile vile kupunguza utegemezi kutoka nje kupitia kwenye bajeti yetu.

Lakini vile vile jambo jengine aliagiza Mhe. Rais kwamba anataka kuhakikisha serikali inakusanya mapato mpaka kufika bilioni mia nane mapato ya ndani kabla, yaani hii ni sera ya CCM ya *vision 2020*. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli baada ya kusoma au kumsikiliza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango mambo haya yote mawili tayari anayatekeleza kwa vitendo. Kwa kweli hali ya utegemezi tulikuwa tunategemea utegemezi mwaka 2015/16/17 karibu asilimia 11, lakini akaahidi atapunguza mpaka iwe asilimia 7, leo katika bajeti tunayokwenda nayo 2018/2019 anatuambia utegemezi utabakia asilimia 5. Kwa kweli hii ni *credit* kubwa katika nchi zetu za Afrika, mimi nadhani sijui kama Zanzibar sio kama sisi ndio tutakuwa tunaongoza.

Lakini vile vile mwelekeo wa makusanyo Rais aliagiza tufikie mpaka mwaka 2020 tuweze kukusanya bilioni 800, leo matarajio anatwambia tunategemea kukusanya bilioni 807 tayari tumeshavuka *vision 2020* hata 2020 haijafika. Sasa Mhe. Mwenyekiti, waziri huyu tena tumpe nini, maana yake lazima tutafute vitu vya kumpa, tumpe nini ukiacha haya mambo mazuri anayoyafanya na heshima gani tumpe. Kwa kweli Mhe. Waziri tunakuombea Mwenyezi Mungu aendelee kukupa hekima na busara, lakini vile vile na utulivu na usikivu kama ulivyokuwa nao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, siku za mwanzo mwanzo mimi najua Dkt. Khalid Salum Mohamed tulipokuwa tukiishauri serikali namna gani ya kukusanya mapato na mpaka wakati mwengine tulikuwa tunatumia lugha za kuudhi, ili waziri aache shughuli zake afanyie kazi kwamba namna gani yale mapato kuporwa porwa. Sitaki kuitumia tena ile lugha kwa sababu kidogo inaudhi watu kunyakua nyakua mapato ya serikali. Kuna lugha hapa Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora) alikuwa akiitumia sana lakini bahati nzuri sasa hivi kaenda huko huko lakini faida yake tumeiona. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mapato yamekua kwa kiasi kikubwa na hili kama ingelikuwa sio mashirikiano ya karibu, sitaki kusema kwamba hawana mashirikiano. Lakini takwimu na *trend* ndio zinavyotupa kwamba kama ingelikuwa bajeti zetu tunajitegemea *hundred percent,* kwa mfano tunapokwenda katika mikopo na misaada ya nje, kama ingelikuwa waziri wetu ana uwezo wa kwenda kule kwenye mikutano ya G8, akenda akapeleka mapendekezo ya Zanzibar tunahitaji msaada na mkopo wa aina fulani. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi *Terminal II* ingekuwa tumeshaimaliza, barabara ya Wete/Chake Chake ingekuwa tumeshaimaliza, miradi ya *Rehabilitation* ya barabara za Mkoa wa Mjini na Magharibi tungekuwa tumeshamaliza, bandari ya Mpigaduri tungekuwa tumeshamaliza na mambo mengine mengi, kuna sijui pesa za India.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kitu kinachoniuma leo nimejaribu kuangalia katika bajeti ya maendeleo fedha za wafadhili tumepata asilimia 40 hata asilimia 50 haijafika sababu gani. Sio

kama pesa hazipo, leo *donors* tayari fedha zipo kama mfano barabara ya Wete/Chake Chake *BADEA* pesa ipo kwenye akaunti. Leo Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kutia saini fedha zile zitumike kwa ajili ya kuondoa kero ya wananchi mpaka leo hataki. Fedha za Uwanja wa Ndege wa Zanzibar huo hapo Wachina wapo wanajenga wameshatishia wanasema mpaka ikifika kati kati ya mwezi wa Juni kwendea mwisho wa mwezi wa Julai hawajapata pesa wanaondoka. Leo Dkt. Mpango yuko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi narejea ile kauli ya Mhe. Mbunge Saada Mkuya aliyozungumza kule Bungeni akamwambia Waziri wa Fedha na Mipango katika mipango yako mbona Zanzibar haimo. Hii leo tunamthibitishia kweli Dkt. Mpango hana mpango na Zanzibar. *Why?* Mhe. Mwenyekiti, juzi nilimsikiliza sana Katibu Mkuu na namuomba Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kama alivyokwenda Bungeni na hapa kwetu aje azungumze na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Alizungumza maneno mazuri alisema ameshamlima barua Waziri Mkuu na vile vile atamlima barua na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Sasa tunamuomba Katibu Mkuu wetu wa CCM amlime barua Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amuulize miradi ya Zanzibar kwa nini hamuitii saini tukapata pesa tukaendeleza miradi yetu. Leo Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia bajeti inaangaliwa nini, bajeti ni mambo matatu, mipango, mapato na matumizi. Mipango tunayo imejaa kwenye vitabu leo tunazungumza miradi *Terminal II*, sijui tunazungumza bandari ya Mpigaduri zaidi ya miaka mingapi mipango tunayo. Lakini sasa katika mapato wenzetu wanayakalia. *Why?* Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango angalieni mpango mwengine namna gani ya kuweza ku-*finance* miradi yetu ya maendeleo, *otherwise* tutakuwa tunakuja kuzungumza vitu havitekelezeki, kesho tunakuja kuzungumza tena. Maana yake angalau kingekuwa kitu kimoja tungeambiwa labda Zanzibar pesa mnazitumia vibaya. Basi kwa miradi yote? Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nilisema nilizungumze kwa uchungu na ukali kwa sababu linaniuma na naumwa na maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kumpongeza sana Mhe. Waziri nakwenda haraka haraka naangalia katika kifungu cha 36 hichi sina haja ya kukirejea tena kwa sababu tayari bajeti yetu safari hii tutakwenda karibu trilioni 1.3 kutoka 1.087, tunawapongeza sana serikali.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika suala zima la Mfuko wa Miundombinu mgawanyo wake. Kazungumza mwenzangu Mhe. Simai Mohammed Said kama sikosei, lakini na mimi vile vile nilikuwa najaribu kuzungumza. Unajua Mheshimiwa katika Mfuko wa Miundombinu ukiangalia ule ugawanyo wa zile fedha, kuna fungu moja kubwa sana ambalo sipendi tena kulirejea, lakini najaribu kulirejea kwa sababu ili Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango mwakani anapofanya mgawanyo wa lile fungu aangalie kwenye lile fungu la *CCTV* ambalo limetengewa karibu bilioni 20. Tuna mambo mengi ambayo tunahitaji kufanya, fedha kwa kweli ni chache kama nilivyosema tunahitaji kufanya *rehabilitation* ya barabara zetu za ndani.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 44 kifungu cha 99, tunamshukuru sana Mhe. Rais baada ya ziara yake ya Falme za Kiarabu, tunategemea pale kuna mfuko wa *Khalifa Fund*. Hili naliomba sana Mhe. Waziri na timu yake wajaribu kulifuatilia kwa sababu tumeshuhudia kuna ziara nyingi sana za viongozi wetu wanakwenda nje ya nchi, wanakwenda wanafuatilia mambo na kuna ahadi zinapatikana lakini hakuna *follow up* na unajua wenzetu Waarabu hawa. Wenzetu Waarabu wana

mambo ya *hewallah,* inatakiwa kila wakati unamgongea hodi, hodi, hodi vipi bado? Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na watendaji wake najua juu wananisikia basi huu mfuko wa *Khalifa Fund* utaweza kutusaidia sana katika kusaidia ajira kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 45 katika kitabu chake Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma nikukumbushe dakika nne umebakiwa nazo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Eh! Mhe. Mwenyekiti, najua kuna zile dakika zako za busara kwa sababu hii ndio Bajeti Kuu ya Serikali. Naendelea kusisitiza tena najua dakika tano za kawaida lakini bado naomba unigaie na zile zako za busara.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la vipaumbele vya serikali, moja katika eneo ambalo limepewa kipaumbele ni eneo la Bandari ya Mangapwani. Pale mimi kitu ambacho nakiomba nashukuru kwamba serikali wanasema watatumia utaratibu wa PPP kwa kweli tunashukuru sana. Kitu ninachokiomba wale waliokuwepo pale naomba wapewe mikataba ili mtu ajijue atapata nini na atafidiwa vipi. *Otherwise* tunaweza tukaja tukaibebesha mzigo mkubwa sana serikali huko baadae. Ile *PPP* itakapofanyika pale kuna wadau ambao tuliwakuta watapata athari kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kama nilivyosema bajeti ni mapato na matumizi. Leo naishukuru sana serikali yetu katika vipaumbele kimoja walichokiweka ni suala la kuimarisha huduma za afya. Hapa nimeshasema na naendelea tena kusema, fedha nyingi sana zinakwenda Wizara ya Afya. Mimi nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo bado sijaridhika na huduma ambazo zinapatikana. Mhe. Mwenyekiti, mwaka uliopita tulipitisha bilioni 7, mwaka huu tunapitisha bilioni 12, leo nitashangaa sana mtu atakapokwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja akaambiwa bendeji hakuna, akaambiwa plasta hakuna, sijui kuna *reagent* gani hakuna nenda Kilimani kapime mkojo. Leo Mnazi Mmoja wanashindwa kupima mkojo mtu aende Kilimani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Spika, akurejeshe tena kwenda nafasi yako ukalisimamie suala hili. Leo nilisema hapa hata ukiangalia michango ya bima ya afya katika hospitali inayopata pesa chache sana ndio hospitali ya rufaa. Na ile kama nilivyosema sio hospitali ya biashara lakini ukishakwenda na kadi ya bima ya afya pale inakuwa sio biashara ile ni huduma. Ukiangalia hospitali yetu ina vifaa vingi vipya lakini vibovu kwa sababu hakuna fedha za kufanya *rehabilitation*.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ninachokiomba Wizara ya Afya katika eneo Kamati yetu italitupilia jicho la karibu kwa sababu Rais kwa kweli anajaribu kuboresha kila pahala. Leo tumekwenda hospitali ya Mkoani kuna matatizo tayari anataka kujenga nyumba za madaktari. Tumekwenda maeneo mbali mbali tumelalamika kuhusu suala la madawa, tayari Rais amewauliza wenyewe Bodi ya Madawa ili wananchi wapate dawa na huduma nyengine za afya, kiasi gani mnataka, walisema bilioni 9, akawambia nakupeni bilioni 12, tena wapate nini. Kwa kweli itakuwa ni aibu sana kwa wananchi wetu kukosa huduma ya afya baada ya kupitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, jengine hili najua limo kwenye Kamati yangu na sijajua Mhe. Spika, kama ataendelea kunibakisha kwenye Kamati hii hii. Lakini katika kitu ambacho siridhiki nacho suala la visima vya Ras al Khaimah mpaka leo kwamba bado tunazungumzia kama historia. Kama tungelikuwa tunajua hasa tungeliacha mambo yote tukashughulikia maji yote. Kwa sababu tunapokwenda kwenye uchaguzi na bahati nzuri na wewe Mwenyekiti ni Mwakilishi katika bakora moja tunayopigwa na wananchi wetu ni suala la maji. Leo tuna miradi mipya chungu nzima ya maji. Maana yake mwisho hatutoviita tena visima, maana kisima inabidi kinatoa maji, mashimo ya Ras al Khaimah yapo 150, yale yamefanywa *study* kama visima vile vitaungwa vyote hakutokuwa na tatizo la maji tutakuwa tunazungumzia mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, najua safari hii serikali mmetenga karibu bilioni 4, lakini bilioni 4 zile zitakwenda kwa taasisi nzima. Mimi naomba bado serikali tuweke nguvu katika suala la kuvimaliza visima. Hebu tuweke *target* mpaka ikifika mwaka 2019 mwishoni tuseme basi vile visima tuwe tumeshavimaliza. Hili namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango lakini vile vile na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kuweka mpango kazi wa kuhakikisha mpaka ikifika mwaka 2019 mwishoni visima vya Ras al Khaimah vyote viwe vimeshamaliza.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie haraka haraka zile dakika zako ulizonipa, nakuja katika hoja ambayo aliyoizungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub na mimi vile vile naiunga mkono iko katika ukurasa …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma dakika zako zimekwisha unasema nimekupa, sijakupa bado, sasa hivi ndio nakupa dakika tano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante Mwenyekiti, mimi Mwenyekiti ndio ninavyokupenda kama hivyo kwa sababu unajua Mhe. Mwenyekiti. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii bajeti haipitishwi kwa vifungu, hii tunaulizwa je, ndioooo! Sasa nitakuja kuona haya na aibu kubwa baada ya sifa zote nilizompa Waziri wa Fedha na Mipango halafu ikaja ikasikika sauti yangu inasema siooo! Kwa kweli nafikiri hata wananchi wangu watanihukumu.

Sasa Mhe. Waziri ametuomba katika hichi kitabu chake cha Mapendekezo ya Bajeti huu ukurasa wa 35 na katumia lugha nzuri tu. Serikali imekuwa ikitoa unafuu kwa ushuru wa forodha na kodi nyengine, uingizaji wa bidhaa muhimu za vyakula na mambo mengine, unga wa ngano. Hapa mwisho, kufuatia kuimarika kwa uzalishaji nchini kupitia Kiwanda cha Unga wa Ngano *(Zanzibar Milling Corporation)* na kufufuliwa Kiwanda cha Sukari Mahonda imejitokeza haja ya kupunguza unafuu unaotolewa kwa uingizwaji wa bidhaa hizo muhimu ili kuweza kulinda viwanda vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni ombi, sasa tunamuomba Mhe. Waziri na sisi tunamuomba ombi hili tunalikataa. Ukiondoa unafuu wa kodi hii ambayo wanalipishwa sasa hivi wanaoleta unga na sukari kwa ajili ya kulinda hivi viwanda, ina maana wale ukiwaongezea kodi ikirudi ile asilimia 25 au 20, ina maana na wao sasa wataongeza bei ya unga wanaoingiza nchini na wataongeza bei ya sukari kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kule majimbo yetu ya ng'ambu maskini ile boflo mtu ndio anatoka nayo anakwenda skuli, haina dagaa, haina chochote. Leo ukija ukiondoa unafuu huu boflo itapanda bei, wananchi wetu hapa tumeambiwa pato la mwaka katika pato la mwananchi karibu ni dola hata elfu moja haijafika, ni dola 907. Kuna wengine Mhe. Mwenyekiti, pato lake la mwaka hata dola 200 halifiki, ndio wale wanaokuja nyumbani asubuhi unatoka unamkuta anakwambia baba nigaie japo 500 nikapate boflo ya watoto. Ukiondoa unafuu huu boflo itapanda bei na kwa kweli itakuwa sio jambo zuri.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Zambia iliwahi kupanda shilingi 50 ya sembe, kulitokea sokomoko mpaka Rais Keneth Kaunda kaondoka kwenye madaraka. Sisi kwetu hatuko hivyo kwa sababu kuna Wawakilishi makini wanamsikiliza Waziri na wao wanamshauri Waziri. Hili naomba ili bajeti yetu tuiitikie kwa nguvu zote na hili naomba utukubalie. Hili nilisema nalo niliseme ili iwe na sisi tuweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo. Hapa Mhe. Waziri ametaja katika yale mambo ya kuboresha huduma za wananchi ameweza kutuboreshea mtaro wetu wa Darajabovu uliopitia Mboriborini mpaka Saateni. Tunakushukuru sana Mheshimiwa na umaskini umepungua. Lakini nina jambo moja kuhusu suala la ziwa la Mwanakwerekwe, hili naona vile vile mnataka kufanya utaratibu wa kuyaondoa maji kuyapeleka baharini. Lakini kuna wataalamu wa mazingira tuliwahi kukaa nao kuna kipindi wakasema lile ziwa la Mwanakwerekwe serikali bora ilijengee mikingo ili yale maji yasi-*flow* kwenda mitaani. Kwa sababu wanasema yale maji yanayotuama pale yanasaidia kuhifadhi umajimaji na unyevunyevu ambao unasaidia katika visima vyetu ambavyo vingi vimeshavamiwa na makaazi ya watu visikauke.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba katika huo mpango ambao mtakaoufanya bila ya shaka *feasibility study* mtafanya muangalie yale maji kuweza kuya-*retain* ili unyevunyevu uendelee kubaki na yale maji yatakayozidi yawe yana-*flow* kuujengea mtaro kwenda kuupeleka huko. Lakini ikiwa yale maji yataondolewa moja kwa moja na pale patakuwa pakavu kwa kweli tunaweza tukajikuta hii dhiki ya maji na tabu ya maji ikaja ikaendelea.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini vile vile nakushukuru kwa kunigaia dakika zako na naamini nimezitendea haki. Baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja baada ya Mhe. Waziri kukubali lile ombi langu moja tu kidogo la kusema kwamba yale aliyoyapendekeza kwanza ayaache ili wananchi wetu waendelee kupata huduma kwa unafuu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Sasa nilimwita Mhe. Suleiman Sarahan Said lakini kwa vile muda hauruhusu Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil aliniomba dakika tano nahisi tunaweza tukamalizia. Kwa hiyo, naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa sasa Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na nalishukuru Baraza lako kwa kupitia uongozi wako na mimi kuniona kuweza kuchangia bajeti hii.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama hapa na mimi kutoa mchango wangu. Kwanza mimi naiita bajeti hii ni bajeti nafuu, bajeti mkombozi na bajeti yenye kumjali mwananchi, lakini hiyo ni *slogan* ya bajeti hii. Kitendo cha bejeti hii serikali kutokupandisha kodi hata senti moja katika utoaji wa huduma hichi kinaonesha hii ni bajeti nafuu na ni bajeti yenye kumjali mtu mnyonge na mtu wa chini kabisa.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi au wananchi wetu Mhe. Waziri walikuwa wana wasi wasi labda bajeti hii itakapokuja itakuja na mabadiliko ya kodi na mabadiliko ya ukuaji wa vifaa na huduma mbali mbali. Naipongeza serikali kwa kuwa bajeti ya mwaka huu inakusanya 807 bilion ya makusanyo, wakati matumizi ni trilion 1.3. Hii inaonesha kwamba ni *balance of payment* kwamba tukijikaza kidogo kidogo tu tunaweza tukafanya bajeti yetu ikawa ni bajeti yetu wenyewe pasi na kutegemea wafadhili. Hizi ni juhudi za Mhe. Rais kupitia wewe kukuamini Mhe. Waziri kwa kusimamia sekta hii kwa mafanikio makubwa. Serikali ndogo kama hii leo tunaingia katika historia katika ukanda ya Afrika Mashariki kwa kuwa na bejeti yenye kukusanya vizuri. Ndio maana hata wawekezaji sasa wameanza kutuunga mkono na wafadhili wa maendeleo uliowataja wameanza kutuunga mkono, kwa sababu sisi wenyewe tunajitosa katika kukusanya kodi. Kwa hivyo hongera sana bajeti hii mimi tena naiita ni bajeti nafuu na ni bajeti mkombozi.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa maendeleo nimeona Mheshimiwa vipaumbele vyako vyote ni vyenye kuondoa kero za wananchi wetu. Wananchi wetu mbali ya maendeleo ya kawaida na utulivu uliyokuwepo Mhe. Mwenyekiti, lakini wanahitaji kuona mabadiliko na maendeleo ni mabadiliko ya hatua ya kutoka tulipo na tunakokwenda. Kitendo cha Mhe. Rais kupeleka umeme katika visiwa viwili vya Pemba Fundo na Kisiwapanza, hili ni jambo la kupongezwa mno. Sidhani kama lilikuwemo katika bajeti ya serikali, lakini kwa umahiri wake na kwa kukuamini Mhe. Waziri tumeweza kutia umeme kwenye visiwa viwili pasi na kutegemea pengine katika *original budget.* Hilo ni hongera sana, serikali yenye kujali wananchi wake kuwaondolea matatizo, hongereni sana. Naiita tena hii bado ni bajet nafuu, bajeti mkombozi na ni bajeti yenye kujali wanyonge.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kero ambazo zinasemwa sana au zinaumiza sana nilikusikia kwenye hotuba yako kwamba kero ya maji kwenye barabara ya Kiembesamaki imeshapatiwa ufumbuzi na *sign construct* tayari imesainiwa. Kwa hivyo tunategemea *within four months* au *quater* ya mwanzo baada ya bajeti hii kupita najua tayari limetoka tunategemea kwamba kero ile itaondoka kusudi pahala pale wanapita wageni na wananchi mbali mbali kuwa ni kero. Hilo nakushukuru sana na bajeti hii bado naiita bajeti nafuu.

Kero nyengine nimeona kwenye bajeti yako hii kubwa kwamba suala la maji la Mwanakwerekwe na Kibondemzungu nalo litakuwa historia. Tunaomba sana suala hili mwakani tulizungumze kwa nia kwamba serikali imemaliza suala lile na pia nalo limekuwa historia. Nia ya kufanya hivyo tunayo, uwezo tunao, mipango tunayo, Tume ya Mipango yako inayo na timu yako nzima inayo. Nakuomba sana suala hili Inshallah tukijaaliwa mwakani linazungumzwa *done! done!* watu wote wanajua kwamba kero hizo zimeondoka.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mwisho katika kutumia dakika tano zangu napenda kuipongeza Wizara hii ya Fedha ya bajeti hii kwa kuona umuhimu wa kukuza siku za urejeshaji wa *return*, hii ilikuwa kero Mhe. Waziri, watu walikuwa wakitetemeka, wafanyabiashara walikuwa wanakitetemeka, wakifanya *consideration* ya siku, kuna *holidays* na pengine watu wanataka wapumzike kwenye nchi yao ya amani lakini sasa ume-*extend 20 days or every ending month.* Kwa hivyo hii nakupongeza na wafanyabiashara wamelipokea vizuri zaidi. Hongeza sana Mhe. Waziri.(*Makofi*)

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, bado nitaendelea kidogo kumalizia katika kuikubali bajeti hii kwamba bado nafasi ipo kubwa, mara nyingi huwa unazungumza kama bado tuna fursa zaidi ya kuweza kuchagia bajeti hii kwa ukubwa zaidi. Sijaona hasa msukumo mzuri na mkubwa kimkakati, mashirika ya umma kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Mashirika haya yanafanya *production* kubwa, yanazalisha na yanakusanya, hapa angalia sana pato hili litazidi, weka mkazo.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa awamu hii ilivyoingia mimi sijaingia Barazani lakini Waziri wa Fedha aliyepita alianzisha mfuko maalum wa mashirika yaweze kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali, kaza kamba hapa ili tuweze kuutunisha mfuko huu iwe bajeti yetu ilingane na matumizi yetu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimetumia dakika zangu na ninakushukuru sana, hii ni bajeti nafuu naiita, wananchi wetu wanaisherehekea na wanaiunga mkono tunahitaji utekelezaji. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha kikao hichi naomba niwataje wachangiaji wetu wa mwanzo jioni hii ya leo. Wakwanza atakuwa Mhe. Suleiman Sarahan Said, atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abei na Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali.

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wachangiaji wote waliochangia na pia niwashukuru kwa utulivu wenu. Sasa naomba niakhirishe kikao hichi mpaka saa 11:00 za jioni ya leo, nawashukuru sana.

(Saa 7:00 za mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 za jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said, atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein katika jitihada zake za kuiletea maendeleo Zanzibar na wananchi wake pia akiwa na mshauri wake mkuu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi katika jitihada zao za kuendelea na kuyaona maendeleo yenyewe ambayo tunakwenda nayo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nisifie tena kwa Mhe. Waziri kutokana na ufafanuzi mzuri wa vitabu vyake ambavyo vimeeleza hali halisi tulipo, tulikotoka na tunakoelekea kwa hivyo nimsifie sana pamoja na watendaji wake waliyovitengeneza vitabu hivi, kwa uweledi kabisa unafahamu nini ambacho serikali inaendelea katika muda ambao tunakwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na kuchangia kwangu katika suala la upande wa ajira nizungumzie tu kwamba pamoja na ukuaji au kuongezeka kwa uchumi lakini bado tatizo la ajira halijakuwa la ufumbuzi katika nchi yetu, tumeona tumepiga hatua nchi yetu inaleta maendeleo tumeona tumepiga hatua tumekuwa kiuchumi lakini bado suala lile lile la ajira bado linaleta utata. Tatizo la zaidi tunalisemea sana tatizo letu la ajira lakini ajira zinapatikana, lakini tumekuwa hatuna mfumo madhubuti wa kuweza kuzilinda ajira zetu zilizomo ndani. Kwa kweli, sisi tuna nafasi nyingi tu tunazoziona kwamba zinapatikana lakini bado ajira zetu tunazitoa kwa watu ambao ni wageni tunawaacha wananchi wetu wakihangaika.

Kwa mfano, tunao walimu wanatoka vyuo vikuu tunasema hatuna walimu wa sayansi si kweli bado walimu wa sayansi tunao, ukenda huko vyuoni unaenda kuambiwa huyu kamaliza hii huyu kamaliza huku au wanatudanganya wale, lakini huku tunatafuta walimu kutoka nchi nyengine. Vile vile, tukisema watu wa mahotelini watu wa hoteli nini tunakwenda kuchukua watu kutoka wengine wakwetu ajira hawapati. Kwa hiyo, lazima tuweke mfumo maalum wananchi wetu kuwaekea mfumo maalum na hata hawa wawekezaji, hawa wawekezaji sio kila mmoja aje na mdomo wake wakwamba kisha kuwa muwekezaji yeye ndio mwenye amri ya kuajiri hiyo lisiwepo, hapa mlikuja kwetu na lazima afuate mfumo wetu na lazima watu wetu waajiriwe kwa njia yoyote (*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hili nilikuwa nasema niliseme ili tuweke mfumo madhubuti bado hatujachelewa, lakini bado uchumi wetu unakuwa lakini bado ajira hatuna kwa vijana wetu, kwa hivyo ilo nilikuwa niliweke hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nilizungumzie suala jengine ambalo limenishtua kwenye kitabu hiki suala la biashara yetu na Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, kama kitabu cha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kinavyozungumza kinatilisha huruma, utakuta sisi mapato yetu yanaongezeka katika kutoa vitu Bara kuleta Zanzibar, lakini sio sisi kutoa Zanzibar kupeleka Bara, tunaweza kuambiwa hapa kwamba sasa hivi tumeshuka tulikuwa na shilingi bilioni 84, lakini leo utakuta mtu anakwambia tuko karibu asilimia 60 ya uletaji wa kutoka nje kuliko sisi kutoa ndani kupeleka nje.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hapajabadilika mfumo wowote, hapajakuwa na matatizo yoyote nini ambacho kinatufanya biashara zetu za kwenda Bara zirudi nyuma kwa hivyo ningemuomba Waziri hili ni pato kubwa lakini limerudi nyuma nchi mmoja. Sasa sijui hapa tuna tatizo gani wafanyabiashara wasikilizwe ili hali hii iweze kutatuka, ili tuweze kuendelea na biashara zetu.

Sisi kama unavyotujua Mhe. Mwenyekiti ni kisiwa tuna nafasi ya mbele na nyuma na ubavu na wapi na hatwende pahali pengine popote sasa ni lazima kama pahala tuweze kuangaliwa kwamba hawa mwisho wao ni hapa hilo lazima nilizungumze. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama mengine tunavyolizungumza utaratibu wa ardhi. Hivi sasa tumekuwa na mfumo wa kupima ardhi ya Zanzibar, lakini hatuna mfumo wa utumiaji bora wa ardhi ya Zanzibar, kila mmoja anakata pande lake anajenga mwisho tutakuwa hata pakuchimba mgomba hatuna, mfumo uliokuwepo wa marehemu Mhe. Abeid Amani Karume Rais wa kwanza wa Zanzibar alikuwa na mfumo wa kujenga ghorofa tusende mbali leo Zanzibar nzima inajengwa kila unapopita, pori linaondoka mvua hatupati miundombinu yote inaharabika kutokana na tabia za nchi hatuna utaratibu wa kuitumia vizuri ardhi na wala ardhi yetu haikuwi wanaokuwa ni watu. Kwa hivyo, ni vyema sisi tukaweza kuilinda ardhi yetu muda kwa sababu ardhi inapoijenga inapoteza kila aina ya thamani kilichopo ikiwemo mbolea na mambo mengi yote.

Kutokana na hali hiyo, ni lazima ardhi ibanwe palipojengwa pashajengwa palipozuiliwa pazuiliwena nyumba zijengwe nyumba za ghorofa, ili ardhi itosheleze na kilimo tupate humo humo, sasa kama tutaendeleza kuitumia vibaya ardhi yetu tutakwenda kubaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie na pato la mwananchi mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, bado pato la mwananchi ni dogo sana Wazanzibari ni wachache, Wazanzibar ni masikini sana lakini bado tatizo la utapia mlo lipo. Kwa kweli, bado mpaka leo unalizungumzia suala la Zanzibar kilo ya nyama shilingi 10,000/- imepanda yaani kila baada ya muda inapanda hairudi chini zaidi ya kwenda juu ikifika siku za Sikukuu kilo moja ya nyama shilingi 15,000/-.

Kwa hivyo, lazima tukubaliane tutaongeza bajeti ya afya mpaka tutafika shilingi bilioni 20, lakini kama watu hawana lishe ubovu utaongezeka kila siku, tunaweza tukaishusha bajeti watu wote wakiwa wazima, zamani bajeti ya afya ilikuwa shilingi 300,000/- au 500,000/- kwa sababu watu walikuwa wazima walikuwa hawaumwi ovyo, leo kwenye nyumba kila unayempima hakuna hata mmoja ambaye ni mzima wote wabovu kwa sababu hamna lishe, leo nyama mnawania mfupa mmoja ile mbavu mmoja unawania nyama na mtu ale nyama ashibe aweze kufanya kazi nyengine. Leo nyama kilo shilingi 10,000, utumbo sijui unauzwa kiasi gani kwa kilo moja, atakula nini, lazima tukubaliane na mfumo mzima wa mazao na mfumo wa lishe wananchi wa Zanzibar wawe na nguvu za kuweza kufanya kazi.

Leo kila mtu mmoja ata yule kijana mdogo mdogo hawezi kufanya kazi, vyakula tulivyonavyo havitoshelezi na sisi sasa hatuna ukulima, sisi vyakula vyetu ni vya kuagiza na bei ndio zinapanda kila siku mchele wenyewe mashaka.

Mhe. Mwenyekiti, juzi niliona *clip* moja ilikuwa imerushwa na nina uhakika si ya peke yangu na jamaa alikubali ni dokta mmoja anasema mimi niko tayari niitwe niko tayari nioneshe watu wamefanya jaa la sadaka Zanzibar, watu mwenye tende mbovu ndio wanaileta Zanzibar watu waje wale, watu wenye mchele mbovu ndio wanawapelekea watu waje wale kwamba sisi ndio walaji. *(Makofi)*

Lakini ile athari yake Wizara ya Afya ndio itakayoona na sisi wenyewe ndio tutakaona maradhi yale baadae. Zanzibar tulikuwa tunaweza kukaa miaka kumi tunayasikiliza maradhi ya kutoka nje, hivi sasa Zanzibar inatumbuka maradhi kila siku hata uko nje hayako tena kutokana na matatizo mengi yalotupata, juzi jamaa anaonesha mchele akiushika hivi unapukutika wote anasema mimi niko tayari ukiuliza hapa unaambiwa bwana katika kwetu tuna *Zanzibar Bureau of Standard* ile tunaita ya ukaguzi tunafanya kazi vizuri bandarini mchele huu unapita wapi

mpaka unakuja kuuzwa mchele mbovu au unakuja kutolewa sadaka mchele mbovu au zinauzwa tende mbovu hatuna lazima hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lazima serikali isimame kidedea ili kuwatetea wananchi wake kutokana na vyakula vinavyoletwa sisi tusitizame mfumo wa kulipa kodi lakini kodi zetu zitakuwa zinapotea mbele ya maradhi baada ya kuwa wananchi wetu wote ni wabovu.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na hilo nilizungumzie lakini nikizungumzia suala la chakula nizungumze bado serikali ina jukumu la kuhakikisha wananchi wake wanapunguziwa maisha kila siku. Mhe. Mwenyekiti, hili pato ndio linalomfanya mwananchi wenzangu wamelizungumza sana suala la maji suala la elimu bado Mhe. Mwenyekiti mtu wa chini ana tatizo sana la mtoto wake kupata elimu pamoja na serikali inajitahada zake zote, lakini bado suala la elimu bado elimu ni kununua kwenye shule za binafsi suala ndio angalau linaonekana kwenye elimu nzuri sasa hakuna mtu mwenye roho ambayo tofauti sote tuna roho moja na yule mwanae akifika kwenye *degree* lazima anataka aende aje amuokoe tatizo linafika hapo kwenye tatizo hilo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana serikali ikalitizama kwa jicho la huruma sana wananchi wake wakatafuta kila aina ya mbinu, leo samaki akinunuliwa bei yake humnunui, mnyama akichinjwa nyama huinunui, mchele ukiletwa bei kubwa lazima kitu hichi kifanyike kwa utaratibu wa wananchi wetu vitu vishuke bei.

Kuondoa matatizo ya afya Mhe. Mwenyekiti namsifu sana Mhe. Waziri kaongeza ana shilingi bilioni 12 za kuleta madawa, lakini yatakuwa hayatoshi watu wote ni wabovu. Kwa hivyo, kwanza alishe watu, watu wawe *strong* watapunguza dawa watakuwa hawali dawa tena watu wanakula nyama, wanakula kila kitu. Kwa hivyo hapa lazima tuweze kuangalia kila kitu ambacho kinaendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie utaratibu duniani nchi zinajipanga na nchi yetu sisi wananchi wake wanaisikiliza serikali zaidi kuliko chochote, ukiambiwa TV hii ya serikali inasema ukweli wataisikiliza.

Sasa tatizo tulilonalo sisi tunaenda kwa mazoea mpaka sasa hivi mtu anaoa wake wanne, mpaka sasa hivi mtu anafanya mengine anayotaka mwenyewe lakini ukilichukulia suala zima bado hatujaweka *limit* ya watoto tunafanya kama kuku unaangua mayai uliyonayo nayo tu, wewe ni binaadamu unatakiwa upange hii hali itakuwa ngumu mtu mmoja masikini anawake wanne ana watoto 40 huyo hata umfanye nini haji juu wale watoto watakuwa sio na yeye mwenyewe siye wale mama wote ukiwaona kama wamezikwa wamezikuliwa, lazima na serikali ianze kufanya utaratibu angalau watoto saba, watano iwe basi. Kwa mfano, kwetu sisi Pemba mtu aliyekuwa hakupata uzazi watoto kumi na tano unaambiwa huyu hakupata uzazi ana kumi na tano (*makofi*).

Sasa matatizo haya lazima tuyaangalie, serikali lazima itizame huku tunakokwenda mtu anaolewa akiachwa tu anahisabu watoto tu halafu wote wale anakuja kuleta mzigo kwenye serikali hata dini zimesema humu lazima na dini katika upande wa mufti ichukue mkondo wake. Kwa mfano, mama anazaa leo hatimizi hata miezi tisa anazaa mwengine yule mama anatakiwa yule mtoto ambaye amemkatiza maziwa yake alipe ni nani anayemlipa humu, mama mmoja ana

watoto huwezi kuwahesabu mmoja mwaka mmoja na nusu, mmoja mwaka wa pili, mmoja mwaka wa pili na nusu miaka mitatu watoto wanne. Sasa lazima vitu hizi vifanyike na utaratibu uzungumzwe. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala jengine la ujenzi wa barabara wenzangu wengine kama walivyozungumza. Kwa kweli, barabara inatuchukulia pesa nyingi sana na barabara hazichukui muda kuharibika lakini pia barabara hizi wajenzi wake ni wa kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nia na madhumuni ya kutengenezwa kwa UUB ambayo hii ni kitengo maalum hichi cha miundombinu cha barabara, wataalamu wapo hawana vifaa hawa wanatuokoa wakati wa kampeni ndio unaposema njia hii isafishwe lakini wakati wa kampeni hatumwiti mkandarasi tunamwita huyu. Sasa sisi tunachokifanya hivi sasa Mhe. Mwenyekiti ifanywe bajeti ya kwenda kununuliwa vifaa vya kuweza kutengeneza barabara zetu ndani.

Kwa kweli, uchumi unapotea kwa sababu sisi tumekaa kama pakacha tunatia maji yanatoka kwa sababu pesa tunazozikushana hazitusaidii sisi zinakwenda nje zote kutokana na mbinu tunayoitumia. Kwa hivyo, ni lazima UUB kama ni barabara ni pesa nyingi inapotea hii itengenezwe upya na iwe na wakandarasi wazuri pamoja na *engineers* wazuri, ili iweze kufanya kazi na vifaa vizuri barabara zetu hata kama zitakuwa zimetumika vibaya au zimekuwa mbovu tutazirekebisha vizuri sana. Mhe. Mwenyekiti hilo lilikuwa ni angalizo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu habari ya ubunifu wa vyanzo vyetu vya mapato. Mhe. Mwenyekiti, vyanzo vya mapato bado tunavyo vile vile vya asili na bado tumeongeza kidogo, lakini tunakokwenda tuachane na kuokota shilingi mbili mbili mwenye baskeli, mwenye susu la samaki. Kwa hivyo, tutafute mitaji mikubwa ili yule tumuongezee pato lake asilipe kodi zile ndogo ndogo ambazo hazina maana, wenzetu wanaondoa huko zile pato la ndani lile la kufunga funga mazao yale hayana maana mtu hawezi kulima shamba lake mbio ukamwambia atoe kodi mvua zote kalima mwenyewe halafu unamwambia bado una kodi.
Hivyo, ni vyema lazima tuondoke kule tutafute mitaji mikubwa iweze kutuingizia pesa, ili aweze na serikali yetu kuweza kufanya vitu vya maana na vikubwa zaidi na kutokuwa tegemezi wala kuomba msaada kwa mtu yoyote. Kwa hivyo ni lazima nafasi tunayo sana.

Mhe. Mwenyekiti, haiwi maeneo mengine ya majangwa ya Sahara uko ni majangwa wenzetu wanayatengeneza yanakuwa kivutio, lakini mengine yanatengenezwa wanaweka viwanda haiwi sisi tuna bahari, sisi tuna kila kitu ardhi yetu nzuri tunashindwaje. Kwa hivyo, ningeomba sana serikali ikae chini tutafute mbinu mbadala wa kuweza kusaidia mambo ya vyanzo vya kodi ambavyo vitatusaidia sana.

Lakini chengine ni mpango wa viwanda, viwanda hivi tunavyosema tunavyo ndani hatujavilinda sasa ninavyoona sisi tuna mpango sana wa kufanya viwanda. Kwa hivyo, tuanze kujipanga hivyo vilivyopo kwanza tuvi *control*, sukari iliyoko Mahonda inatutosha kama inatutosha ya nje isiingie ile tuweze kunywa kwa sababu ni nzuri tumeipanga, tutumie sukari yetu lakini sasa unamwambia ushindani uko wa *free* ukimpa ushindani kiwanda kinakufa kikifa na yule wa kule hatuletee unaambia Brazil sukari hakuna tunakunywa maji matupu. Sasa huyu tumlinde miwa tunayo, maeneo tunayo tufanye kazi zetu, kwa hivyo niangalie masuala ambayo ya viwanda tuanze kuvilinda. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie habari ya bandari. Mhe. Mwenyekiti, tunaizungumzia bandari kubwa ya Mpigaduri lakini pia tuna bandari yetu ile pale ya Malindi. Lakini hapa kati kati baada ya kulitoa eneo letu lile la hoteli ya Bwawani tukampa muwekezaji pale tulikuwa ndio tume – *serve* sasa hivi kuweka *container*, hivi sasa huyu muwekezaji nafikiri ameshindwa ataturejeshea wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa tahadhari tu kwamba *containers* yalikuwa hatuna pa kuyaweka, *containers* ilikuwa safari ni ndefu yakwenda kuyatafutia ni gharama kubwa sana tungetumia lile eneo la Malindi kama muwekezaji ataturudishia pale bado kwanza pazuwiwe na bandari pawe sehemu ya kuwekea *containers* mpaka tutakapopata bandari yetu huru ambayo ina nafasi ya kutosha tutayatoa katika maendeleo mengine. Lakini gharama kubwa itapotea pale.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, bado pamoja na makusanyo ulio nayo pamoja na mambo bado miaya ya kuvuja pesa ya kuvuja mapato unayo. Kwa hivyo, bado kuna mambo mengi ya kuweza kujipanga mipango ya kupotea pesa kiholela holela za serikali izibwe iweze kutumika kwa wanahusika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la maji bado linakuwa kama ni mzigo sana kwa serikali, maji bado linakuwa tatizo kwa wananchi, mwananchi yeyote asubuhi hawezi kwenda kazini kama hajapata maji, lakini suala la maji bado halijatatuka wenzangu walisema tungewacha kazi zote tukatafuta maji ya uhakika ya kuweza kuangalia, lakini hatuna haja ya kutafuta yote lakini suala la maji lazima liangaliwe kabisa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti…….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe zimebakia dakika nne.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, bado dakika nne, *ok* ahsante. Mhe. Mwenyekiti, suala la utalii nimeona tumeongezeka utalii kutoka shilingi 300,000 mpaka shilingi 400,000/-, lakini bado utalii kwetu ni ule ule wa eneo liliopo na mara nyingi limevunjika zaidi na jengine limeshapotea yaani bado utalii hatujaufanyia kazi ukatuletea tija, kwa kweli utalii hatujaufanyia miundombinu mizuri, leo unakwenda kwenye maeneo ya utalii hata kikombe cha kahawa hakuna unakwenda kwenye maeneo ya utalii hata mkahawa hakuna na maeneo yale wanakwenda watu wanapumzika.

Kwa hiyo, kwa nini tusijenge maeneo ambayo baada ya kupata utalii, leo unasema una msitu wa Ngezi hapana hata banda la hoteli hapana chochote, mtu anakwenda mle achukue mihogo yake na kila kitu eti anakwenda kutalii. Lazima maeneo yale yapambwe watu wavutike ili watu wawe na mitaji pamoja na sekta ya ajira ipatikane, lakini sisi maeneo yetu tumekaa kama magofu, kuna kule kuna msikiti Chooko haujulikani ukitaka kwenda kutizama mpaka umtafute mtu wiki nzima aje akueleze kitu gani.

Kuna huko kwa Mkamandume, hakujulikani Kaburi la Mwanamwari hakujulikani, vitu vipo vingi vya kuweza kutusadia sisi tukapata mapato na wananchi wakajua kwamba eneo leo lile lingewasaidia lakini bado serikali haijatilia nguvu kwenye maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la elimu, kwa kweli elimu ina haja kubwa sana sasa hivi ya kuitumia tulivyo, tuwatumieni wasomi wetu tutumie katika mbinu mbadala ambazo za kutumika, sio kwamba elimu iliyotumika ni ajira kwa serikali ndio iliyotumika skuli, ndio iliyotumika kwenye maeneo yote mtoto yoyote ajira yake apangiwe ajira ya serikali, hatuna ajira mtoto anamaliza Chuo Kikuu hafundishwi kutafuta ajira anafundishwa asubiri kazi za serikali. Kwa hivyo, ile elimu yake hajui hata amekuja kuifanyia nini mtu amesoma mifugo, mtu amesoma kila kitu asubiri serikali, serikali hiyo itakuwa inawaajiri wangapi lazima tufundishwe na ujasiriamali ambao una pesa zaidi kuliko haya serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la udhalilishaji. Sisi tuna *deal* na vitu vidogo vidogo sana serikali inachukuwa juhudi kubwa kwa udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti, dawa ndogo ya watu wanaodhalilisha wanatia hasara serikali wanawaharibu watoto kazi ndogo wewe unamjua asilimia mia huyu amemharibu mtoto mpige sindano asifae tena basi kazi imekwisha unamwachia tena mambo yake yamrudie na mwengine yule ni kuhasiliwa kisha kazi yake kazi ikamatiliza sasa tunasubiri tukamfunge huko jela anakwenda kufanya mengine zaidi na ndio mnampa nafasi zaidi haya.

Kutokana na hali hiyo, akifanya apigwe sindano basi kazi yetu imekwisha wako mbwa hatutaki mbegu tena tunatoa mbegu basi kazi imekwisha sasa mtu tunamuachia aje afanye tena arudi aje afanye tena huyu hakubaki ashakula nyama ya mtu huyu Mhe. Mwenyekiti harudi tena lazima nyama ya mtu atairudia ameshaionja. Kwa hiyo, lazima hapa tuangalie adhabu nyengine lazima zitolewe kwa ukali kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nalizungumzia suala jengine la mafuta, kwa kweli tushajipanga sana kuzungumzia suala la mafuta tuwaulize wenzetu tusijipange na fahari kubwa na kuwa wapi tutashimba mafuta na tukawapa tamaa wananchi wetu nini mafuta. Mafuta yanaweza kutuletea balaa, mafuta yaweza yakatukoroga ni kitu ambacho kwanza ni cha rehema ya Mwenyezi Mungu ni kama maji unaweza ukachimba kisimani usipate na ukapata, lakini hata hayo mambo yake sivyo tunavyo ya *publish* tunafanya kama yakija mafuta hata mtu asifanye kazi tena atalipwa tu ndani atafanya kitu gani hii ni *by the way*. Kwa maana hiyo, lazima atutizame mfumo wetu wa kilimo, tutafute mfumo wetu unatuendelea mafuta tuyaache yatakapo kuja yakatufaa tutasaidiana na mafuta. Lakini sasa hivi kila mmoja huko mitaani anauliza mimi kwangu hakutoki mafuta kwetu kunatoka mafuta msomi anakuwa hivi tatizo la mafuta mheshimiwa tuliache kama lilivyo nchi za wenzetu zina mafuta, zina vita na hazikuwafaa kitu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote basi niunge mkono hoja asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa na Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: *Bissimillah Rahman Rahim* Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu aliyetujaalia tukakutana leo hapa tukaweza kuipitia bajeti hii ya serikali, bajeti ambayo ni nzuri na ina kila hali ya kuisifu.

Mhe. Mwenyekiti, waswahili wanasema kwamba "Mcheza kwao hutunzwa" akizidi huongezwa. Kwa upande wangu naongeza sifa natia chumvi katika bajeti hii nikilinganisha na bajeti tatu ambazo nimezishuhudia wakati tulipoanza kuingia katika Baraza hili, labda kidogo kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti tuangalie nyuma bajeti ya 2016/2017 ya 2017/2018 na hii ya 2018/2019. Tulitoka katika shilingi bilioni mia nane na kitu 2016/2017 tukaja *trillion* 1.08 2017/2018 na leo tumefikia *trillion* 1.315 bajeti ambayo yakutekelezeka si bajeti ya kuhadisia ni bajeti ambayo inatekelezeka na tunasema inatekelezeka kwa sababu gani. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia makusanyo ambayo tuliyakuta sisi kwa kipindi kile ya ndani yalikuwa bilioni 399.0, sasa leo tunazungumzia bilioni 677.6 tukiitoa bilioni 399 tunapata zaidi ya shilingi bilioni 278.6 za makusanyo ya ndani. *(Makofi)*

Hatuna budi kuipongeza sana serikali yetu, shukrani na pongezi za pekee zimuendee Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein akisaidiwa na Waziri wake wa Fedha na Mipango, watendaji wote wa serikali pamoja na mawaziri wengine kwa kusimamia vizuri Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu hapa tulipofikia tumefikia kwa sababu ya muongozo wa ilani ya chama chetu, utekelezaji wa chama chetu. Chama chetu ndio kilichotowa sera hizi za kutoka katika uchumi tegemezi na tukaja katika uchumi wa kati. Tulitegemea kwamba itakapofika mwaka 2020 lakini kiwango cha makusanyo tuna imani kile ambacho kimeelezwa kwenye lengo kabla ya mwaka 2020 kitafikikiwa kwa kasi tunayokwenda nayo na nasema hivi kwa sababu gani, kwa sababu kutoka Aprili 2016 tulipoingia sisi hapa katika Baraza hadi leo Aprili 2018 ni miezi ishirini na nne. *(Makofi)*

Miezi ishirini na nne hii kama tutaigawa kwa siku tutakuta makusanyo ya ndani ambayo yameongezeka yana kusanywa kwa siku ni wastani karibu shilingi milioni mia tisa na zaid kwa siku hongereni sana watu wa *ZRB*, Wizara ya Fedha, pamoja na serikali yote kwa ujumla kwa kazi nzuri munayoifanya na sisi tunawaahidi kama tuko pamoja na nyinyi tuwaombee Mwenyezi Mungu awape nguvu muweze kutekeleza majukumu yenu yalioko mbele. *(Makofi)*

Vile vile, tukiangalia kama tunakusanya ni jambo moja kwa sababu kukusanya ni jambo moja na kuweze kutumia pia jambo jengine. Kwa mfano, tukiangalia katika *page* ya 14 ya kitabu hiki utakuta jinsi gani ya matumizi ambayo yapo wenzetu wamesema kwamba walikuwa na lengo la kutumia shilingi 695.0 bilioni, lakini wametumia shilingi 461 bilioni kwa kazi za kawaida ambapo kuna tofauti karibu milioni 200 angalia jinsi ya *balance* ya matumzi walivyo yaweza kuya-*control* hii ni dalili ya wazi kwamba wenzetu wanataka kutupeleka pale tulipo pakusudia.

Kwa hivyo, nawaomba sana kwamba bidii hii ambayo wameianza na kasi hii ambayo wanaiendeleza au wanaifanya, ili Mwenyezi Mungu akipenda ikifika hiyo 2020 tuwe tumemaliza, tumepindukia lile lengo ambalo tumelikusudia. Lengo ambalo tukilifikia basi ni dhahiri kwamba tunaweza tukafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuweza kukusanya karibu shilingi bilioni 900 kwa mwezi na kidogo na ukigawa kwa hilo ongezeko ambalo nimelisema, ni kazi kubwa sana si kazi ya mchezo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na timu yake pamoja na kazi nzuri inayofanywa na watendaji wake, lakini bado iko haja ya kupanua wigo wa makusanyo ya kodi, kwa sababu inaonekana kwamba bado wapo watu hawajakuwa tayari katika kazi hii ya kuunga mkono azma ya serikali ya kuweza kufanya bajeti ambayo inajitegemea sisi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2016 wakati tunaingia sisi bajeti yetu ilikuwa ni tegemezi karibu kwa asilimia 40, sasa leo tujiangalieni katika bajeti yetu sisi ni *trillion* 1.3 makusanyo yetu ya ndani ambayo tunayategemea kuyakusanya Mwenyezi Mungu akipenda bilioni 677.6 angalia ni kwa kiasi gani tutakuwa tumeweza kujitegemea sisi wenyewe. Lakini isitoshe ni kwamba hata tunapolizungumzia lile deni kukua kwa deni la taifa limekuwa kwa sababu ambazo wenzetu wamezieleza katika kitabu chao.

Kutokana na hali hiyo, nawaomba sana watendaji kwamba wasibweteke na matokeo mazuri ambayo tumeyapata kwa miaka hii tuongezeni kasi na maendeleo ya kweli yatapatikana kama pale aliposema Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipotwambia kwamba ili tupate maendeleo katika kazi vitu vitatu ni muhimu kwanza nidhamu, pili uwajibikaji ikisha kuipenda kazi yenyewe ambayo unaifanya ukiamini kama ndio kazi yako ambayo inakupatia riziki.

Mhe. Mwenyekiti, tutakapokuwa na dhamira ya hiyo ya dhati basi ni wazi kwamba kasi tuliyoanza nayo ambayo tunakwenda nayo tutaifikia bila ya matatizo huo ni upande mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini upande mwengine tutakuja yajadili hayo tutakapo yakuta huko mbele kuna Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo vitabu tumepewa na tumeanza kuvitizama kwenye ripoti yake hii anasema kuna baadhi ya taasisi za serikali ambazo zimetajwa katika ripoti kwamba wamefanya ubadhirifu wa fedha za serikali, lakini taasisi zile zinapata hati zinazoridhisha. Sasa ikiwa mtendaji wa serikali au wizara imetajwa na imeanishwa kwamba idara hii au wizara hii imefuja fedha ya serikali ikisha inapatikana hati inayoridhisha hao wenye makosa ambao wanatajwa itakuwa vipi ikiwa aliyefanya vibaya anapata hati inayoridhisha, mwenye kufanya vibaya atapata hati gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali yangu kwamba watu hawa wanaofanya ubadhirifu kwa fedha za umma wasinyamaziwe kimya, ili tuweze kufikia lengo tunalolitaka hii tabia ya kuoneana aibu tuiondoweni tufute tabia ya kuoneana aibu ikiwa nimefanya makosa Omar niambiwe Omar umefanya kosa. Kwa kweli, Mwenyezi Mungu mwenyewe alisema kwamba napenda kidogo ninukuu anasema kwamba *"Mzinifu Mwanamke na Mzinifu Mwanamume miongoni mwao wapigeni bakora mia"* wala anasema Mwenyezi Mungu kwenye *Quraan Surat Nour wala isiwajieni nyinyi huruma katika kutekeleza amri hiyo* na adhabu yao wanasema ishuhudiwe na watu. Sasa na nyinyi munapowadhibu hawa watangazieni kwamba fulani kafanya ubadhirifu atangazwe mwengine ndipo atakapojua kwamba kufanya hivi ni makosa akahofia. Kwa kweli, wenzetu wanajitahidi kukusanya kiasi kama hiki wametufikisha hapa tulipo leo, sasa leo wanatokea wengine wanatumia vibaya fedha za serikali ikisha tukiwanyamazia hatufiki pahala.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein sana kwa kuanzisha kile Kitengo cha Tathmini, kitengo kile kifanye kazi yake za tathmini kwa kuzisimamia wizara za serikali ili iweze kubainika watu wanaofanya vibaya, sisi lengo letu ni kufanya vizuri ili nchi yetu iende vizuri, wananchi wetu waweze kufaidika kama ambayo mwenyewe Mhe. Rais wetu mpendwa wa Zanzibar anataka, asitokee miongoni mwetu badala ya kwenda mbele hatua kumi akaturudisha nyuma japo hatua moja tayari ameturudisha nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linatuhudhunisha, lina tusikitisha, linaumiza kuona kama wewe mtumishi wa umma ambaye umepewa jukumu umepewa dhamana badala ya kuridhika wewe huridhiki, hurudhiki unachokipata wenzetu wanafanya kazi hawa usiku na mchana wa kukusanya kodi wananchi wetu tunawakata kodi, mfanyabiashara tunamkata kodi lakini zinapokwenda kwenye mkono ya baadhi ya wengine walokuwa hawatosheki wanaona nimeletewa mimi ninyofowe. Mhe. Mwenyekiti, siku ya kuchangia hiyo hotuba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tutazonesha hisia zetu jinsi gani ambavyo tungependelea tuyaone kwa wale watu ambao wametajwa katika ubadhirifu kwa sababu kwaka 2013 kuna watu ripoti yao ilitolewa kwamba wamefanya ubadhirifu na hatujasikia hatua zilizochukuliwa kama tunavyoambiwa tukifanya kitu tukitangaze na hawa watangaziwe.

Kwa mfano, leo Wizara ya Afya kuna watu wamewalipa madaktari ambao hawapo wako Cuba pesa zimeanishwa mule tunakwenda wapi, daktari hayupo kisharudi Cuba lakini Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anasema Wizara ya Afya kalipwa, kalipwa nani malaika au shetani maana yake ndio tusiyemuona. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwamba sisi tuna kazi kubwa, serikali imejipanga inatekeleza, Mhe. Rais wetu wa Zanzibar masikini mzee huyu busara na hekima aliyonayo na uwelewa wake na uweledi wake na nguvu yake yote anafanya kazi, leo kusikia jambo kama hili kama anatoka watu au kuna mingoni mwetu wanakuwa bado hawataki kuona ukweli wa mambo haya, Mhe. Mwenyekiti inasikitisha sana. Kwa hivyo, nawaomba sana kwamba jambo hili wafanyakazi au watumishi sote si jambo zuri kwamba sisi ni wajibu wetu kuridhika na hichi tulichonacho. Kwa hiyo, ikiwa ni mkurugenzi au ni afisa, au ni nani unalipwa mshahara karibu milioni moja…

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano Mhe. Mjumbe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, utaniongeza tatu. Mhe. Mwenyekiti, shida kwa mtu yule wa kima cha chini tumeona leo Dkt. Ali Mohamed Shein alivyofanya, tizama serikali ilivyodhamiria kuwalipa wafanyakazi wastaafu imeongeza shilingi bilioni 2.4 za kiinua mgongo kwa ajili ya wafanyakazi wetu. Jamani tunataka nini, lipi linalotakiwa tena, kwa nini tusiridhike wenzetu hawa wanafanya kazi hizi ngumu kwa sababu hakuna pahala pagumu pakufanya kazi kama sekta yenye pesa ya makusanyo, ni rahisi kushawishika. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango hongera na timu yako lau kama ungelikuwa ni mtu lege lege au ni mtu mwenye tamaa usingefika hapa. Kwa hivyo, nasema wenzangu nawaomba tumuunge mkono sana, Mhe. Waziri yuko makini sana. *(Makofi)*

Kwa kweli, kuna watu watamchukia kwa sababu ya kufanya kazi, lakini siku zote ukilitenda lile zuri ambalo watu hawalipendi ndio utakapopata vikwazo kama hivyo. Lakini akirudi nyuma atakuja kuharibu, basi asirudi nyuma akaja akageuka jiwe, isipokuwa aendelea mbele tu na Mwenyezi Mungu atamsaidia na sisi tuko pamoja na yeye na *inshaallah* lengo letu litatimia tutafika tulipopakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii narudia kukwambia ni bajeti ya mfano na niwaombe wenzangu wote kwa umoja wetu tuiunge mkono bajeti hii na tutoe mashirikiano makubwa ili tuweze kumuwezesha waziri aweze kukusanya na aipe serikali pesa na mawaziri ambao kwa msingi tumeshawapitishia bajeti yao.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nilikuwa nataka kuzungumzia suala la maji ambalo Mhe. Hamza Hassan Juma amelizungumza sana. Mhe. Mwenyekiti, suala la maji bado ni tatizo pamoja na kuwa tunayo miundombinu ambayo kwa asilimia 90 imeshafika vijijini lakini uhalisia wa upatikanaji wa maji bado una matatizo. Kwa hiyo, naomba sana tu serikali kwamba suala la maji *ZAWA* waweze kuongeza kiwango cha uzalishaji wa maji, kwa sababu lengo lao uzalishaji wa maji bado liko chini kidogo pamoja na kuwa na miundombinu ya kutosha tunayo.

Tukijitahidi Mwenyezi Mungu atujaalie tuweze kuwafikishia wananchi wetu huduma za maji, kwa sababu kuna maeneo mengi ambayo bado yana mahitaji haya ya maji. Miongoni mwetu kila Mheshimiwa Mwakilishi hapa kadhia ya maji imemgusa, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango namuomba ule mradi kutoka India Mwenyezi Mungu amjaalie ampe uwezo tuusimamie ili uweze kufanikiwa, kwa sababu naamini mimi kwamba mradi ule ndio utakuwa mwarubaini wa tatizo la maji hapa Zanzibar. Tukiusimamia ule kwa upande wa huduma tukiweza kukamilisha malengo yetu ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, tukaweza kumalizia *Terminal III*, tukaweza kuimarisha miundombinu, tukaweza kuweka vivutio vizuri kwa watalii basi nina imani kwamba mwaka 2019/2020 tutakuja na bajeti ya *trillion* 1.5 ambayo inatekelezeka. Tuangalie vipaumbele ambavyo umevianisha ili tuvisimamie vizuri naamini hilo hutaki kuambiwa ili tufikie lengo.

Kwa mfano, leo hii ikiwa tulikuwa tunapokea watalii laki nne na zaidi tuweke lengo angalau la kupokea watalii 600,000 mpaka 700,000 ifikapo mwaka 2020, ili tuweze kukidhi lile lengo la makusanyo yetu ya ndani kama tulivyojipangia. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niliyoyazungumza kwa heshima kubwa na taadhima napenda kutamka kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na ninawaomba wenzangu wote tuiunge mkono na tuipitishe kwa shangwe na vifijo, ili serikali iweze kutekeleza adhma yake katika mwaka wa fedha wa 2018/2019. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako. Nimekuona Mhe. Simai Mohammed Said kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nasimama kwa kutumia Kanuni ya 58 pamoja na vifungu vyetu ndani ya Katiba ya Zanzibar, lakini pia 59(1) na 59(10) pamoja na 59(6) naomba ninukuu hiyo ya 59(10)…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba nikuweke sawa umesimama kwa Kanuni ya 63 kuhusu utaratibu, nimekuruhusu kwa hiyo nataka uniambie labda Kanuni gani imevunjwa ili tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, sikutaka kuisoma Nam.63 kwa kujua kwamba tumefahamu sote, lakini lengo langu naomba ninukuu Nam.59(10).

> “Katika mjadala wowote, mawaziri watatajwa kwa kutumia majina ya nyadhifa zao, wajumbe wengine wote watatajwa kwa kutumia neno “mheshimiwa” kabla ya majina yao, na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu wataitwa kwa mujibu wa nyadhifa zao wanapowasilisha ripoti za kamati”. Lakini ukisoma pia 59(6) inasema:

> "Ni marufuku kwa mjumbe yeyote kutumia jina la Rais au la Makamu wa Kwanza au Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni yakutaka kushawishi Baraza kuamua jambo lolote kwa namna fulani".

Mhe. Mwenyekiti, sina lengo au nia mbaya ya kumnyoshea kidole mjumbe yeyote isipokuwa tu nikukumbushana kwamba humu ndani tumekuwa tuna mazoea ya kujisahau kwa wakati mwengine tunavyomtaja Rais wa Zanzibar tunashindwa kumtaja kama ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Lakini mara nyengine watu humwita kwa jina lake Dkt. Ali Mohammed Shein inazungumzwa humu ndani. Kwa hiyo, mimi lengo langu ni kukusaidia wewe kama Mhe. Mwenyekiti juu ya kiti chako, juu ya kazi ili kuweza kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu wananchi wanatusikia tusiwe tunafupisha uraisi wake pamoja na kiti chake alichokalia. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Simai Mohamed Said kwa ukumbusho huo, lakini nadhani Mhe. Mjumbe aliyepita alikuwa akizungumza na akitaja Mhe. Rais kwa jina hilo pia ila ni vizuri kwa kutoa ukumbusho huo kama unahisi hilo jambo limezoeleka, basi nadhani Waheshimiwa Wajumbe wamekufahamu na hivi ndio tunavyotaka twende kwa mujibu wa kanuni zetu. Nakushukuru sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa kuzijua kanuni.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba tumshukuru sote Mwenyezi Mungu kwa kutupa pumzi na kuweza kuendelea na vikao vyetu hivi.

Mhe. Mwenyekiti, tuko hapa siku ya leo kuijadili Bajeti ya Serikali nzima ya Mapinduzi ya Zanzibar. Namshukuru Waziri wa Fedha na Mipango na watendaji wake wote kwa vitabu vyote hivi ambavyo toka juzi tulikuwa tunapewa muhtasari na hasa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo na makusanyo ya kodi, napenda kuipongeza Wizara ya Fedha na Mipango na watendaji wote wa wizara hii na taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya kama *TRA, ZRB.*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa wito kwa wafanyabiashara tuwe na utamaduni wa kulipa kodi, kwa sababu kodi ndio uhai wa utekelezaji wetu wa mambo mengi katika visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa hiyo, tuwe na mtindo wa kubadilika naomba taasisi hizi wazidi kutoe elimu kwa wafanyabiashara katika kodi hizi ambazo zinakusanywa na naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafikia malengo ambayo tumejiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wamekusanya kodi na wanaendelea katika mwaka huu wa fedha ambazo zisopungua *trillion* 1.1. Mhe. Mwenyekiti, kukusanya pesa zikaingia kwenye mfuko na matumizi yake, mambo mawili yako tofauti. Ukusanyaji wa fedha *ZRB, TRA* na taasisi zote hizo

zikakusanya pesa, lakini hofu yangu Mhe. Mwenyekiti tunaweza tukakusanya pesa matumizi yake ikawa tumebeba pakacha tukatia maji.

Mhe. Mwenyekiti, katika matumizi lazima serikali, viongozi na watendaji wote tuwe wasikivu na tujue tunafanya nini. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano moja tu ambayo haya yote niliyoyazungumza leo nina ushahidi nayo na nitaziwasilisha mbele ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tumemaliza bajeti ya Wizara ya Afya, tulipomaliza bajeti ya Wizara ya Afya siku ya tatu Wizara ya Afya wamepelekewa *invoice* walipe bilioni 3 za dawa. Sasa sisemi kwamba nini, lakini kwenye kitabu chetu hakijasemwa kwamba Wizara ya Afya inadaiwa na kampuni ya Dar-es-Salaam *three billion*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tumepitisha kwa nia nzuri bajeti ya madawa, bajeti ya sehemu mbali mbali za barabara, elimu, afya, kilimo na sehemu nyengine. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali inawezekana ndivyo, lakini serikali lazima ifanye uchunguzi je hizi *three billion* zilikwenda kwenye bohari kwa nini ikapita bajeti halafu siku ya tatu yule mfanyabiashara kutoka Dar-es-Salaam akaleta *three billion*.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema tuwe waangalifu sana, serikali yetu ni Serikali ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar tumekuja huku ndani kwa maslahi ya wananchi, "hujafa hujaumbika". Tumekuja huku kuwatumikia wananchi sasa tukija tukakusanya Wizara ya Fedha na Mipango, *ZRB, TRA* na taasisi nyengine zikakusanya fedha halafu hizi fedha zikawa hazifahamiki tukasema aah wizara hii tunaipa, lazima tuwe na uangalizi mheshimiwa tunachokipata ndio tunachokitumia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hilo nataka niliseme tunaijua Wizara ya Afya ni ya serikali ilikuwa inanunua madawa kwenye *MSD* lakini kama unafika pahala *over three billion* tuambiwe dawa zile zilitumika, ziliingia kwenye bohari au ndio kitu ambacho lazima serikali iwe waangalifu, *may be* niombe hilo.
Mhe. Mwenyekiti lakini isitoshe hapa tukija katika Wizara ya Kilimo tumekuwa na utamaduni wa kununua mbolea kupitia Dar-es-Salaam, kiwanda kiko China cha mbolea na ushahidi ninao, wizara inayohusika inakwenda kumtafuta mfanyabiashara Dar-es-Salaam ananunua kutoka China analeta halafu inalipwa Zanzibar, *we have to be honesty* Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu sisi sote na tuna uchungu na nchi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunatakiwa tuwe waangalifu, napenda serikali vitu kama hivi kwa nini visiende moja kwa moja kwenye viwanda anatokaje mfanyabiashara kutoka Dar-es-Salaam hivyo Wazanzibari wote hawana uwezo wa kuagiza mbolea na wakanunua, nina ushahidi. Lakini mbolea inanunuliwa Kiwanda cha China mfanyabiashara kutoka Dar-es-Salaam anaagiza sasa hizo gharama zinaongezeka. Kama gharama zinaongezeka tukipunguza gharama si tutapata mbolea nyingi, badala ya mbolea tani 400 tutapata tani 700. Kwa hivyo, naomba serikali tutakuwa tunakuja hapa tunazungumza mwelekeo wa bajeti lakini matumizi yake lazima tuwe waangalifu.

Mhe. Mwenyekiti, tunakopa, tunapata msaada awamu ya sita kwa mfano hapa, *terminal III* ile pale ilitiwa saini kwa milioni 58 dola. Matokeo yake awamu ya saba ilipokuja *terminal III* pesa za mkopo wanalipa Wazanzibari ilikuwa ni *terminal* ya maegesho ya ndege ya 737, wakati huo

Uwanja wa Ndege wa Zanzibar zimeshakuwa ndege zinatua 797, 767. Serikali ya awamu ya saba imebidi isitishe mradi ule wazungumze na Benki ya China tuongeze tena mkopo wa dola milioni 70. Sasa Mhe. Mwenyekiti, huu ni uzembe, ni aibu lakini ni huu mkopo ambao Wazanzibari wanakwenda kulipa. Kwa hivyo, 508 tumeongeza ziada ya milioni 70 haya yote yamo kwenye matamshi ya serikali. Kwa hivyo, tunakuwa sio wabunifu, uwezo wetu mdogo kila mmoja anataka kusema aah mimi sasa hivi awamu yangu hii wacha nikatie jiwe la msingi pale nionekane mimi nimetia jiwe la msingi *terminal III,* kumbe unataka kuwatia hasara Wazanzibar, huu ndio ukweli.

Kwa hivyo, *terminal III* ile awamu ya saba ndio iliyofanya kazi ikasitisha mradi ule ili kuupanua wigo, ndege kubwa zitue na ziegeshe na *runway* zifanye. Kwa hivyo, serikali ikabidi izungumze tena na benki kutafuta mkopo. Mimi naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kututilia dhamana tukapata mkopo ule. Kwa hivyo, lazima kufanya kosa si kosa, kurejea kosa ni kosa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka tuwe waangalifu sana katika taasisi hizi tunapofanya mchakato wa kununua vifaa na wa kutizama mambo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika yote hayo nataka tuwe wakweli, mwenzangu hapa ndugu yangu Mwakilishi wa Jimbo la Konde ametoa ufafanuzi mzuri sana. Mhe. Mwenyekiti, kama hatuko tayari tafadhalini msituletee waraka wa mkaguzi mkuu au jambo lolote pasipokuwa na majibu. Sote ni watu wazima, sote tunafahamu na sote tunaelewa.

Mhe. Mwenyekiti, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (*CAG*) wajumbe hapa wameisoma ripoti na huyu Mkaguzi wa Serikali yumo ndani ya Katiba ya Zanzibar *page* 136, kifungu cha 112 ametajwa humu. Leo Mhe. Mwenyekiti, tunakuja hapa tunaambiwa taasisi hazijawasilisha mahesabu, mkaguzi yumo ndani ya Katiba. Lakini mimi kinachonipa hofu mheshimiwa sisi kama wafanyabiashara imetajwa na *PBZ*, sasa sisi wafanyabiashara tunapata wasi wasi tuna pesa zetu tuna uzalendo wa kuweka pesa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi ninachosema ni suala ambalo limo na kama hatukuwa tayari kuzitaja au kuzileta tusizilete humu ndani, imo ndani ya Katiba au tuifute Katiba hii. Mhe. Mwenyekiti, lazima tuwe wa kweli haya mambo yametokea Bara Serikali hii ya CCM ya Rais John Pombe Magufuli kuna wengine wamekwenda kwenye makarandinga kule ndani. Tusijione kwamba hapa tuna miaka miwili ya kushuka kilima, tusioneshane mabavu watendaji ndani ya serikali hadi miaka miwili tunateremka kilima hivi sasa. Lakini, ile pale Serikali ya Rais Magufuli mafisadi wote wamefichuliwa pale na wengine wamewekwa ndani na wengine wanafyagia Muhimbili pale lazima tuwe wakweli kwani tuna utawala bora, *good governor* lazima tuambizane hatukuwa tayari tusilete humu ndani kwani sisi watu wazima ndani ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, hii ndio Katiba na nitaiwasilisha nisije nikaambiwa Katiba hii kaandika Mohammedraza hapa. Kwa hivyo, yamo ndani ya Katiba tunajadili masuala ya nchi, tunajadili masuala ambayo yana faida taasisi tunauliza zimepata hati vipi. Kwa hivyo, niipongeze kamati hii iliyowasilisha na hii ni *hansard* nimeichukua moja kwa moja kwenye kamati.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kwenda na vitu ambavyo havina utaratibu maalum. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na serikali nzima tuwe waangalifu sana, tunakijua

kila kinachotokea, lakini kuna mambo mengine inabidi uweke mawe mfukoni ya hakiba, huwezi kupanda mchongoma ukavuna zabibu.

Mhe. Mwenyekiti, naliomba hili katika masuala mazima ya ukusanyaji sina tatizo, lakini matumizi yake serikalini na haiko mbali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tuje katika masuala ya fedha ya pamoja, *account* ya pamoja. Nafikiri bado lazima tutizame Muungano wetu uliokuwa mzuri, Muungano wetu uliokuwa umetuletea historia, lakini na hii Tume ya Pamoja ya Fedha imo ndani ya katiba, *page* 187 kifungu 133.

Mhe. Mwenyekiti, ipo Kamati ya Fedha ya Pamoja hiyo ndio itakuwa suluhisho la matatizo ya Muungano. Juzi Rais wetu mpendwa John Pombe Magufuli amepokea karibu *over billion as dividends from TTCL*. Je, tunajiuliza Zanzibar hatumo. Kuna mashirika mengi kama *Air Tanzania*. Mhe. Mwenyekiti, kwa zaidi ya miaka kumi hakuna utekelezaji wake. Sasa hii Tume ya Pamoja ya Fedha ingelitoa matatizo yote ya Muungano kwa sababu kila mmoja ana shida. Kwa hivyo, Tume ya Pamoja ya Fedha ingelikuwa suluhisho la mambo yote tunajua kama hizi pesa za Muungano, lakini Mheshimiwa leo hatujui kwamba wenzetu wanapokopa pesa wanakopa kwa serikali gani.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwe muwazi na tuzungumzeni uwazi, sote tuuzungumzeni uwazi. Bunge linakutana kule, Baraza la Wawakilishi linakutana, Waziri wa Fedha kule katoa bajeti ya Wizara ya Fedha Serikali ya Muungano, Waziri wa Fedha na Mipango katoa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, "funika kombe mwana haramu apite", Serikali ya Tanganyika imejificha ndani huu ndio ukweli, ndani ya Muungano wetu na *we have to be honest*. Hivyo bajeti wale wanazungumza mwisho Chumbe na sisi tunazungumza mwisho Chumbe *unless to be honest*, lazima tuwe wakweli, tunapenda Muungano lakini tuwe wakweli. Hii hapa yupo Waziri Philip Mpango na hapa yupo Waziri wa Fedha na Mipango yule pale Dokta Khalid Salum Mohamed vitu viwili tafauti.

Kwa hivyo, niombe sana Mwenyekiti hapa tulikuwa na matatizo kama unakumbuka kulikuwa na makubaliano ya *OIC*. Mimi nina ushahidi kwamba tumejiunga na *OIC* na Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Salmin Amour Juma (Komandoo) alituita pale Darajani, akasema tulikwenda kwenye *OIC* nanukuu lugha yake, "kwa sababu ya njaa, kule kuna neema". Nchi ambazo sio za Uisilamu Burkinafaso, Zambia, Msumbiji zote zimejiunga lakini Rais wetu alitwambia Wazanzibari tunaupenda Muungano, tumewaachia Serikali ya Muungano wajiunge na Rais Mzee Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na alikuwa na John Samuel Malecela kwa maandishi na yapo.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tuwe wawazi mimi nina uchungu na nchi, sina urafiki na nchi, iko wapi *OIC* tulipata shida. Hivyo wenzetu hawa wakitaka masuala ambayo ya katiba wao hawana tatizo, sisi tukitaka kujiamulia kujiongezea maisha yetu au uchumi wetu katiba. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti *OIC* lilikuwa ni suala ambalo tulikuwa tufaidike sote. Aliyekuwa Rais wa Zanzibar Dkt. Salmin Amour Juma wakati ule miongo miwili. Kwa hivyo, niombe sana jamani tusikimbie muangaza suala hili. Nashangaa leo Wazanzibari tunakuja ndani tunapiga kelele, tulikwenda kwenye Bunge la Katiba tukatafautiana pale, tukatishana, leo kasa kumcheka kobe.

Mhe. Mwenyekiti, kasa kumcheka kobe...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tano.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Dakika tano ahsante. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tuwe na hii Tume ya Pamoja ya Fedha tupate ufumbuzi. Kwa kweli, naamini Mhe. Rais John Pombe Magufuli kama angelikuwa anaambiwa ni msikivu sana katika historia ya Tanzania na Mhe. Rais wa Zanzibar Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais wetu mpendwa suala hili lipate ufumbuzi halafu tuna mambo mengi ya kiuchumi, kuna mambo mengi ya kujadili. Leo Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje wameweka Ushirikiano wa Kimataifa, wizi lazima tuwe wakweli tusikae humu ndani tukasema tu Muungano, Muungano, tumeyataka wenyewe haya, tumetishiana maisha huko Dodoma. Mimi mtu alinambia tutakuuwa, huu ndio ukweli kwa Mwenyezi Mungu, *Lailaha ilallah Muhamad Rasulullah.*

Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali mbili zikae katika mjadala wa Tume ya Pamoja ya Fedha, tuvumiliane, tuheshimiane, tujadiliane na masuala mengine haya huyu mkaguzi wa katiba hili suala tupatiwe ufumbuzi, tuna mambo mengi ya matumizi.

Kwa hivyo, namuomba Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na serikali majimbo yetu vijijini likiwemo jimbo langu la Uzini tunaomba kupelekewa vifusi. Mimi niko tayari kuchangia, kule ndio kwenye *grassroots* Mhe. Mwenyekiti tatizo kubwa visiwa vya Unguja na Pemba ni vijijini barabara zetu wala hatutaki lami. Kwa hivyo, naiomba serikali katika suala zima hili la matumizi ya fedha serikali kila inapotia pesa ikatizame mradi ule ndio unatumika au pesa zilizoingizwa ndizo zile zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache niliyokuwa nimeyazungumza niishie hapa naishukuru serikali mimi sina tatizo, lakini tuwe waangalifu katika matumizi, tuwe waangalifu katika masuala yote, lakini tuwe waangalifu katika mikataba ya mikopo tunayochukua tusije tukafanya kama yale tuliyofanya, tuwe waangalifu sana.
Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi yamevurugika nchi hii mikataba mingi hayakupita katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu huu ndio ukweli, kwa Mwanasheria Mkuu hayakupita, Mwanasheria Mkuu na Wizara ya Fedha na Mipango wanakuja kupachikwa jambo halafu wao ndio wanaonekana ndio watu wabaya katika kulijadili.

Kwa hivyo, naishukuru sana serikali, niwatakie kila la kheri watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango ninaamini wana uwezo, wana hekima, wana busara, wana usikivu na mimi niunge mkono bajeti hii Mwenyezi Mungu atujaalie kwa siku ya leo ambayo imesimamisha nchi nzima ili matumizi tutapomaliza hapa na niwaombe wenzangu katika taasisi moja ambayo wako watu wafanyaji kazi basi Wizara ya Fedha na Mipango. Kuanzia *ZRB, TRA*, kote huko wamejipanga, nafikiri kina Dkt. Khalid wamejipanga kama akina-Ronaldo na Messi kule. Kwa hivyo, ninaamini uwezo wanao lakini wawe *very serious* katika matumizi ya pesa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naishukuru serikali, naishukuru wizara, naiunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niruhusu hizi katiba nisije nikaambiwa Mohammedraza Hassanaali Mohamedali kaziandika nimpelekee Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango zionekane kwamba hizi katiba ni za nchi, ambapo haya yote niliyozungumza pamoja na Tume ya Fedha ambayo nimechukua *hansard* naomba kuwasilisha kwa Waziri wa Fedha iwe kama kumbukumbu zake, kwamba hii katiba niliyoileta hapa si ya Mhe. Mohamedraza ni ya nchi yetu kwa maslahi ya nchi yetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mohamedraza Hassanaali Mohamedali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akifuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahmani Rahiim.* Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika mwelekeo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo 2018/2019. Naomba nianze kuchangia katika ukurasa wa 34 ambao unasema miradi ya mashirikiano ya sekta za umma na binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kueleza hapa umeeleza ujenzi wa nyumba za bei nafuu eneo la Ng'ambu, kujenga Chake Chake, ujenzi wa kituo cha daladala Kijangwani, ujenzi wa nyumba za bei nafuu. Sasa naomba kushauri kwa Waziri wa Fedha na Mipango kwamba tunapotaja nyumba za bei nafuu basi zije kuwa za bei nafuu na sio kwa maneno tu. Nitatoa mfano mdogo tu ambao umetokea katika nyumba za Mradi wa *ZSSF* unaofanyika Mbweni.

Hivyo hivyo, tulisema kwamba tunajenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya wananchi waweze kumiliki, leo nyumba zile ambazo ujenzi wake upo zaidi Kichina umefuata majumba ya China vyumba vidogo na majengo yenyewe kama yanavyoonekana *style* yake yako Kichinachina, nyumba ya rahisi pale yenye vyumba viwili nafikiri inaanzia na shilingi 159,000,000/-, kuna bango kabisa pale. Nyumba ya vyumba vitatu shilingi 179,000,000; nyumba ya vyumba vinne shilingi 259,000,000/-. Sasa nyumba hizi Waziri wa Fedha atakuja kununua mnyonge gani? Hebu tuelezane nyumba hizi kakusudiwa nani. Sisi Waheshimiwa Wajumbe humu ndani hatuwezi kununua nyumba zile sikwambii mwananchi wa chini ambaye ana mshahara wa shilingi 300,000/- au wale wanaolipwa mshahara wa shilingi 150,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuna sehemu nyengine tusitegemee kwamba watalipwa mshahara wa shilingi 300,000 ziko sehemu za kujishikiza mtu anapata shilingi 150,000 kwa mwezi. Sasa ukipiga hesabu ya shilingi 159,000,000/- ukiigawa hiyo kwa mshahara wa shilingi 300,000/- inakuja miezi 530 ili aweze kulipa nyumba ile iweze kuwa yake ya vyumba viwili Mbweni. Sasa tujiulize miezi 530 tukiigawa mara 12 inakuwa miaka 44 ndio mtu aweze kumiliki nyumba ile tena kwa shilingi laki tatu tatu, ikiwa kwa shilingi 150,000 mtu anatakiwa kulipa kila mwezi basi miaka 88, hivi kuna mtu ambaye atakuwa yuhai miaka 88. Nani ataweza kumiliki nyumba zile kwa miaka 88.

Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Waziri miradi ya serikali inapojengwa hasa kwa ku-*target* wananchi wa hali ya chini basi waweze kumiliki kikweli kweli na sio watu wajenge bei ziwe kubwa, nyumba zile watakuja kununua wengine na baadae ziwashinde badala ya fedha zilizoingizwa kwenye *investment* ya kupata faida watakuja kupata hasara. Sasa tunaomba sana kwa Mhe. Waziri nyumba hizi ambazo nyengine zinataka kujengwa basi angalau tuje tusikie

nyumba ya vyumba viwili shilingi 30,000. Hii ndio itakuwa hasa kwa watu wenye uwezo wa chini wataweza kumiliki kwa mafungu ambayo ya kulipalipa, lakini tukija na ziada ya kuanzia shilingi 60,000,000 au shilingi 100,000,000 hiyo hata Waheshimiwa Wawakilishi itawashinda.

Tuzungumze ukweli, mimi nimepiga hesabu hapa ya ghafla kwa shilingi 300,000 ukilipa kila mwezi uwe unakatwa shilingi 300,000 kwa njia ya deni hapo tena bila ya riba, maana yake kama unachukua benki ukalipe riba sijui nani atakukopesha Tanzania hii bila ya kumuongeza chochote kwa miaka hii. Mhe. Waziri tunamuomba nyumba zile zishushwe bei ile bei iliyopo hailingani kabisa na kiwango kile na hasa ukiangalia *standard* ya nyumba zile na bei zilizopo hazilingani kabisa. Nyumba zile kwa kukisia kwamba *apartment* iliyokuwa na vyumba viwili basi angalau iwe shilingi 80,000,000 kwa nyumba za pale Mbweni kutokana na *area* yenyewe na sehemu ya hali iliyopo, la kwa bei iliyowekwa hatoweza kununua mtu na atakaenunua pale basi huyo ana pesa hajui afanye kazi gani kwa sababu shilingi 159 milioni unajenga nyumba ya chini, una *villa* yako mwenyewe, una *garden* yako, una *fence* yako na pesa itabakia yenye vyumba vinne.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 32 kitabu hicho Utafiti na Nishati Inayorejesheka Jua na Upepo. Mhe. Mwenyekiti, matokeo ya ripoti ya utafiti awali ya mwezi Ogasti, 2017 yanaonesha kuwa wastani wa kiwango cha nguvu za jua kwa siku ni 5.75 *kilowatts*. Halafu hii inathibitisha kuwepo kwa kiwango cha jua cha kutosha nchini kuendelea na uwekezaji katika uzalishaji wa umeme wa kutumia nguvu ya jua.

Mhe. Mwenyekiti, tungemuomba sana Mhe. Waziri kushirikiana na wizara husika kwamba wahakikishe sasa Zanzibar tunakuwa na umeme wetu tujitegemee wenyewe. Umeme wa *TANESCO* uwepo lakini vile vile tutapoleta umeme wetu wa jua, umeme wetu wa upepo na umeme wa bahari wote Zanzibar inawezekana kwa sababu bahari imezunguka kila kona na vile vile upepo tunao na jua tunalo. Sasa tumuombe Mhe. Waziri kwamba ifike wakati iwe historia kutegemea umeme wa *TANESCO* na badala yake kuwa na umeme wa Zanzibar sisi wenyewe na umeme wetu. Kwa kweli, umeme tunaonuua ni bei ghali kama alivyoeleza Mhe. Mbunge umeme tunalipa kule asilimia 18, tukija huku tunalipishwa tena asilimia 18, kuna *infrastructure tax* asilimia 2 na kuna nyenginezo ambazo wananchi hawazifahamu. Sasa umeme Zanzibar ni bei ghali japokuwa serikali inasaidia kulipia lakini bado kwa wananchi umeme bei hii ni kubwa. Sasa Mhe. Waziri afanye maarifa yake yote kabla hajaondoka madarakani tujue kwamba mradi wa umeme wa jua, upepo au ukiwa wa bahari uwe Zanzibar umeshaanza watafutwe wafadhili au serikali yenyewe iingie *share* na mtu lifanywe suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee kwenye mwenendo wa uingiaji wa watalii Zanzibar. Mwaka 2017 watalii waliofikia ni 433,474. Mwaka 2016 walikuwa 376,242, nchi ambazo wanazitaja kwamba zimeleta wageni wengi ni nchi za Itali, Ujerumani, Uingereza na Israel.

Mhe. Mwenyekiti, kama Zanzibar tutaamua, kama serikali itaamua vizuri kuiwezesha sekta ya utalii au wizara ya utalii kwenye kuwapa fedha za *marketing*, kuwapa fedha za kuweza kwenda nje kujitangaza zaidi kwa nchi ambazo wageni wao hawajaanza kuwaleta kwa wingi, hapa tuki-*deal* na nchi kama China yenye watu 1.4 billion, tukifanya *marketing* tukazungumza na Serikali ya China basi hata pa kuwaweka sisi hapa Wachina hatuna. Kwa kweli, Wachina wanasafiri duniani kwenda nchi za nje pekeyao zaidi ya 30 milioni kwa mwaka, hapa waje milioni moja tu basi hatuna pa kuwaweka, vyumba tulivyonavyo sasa hivi ndani ya Zanzibar ni vitanda 45 elfu.

Ukienda nchi za wenzetu vitanda 45 elfu ni hoteli 12 tu zina vitanda 45, Zanzibar nzima tuna hoteli 460 tuna vitanda 45 elfu. Sasa Mhe. Waziri kuna haja wale wawekezaji wanaokuja hapa wasiwe na lengo la kuzungushwa waachiliwe wafanye *investment* kwenye masuala ya hoteli watu tuna vyumba vya kutosha na tunapokwenda kufanya *marketing* ya utalii watapokuja wageni basi wawe wana sehemu ya kukaa bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza hivi kwamba Ujerumani ina watu 82 milioni, Itali 59 milioni, UK 66 milioni, Israel milioni nane na laki nne, jumla ni 216,300,000. China ina watu 1.4 billioni, India 1.3 *billion*, *United State* 326 milioni, Brazil 210 milioni, Russia 144 milioni, Egypt 99 milioni, Uturuki 81 milioni, jumla ni 3.4 *billion* na kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nchi hizi nilizozitaja kama tutakwenda kufanya *marketing* tukakaa na wizara ya utalii ya nchi hizi baina ya nchi yetu na wao wakiamua kutangaza kuwahakikishia wananchi wao kwamba Zanzibar ni nchi ya usalama, ina utalii mzuri, basi hapa Zanzibar mwaka 2020 tuna watalii milioni nne na sio laki nne tena. Uwezo huo upo ni kwenda kujitangaza kukaa na wizara za utalii za nchi za nje pamoja na yetu tukafanya kazi kwa pamoja, tukingojea tutegemee *tour operator*, tutegemee serikali twende tukashiriki kwenye maonesho ya *Germany Frankfurt* au kwengine kujitangaza haitoshi ni lazima tushirikiane na wizara za utalii za nchi hizi nilizozitaja na nyenginezo tutaweza kupata wageni milioni nne kwenye mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye sekta za nje, biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Jumla ya thamani ya uhaulishaji na bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara imefikia thamani ya shilingi 240 bilioni. Kati ya uhaulishaji huo, bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar zimeongezeka kufika thamani ya shilingi 206 bilioni mwaka 2017 kutoka thamani ya shilingi 138 bilioni mwaka 2016, na ongezeko la asilimia 49.6. Aidha, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umepungua kutoka thamani ya shilingi 84.7 bilioni mwaka 2016 kufikia thamani ya shilingi 33 bilioni mwaka 2017, sawa na asilimia 60 ime-*drop*.

Mhe. Mwenyekiti, tungemuomba Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Biashara na Viwanda kama inavyokwenda. Sasa ni lazima serikali hizi mbili zikakaa viongozi wa juu tukafahamiana lugha na mimi naamini Mhe. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi watapokaa pamoja kuzungumzia hali halisi ya masuala haya pamoja na kuwashirikisha Mawaziri wa Fedha wetu na wa biashara kuondoa matatizo haya basi Zanzibar kutakuwa na uchumi na biashara nzuri *between* Zanzibar and Tanganyika.

Hii hali haielekei wao tunaona hapa kwamba wamepata *profit* bilioni mia mbili na sita wao wamekuwa kwa asilimia zaidi ya 39, sisi tume-*drop* asilimia 60 maana yake nini inaonesha dhahiri kwamba kuna vikwazo vimetokezea Zanzibar kiuchumi tumeumia kwa mwaka huu.

Sasa Mhe. Waziri tunaomba sana matatizo haya muyatatuwe kwa kuanzia wao wenyewe mawaziri yamewashinda basi watuambie tujue tunafanya vipi au pelekeni ripoti vizuri huko mbele kwa Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Rais ambao watajua wenyewe wanafanya vipi.

Mhe. Mwenyekiti, ikikaribia dakika kumi naomba unambie.

Mhe. Mwenyekiti, pato la wananchi linasema sasa hivi kwamba ni milioni mbili na elfu ishirini na moja kwa mwaka 2017 limepanda hapo limekuwa milioni mbili na elfu ishirini na moja, sawa sawa na dola mia tisa na saba. Ukiangalia kwa mwezi ukiigawa hiyo milioni mbili na elfu ishirini na moja unapata laki moja na elfu sitini na nane, laki nne na elfu kumi na sita na kwa siku elfu tano na mia sita.

Sasa Mhe. Waziri tunaomba sana pato hili serikali yetu kweli inajitahidi lakini pato dogo sana kwa wananchi na sio wote wanaomiliki fedha hii, hii ni watu wachache ambao wanaweza kumiliki wenye kazi na ambao waliokuwa hawana kazi hata fedha hii hawaipati ndani ya Zanzibar.

Tuna *population* ya watu *1.5 million* lakini kwa siku kama mlivyoeleza kwenye kitabu chetu kwamba kwa siku wanapata elfu tano na mia sita sijui hapo mtu atapa mlo wa muda gani kama anakuwa mtu anakula mara tatu basi atapata *breakfast* tu kwa bei hiyo kwa bei za Zanzibar hasa sasa hivi vitu vilivyokuwepo. Tunaomba sana na hili mliangalie muweke masuala hayo sawa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2018/19. Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna maswala mengi tu yamezungumzwa miundombinu kuna masuala ya barabara, kuna masuala ya *Terminal III*. Naomba sana Mhe. Waziri, pesa tunazotumia ni nyingi serikali wana-*invest* pesa nyingi sana tuhakikishe kwamba *value for money* inakuwepo. Haiwezekani kwamba mtu tuna-*invest* vitu halafu ndani ya muda wa mwezi sita mwaka vinaaza kuvuja barabara zinajengwa za mabilioni baada ya mwaka mmoja zimeshafanya mashimo mtu anaweza kuotesha hata mti huko tutakuwa hatuendi. Hata wananchi watakuja kulaumu fedha zao zinavyotumika waone matunda kwamba vitu vinavyofanyika vinakuwa katika *high standard*.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye kitabu chengine kuhusu Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2018/19. Niende kwenye suala la wenzangu wengi waliozungumza ukurasa wa 35 ambapo ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakukumbusha una dakika tano.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mhe. Waziri alizungumza kwamba ushuru wa forodha na kodi nyengine kwa uingizaji wa bidhaa muhimu za chakula kama vile mchele, Unga wa ngano na shukari. Hata hivyo, kufuatia kuimairika kwa uzalishaji nchini kupitia kiwanda cha unga wa ngano cha *Zanzibar Milling Corporation* na kufufuliwa kiwanda cha sukari cha Mahonda inajitokeza haja ya kupunguza unafuu unaotolewa na uiongizaji wa bidhaa hizo muhimu, ili viwanda vyetu viweze kuhimili ushindani wa haki. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba Mhe.Waziri kwamba Waheshimiwa karibu watatu wameshazungumzia hili na mimi wa nne kwa kweli suala hili Mhe. Waziri haliwezekani.

Kwa sasa hivi ni vyema tunapotaka kufanya maamuzi basi ni vyema tukawashikirikisha wafanyabiashara wa Zanzibar wote kwa pamoja tukaa nao tukawasilikilza na wao wanataka vipi tukakaenao pamoja. Hii hatuwezi tu tukaja moja kwa moja mimi leo nakupa Mhe. Waziri uhakika nimeenda dukani pale Kibandamaiti nimenda kununua mapolo mawili ya kilo 50 leo kuhakikisha tu suala hili Unga wa Bakhresa ni elfu wa arubaini wa tisa ambao unaitwa Unga Poa

risiti hizi hapa na kampuni nyengine elfu hamsini na sita mtu huyu kwenye Zanzibar *Milling* hizi hapa ana-*save* elfu saba kwenye kila polo.

Leo tuna mpango wa kuja kuwazidishia kodi kwa kumsaidia mtu mmoja, hicho kitu hakiwezekani. Lazima tukae na wafanyabiashara wote wao hapa wanasaidia kipaombele kiuchumi wako juu vile vile na hawa wote ni *local investors* ambao ni Wazanzibari wazaliwa. Tuangalie Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Nakukumbusha Mhe. Mjumbe dakika tano zimebaki.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nilisema zikibakia dakika kumi unikumbushe. Naomba dakika kumi unipatie.

Mhe. Mwenyekiti, nimefanya *research* kiwanda kile kina waajiri hamsini na nne *Zanzibar milling*, lakini kuwachanganya wafanyabiashara walioko Wazanzibari ambao karibu wanne wanaoleta karibu wanne wanaoleta vitu kama hivi wana wafanyakazi mia tatu na hamsini kodi wanalipa asilimia 10 yeye huku *Zanzibar Milling Corporation* hailipi kodi imeachiwa *exemption* kila polo anapata elfu saba tena tunataka kufanye nini sasa hivi.

Kwa kweli, nilifikiria serikali itakuja na wazo la kusema wanaweka sawa au la kupunguza kidogo kwa hawa wanaoleta sasa hivi tunataka kumsaidia mtu ili tuangushe wengine. Hapa tunataka kuona bishara watu wana-*competition* kama ilivyo biashara za ndege na biashara ya meli mnaona, sasa hivi kuna meli moja tu kampuni mmoja tu ndio inayotawala zikija kampuni nyengine ndio vizuri *competition* itakuwepo, watu watachagua bei zatashuka hatutokwenda hivyo. *(Makofi)*

Leo umeona meli ya serikali ikiharibika tu siku moja tu watu wote hawana raha kwa sababu wanaumia watu wengine hawawezi kumiliki. Sasa na kwenye biashara tuje tuende kwenye masuala ya kuwashirikisha wafanyabiashara na wao wakatoe michango yao tukawashauri au kama ikibidi tuwape maeneo wafanye nao viwanda uwezo wa kufanya viwanda upo, kuliko hivi tunavyokwenda. Mhe. Waziri kwa suala hili na mimi sikubaliani nalo kabisa hatuwezi kwenda kwa namna hii.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na masuala mengine ambayo nitaeleza hapa deni la taifa limekuwa kwa bilioni mia tano na kumi na tisa. Lakini Mhe. Waziri kama ingekuwa Airport *Terminal III* imefanyika vizuri na hajapita uzembe basi bilioni sabini na nane pointi tisa tungekuwa sasa hivi hatuzihesabu kuzidisha deni la taifa la nje.

Leo deni limeongezeka kwa bilioni sabini na tisa kwenye mradi mmoja tu ambao umesababisha matatizo ya kitoto haiweze *contractor* ambaye Injia anaejenga *Airport* akafeli kwenye mambo madogo madogo. Injia anaejenga *Airport* ana *grade A* lazima aweze kujenga na anakuwa nauhakika mainjia tunaotumia pale na vichwa vyetu sisi vya Unguja tuliokuwa hatuwezi kazi tushaharibu mambo, bilioni thamanini na nane na kidogo tisa nyengine tumejizidishia deni la taifa leo tutaanza kulipa kwa muda wa miaka mingapi keshokutwa inakuja serikali nyengine huu mtihani tunaoenda nao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kupongeza na kujipongeza mimi mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba toka kaingia madarakani kuendesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hajawahi kufeli kwenye suala la uchumi kupitia Waziri wa Fedha na watendaji wake miaka minane tunakwenda sasa hivi uchumi wa Zanzibar hatujawahi kusikia ume- *drop* unapanda tu na hii hongera sana nawapa. (*Makofi*)

Lakini haya niliyozungumza yaje yafanyiwe kazi kwa maana ya kwamba tuzidi kupata sifa. Kwa kweli, naamini Rais anaejitayarisha kuja mwaka 2020 Zanzibar hana kazi, kazi iko safi nyeupe Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wetu Waziri wa Fedha na Mipango jitahidi tupige hivi hivi 2020 bajeti iwe *trillion 2* au *1 billion dollars 2.3 trillion* tupige kazi haya ndio mambo tunavyotakiwa tuende.

Mimi namsifu kwa sababu mimi tabia yangu mtu anapokesea nasema anapofanya vizuri nasema. Mimi toka nimeingia humu ndani sijaona kwamba Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Waziri wa Fedha kwamba uchumi wetu umeshuka sijaona na hili nalipongeza sana tuendelee kufanya kazi na huu ndio wajibu wetu tuliopewa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kukamilisha Ilani yake ya Chama cha Mapinduzi kwenye Jimbo la Chaani. Hivi ninavyokwambia ahadi zote alizoahidi ndani ya Jimbo la Chaani ameshamaliza asilimia mia moja, keshajenga soko, barabara sasa hivi keshalipia yeye ndie anadai kazi, tangi la maji, kituo cha afya na vitu vyengine nitamuomba aje aniletee mimi ili mwaka 2020 asisogee mtu ndani ya Jimbo la Chaani.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakuhakikishia mimi mwenyewe kwa Ilani yangu mimi asilimia tisini ya Chama cha Mapinduzi nimeshamaliza ndani ya Jimbo la Chaani na nawaongejea hao wanaotaka kuja niwakate roho tuendelee na kazi zetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafahamu wako wateuzi ambao Mhe. Rais mwenyewe kawateuwa wanaotaka jimbo lakini jimbo lile ni la Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf Kwa sababu wananchi wanamuamini keshafanya mambo na Rais yuko pamoja na mimi na tunapiga kazi pamoja hatuwezi tukenda.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hapa tunakuweka *line* sawa mwaka 2020 Jimbo la Chaani ni sawa sawa na kwamba upinzani wa vyama vyengine na CCM naamini na mimi na huyo atakaekuja ndie huyo huyo. Niko vyema, niko tayari na nimebakisha ahadi mbili tu za vituo vya daladala na masuala ya uvuvi na haya nayapiga *before 2020*. (*Makofi*)

Sasa niwaambie tu viongozi wa Chama cha Mapinduzi watulie Jimbo la Chaani ni la Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf na pale Mhe. Rais huyu huyu au atakaekuja atanibatiza mimi kuwa ni Mhe. Rais wa Jimbo lile. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na yeye ndie atakaeniweka madarakani kama alivyoniweka safari hii kupitia chama changu. Kwa sababu yeye ndie anaepanga na yeye ndie alienijaalia na naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Jimbo la Chaani mimi nitaendelea kuwatumikia mpaka watakaposema wao basi. (*Makofi*)

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, niipongeze hotuba ya Mhe. Waziri nimuombee kwamba yeye na watendaji wake wote hasa *ZRB, TRA* kwa uungawa wao waliokuwa nao wa kuweza kustahamili kwa baadhi ya mambo madogo madogo kuwachukulia wafanyabishara wanapokosea waendelee hivyo hivyo Makamishna wote watendaji wote wasiwe tu katika hali ya siku hizi wafanyabiashara baada yake wakiona kuna hali ya kuwapunguzia kuna hali ya kuwaone huruma wazidi kuwaonea huruma kwa sababu sisi ndio hali hali tunaiona nchini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo mimi nai- *support* asilimai mia moja. Lakini tuje tupate majibu kwa Mhe. Waziri yaturidhishe hasa kwenye *Zanzibar Millings Factory* ambayo tumeizungumza hii kwa kweli inatuumiza vichwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe nilimtaja Mhe. Rashid Makame Shamsi lakini nimuombe radhi baada yake nimwite Mhe. Mohamed Said Mohamed atafuatiwa na yeye Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini ajiandae.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana lakini vile vile nichukuwe fursa hii kwa aina ya kipekee sana kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa uwasilishaji wa hotuba yake hii nzuri.

Vile vile nichukuwe fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wote Katibu wa Tume ya Mipango na wote waliochangia kuweka hotuba hii nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa na mambo kidogo tu ya kusema kwa siku hii ya leo kwa sababu mengi kamati yangu imeshayasema lakini nikaona sio busara kuwa nisiseme japo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuanza kwenye kitabu hichi cha mapitio ya hali ya uchumi 2017 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2017/18.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende kwenye ukurasa wa 18 kama Mhe. Nadir Abdul- Latif alivyosema lakini mimi nitatia nyama tu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kwa ruhusa yako:

> "Pato la mwananchi ya makisio ya kiwango kinachoonesha wastani wa fedha anachoweza kupata kila mtu kwa mwaka kiwango hicho kimekadiriwa kugawanywa kwa pato la taifa la mwaka dhidi ya idadi ya watu wa Zanzibar inakadiriwa kuwa idadi ya watu watapatao milioni moja laki tano thalathini na nne ambapo kwa kiasi kinajadiliwa kuwa ni ongezeko la idadi ya watu limefikia asilimia 2.8."

Mhe. Mwenyekiti, nikuwa tu napata wasi wasi sana juu ya hesabu hii. Sasa nikiipiga hiyo kwa haraka kwa mwezi maana yake pato ya mwananchi kwa mwezi napata milioni mbili na ishirini na moja elfu hiyo kwa mwaka na idadi ya watu kama hiyo. Lakini pato hilo kwa mwezi ninapata laki moja sitini na nane elfu laki nne na kumi na sita na senti sitini na saba kwa mwezi. Lakini nikija kwa siku napata elfu tano mia sita na kumi na tatu na senti thamanini na tisa na kiwango

hicho Mhe. Mwenyekiti, nakiona kidogo sana na hilo ni pato sio la mwananchi yule wa chini hiyo ni *flat rate* kwa kila mtu ambalo kwa sababu ya uchumi huu. Mhe. Mwenyekiti, mimi si mchumi huwa naomba ni-*declare interest* mapema sana ninapokosea kiuchumi naomba mnisamehe sana.

Sasa nataka nitizame hii shilingi elfu tano kwa mwananchi wa kawaida. Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kwenda sokoni nikanunua mchicha vicha viwili shilingi elfu moja, nikanunua fungu tungule shilingi elfu moja imekuwa shilingi elfu mbili, nikanunua na mkaa shilingi elfu moja shilingi elfu tatu, nikanunua na mchele wangu wa mapembe shilingi elfu mbili elfu tano imemalizika, hizi shilingi mia sita na kumi na tatu nimejaribu kununua chumvi, sasa hapa sijapata nazi na sijapata chochote na huo ni mlo mmoja tu na hivyo ni vyakula vya maji vyote. Lakini ukiangalia ukuwaji au uhai wa mwanaadamu kutoka miaka 50 mpaka 60 kwa mtu wa Zanzibar hatofikia hapo kwa hesabu za haraka haraka inategemea hapa kuwauwa wananchi wetu haraka sana na wananchi hawa kwa nini watakufa kutokana hawana lishe *nutrition* watakuwa hawana.

Niombe serikali sana na hii ni kwa sababu ya bajeti yetu lakini ukija kwenye *IMF* wanasema mtu aishi chini ya dola moja. Sasa kwa Zanzibar hii itakuwa ndoto sana Mhe. Mwenyekiti. Naomba tu serikali kuwafikiria watu wake. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda kwenye Ugatuzi. Ugatuzi huu tumeupeleka chini lakini mimi nilikuwa sioni Mhe. Waziri labda utrakapokuja uniambie viashiria vya uchumi vikoje huko chini hatupati kuviona katika hizo wilaya ambazo tumezigatua bado hatujapa kuviona viashiria vya uchumi.

Lakini vile vile mchango wa taifa katika *D by D* ukoje hatupati kuuona labda wewe Mhe. Waziri utakapokuja uniambie pato la taifa litapatikana vipi katika *D by D* angalau tuweze kuona jinsi gani tunakwenda.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika ukurasa wa 35 wa kwenye kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri ambacho ninaomba ninukuu kidogo:

> "Kupunguza unafuu wa kodi ili kulinda vya ndani. Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa ikitoa nafuu ya ushuru wa forodha na kodi nyengine kwa uingizaji wa bidhaa muhimu na chakula kama vile mchele, unga wa ngano, sukari. Hata hiyo, kufuatia kuimarika uzalishaji nchini kupitia kiwanda cha unga wa ngano cha *Zanzibar Milling Corporation* na kufufua kiwanda cha Mahonda imejitokeza haja ya kupunguza unafuu unatokana na uingizaji wa bidhaa hiyo muhimu".

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nimeanza kupata ukakasi sana juu ya upunguzaji wa kodi. Moja Mhe. Mwenyekiti, katika hili kupunguza kodi kwa sababu kodi yenyewe hapa wanalipa asilimia kumi. Sasa hii tenda tuanze kuipunguza na hasa kwa viwanda vilivyosemwa hapa. Mheshimiwa niseme tu niliwahi kufanyakazi kwenye Kampuni ya *Mkunazini General Trade* ambayo ndiyo iliyokuwa ikileta *Oman Flour Mills* Unga wa ngano wa Oman ndio iliyokuwa ikileta. Mara moja hapa tulikuwa tukileta unga Bakharessa akashusha unga wake, lakini tuliposita kuleta unga yeye akaja kupanisha kwa elfu kumi nzima. Tizama pato hili linavyoumia kwa mwananchi wa kawaida anaumia kiasi gani.

Sasa je, leo tuseme hii ngano inapoingia kwenye kiwanda hichi hailipwi kodi hata senti tano maana yake ni mali ghafi. Lakini nimekwenda kuangalia dukani nimepita yeye anauza unga elfu arubaini na nane kwa mfuko wa kilo hamsini. Lakini vile vile hawa wa kawaida wanaoeleta nje makampuni yanayoleta unga nje yanauza kwa shilingi hamsini na nne, kuna *diference* ya shilingi elfu sita hii hapa yeye amekwenda vizuri.

Sasa tuzidi kumpungiza tunaanza kusababisha *monopoly*. *Monopoly* hii imeanza kuingia kwenye meli sasa hivi hakuna meli yenyewe hakuna boti hata moja ya muwekezaji wa kawaida tumeanza kuingia kwenye *monopoly* na huku kwenye unga tunataka kuingia kwenye *monopoly*.

Lakini nizungumze kwenye suala zima la kuweza kuwaajiri nimeangalia uajiri wake nimekuta kuna wafanyakazi wa moja kwa moja hamsini, lakini hawa wafanyabiashara ambao wanaleta wanafanyakazi sitini ambao wale wa moja kwa ndani mbali kuwa na wale wachukuzi kule bandarini.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri hili kulifikiria sana tusije tukasababisha hofu kubwa kwa wananchi wetu ongezeko la unga wa ngano, ongezeko la vifaa vyengine ni kuangalia kodi hizi zinatosha naziweke kama zilivyo hapa hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye Kiwanda cha Mahonda, Mhe. Mwenyekiti kiwanda hichi Mahonda nacho pia kinatakiwa kiangaliwe jinsi gani tunaweza kwa sababu wanasema *operation cost* zinaendelea kuwa kubwa, lakini *operation cost* zikoje. Je, ule mtaji wao ndio wanaotia kwa mwaka unakuwa *operation cost* zinaongezeka au inakuwaje nitataka kujua kitu hichi kinakuwaje vipi. Vile vile, kama uzalishaji ni mwingi kwa nini serikali isipige kifua sasa kuweza kuwapatia *market* ya kudumu kwa sababu huwezi kuwa na viwanda kama hujafanya *market research*. *Population* yetu hatuwezi kuzalisha au kununua vitu vingi, lakini tuiangalie umasikini wa Zanzibar bado hatujafikia katika uchumi wa kati na hii kwa nini hatujafikia uchumi wa kati hatujaweza kumtayarisha mwananchi kufikia katika uchumi wa kati.

Mwananachi wa Zanzibar leo anashindwa kwenda hata *super market* kununua *sausage* akanunua mayai anashindwa anakula mlo kama niliousema shilingi 5000 kwa siku haiwezekani mwananchi huyu akaweza kule chini. Kwa hivyo, tuitayarishe Zanzibar ifike uchumi wa kati na wananchi wake waweze kuweza kutumia ndio tutakwenda vizuri katika viwanda hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, napingana moja kwa moja angalau wenzangu wamesema lakini ushushwaji wa kodi na upunguzwaji nafuu katika viwanda hivi vya unga mimi nipingane navyo moja kwa moja. Mhe. Mwenyekiti, nioneshe hisia zangu kubwa kwa wananchi kuwa wataumia na bei itazidi sana ya unga wa ngano hapa nchini, naisihi serikali yangu ya Chama changu cha Mapinduzi ijarabu kuona hali itakavyokuwa kwa wananchi wake na ninaimini sana hili lazima italiona kwa unafuu huu. Lakini kupoteza ajira kwa watu wengi ambao watakuwa wanaleta vifaa vile.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee kwenye ukurasa wa 36 muelekeo wa matumizi. Mhe. Mwenyekiti, serikali imekadiria kutumia jumla shilingi trilioni 1,300.3. Kwanza naipongeze serikali yangu sana kwa kazi kubwa inayoiona kwa kuona uchumi wetu unaweza kukuwa na matumizi sasa yanazidi serikali. Mhe. Mwenyekiti, niseme tu uzuri wa serikali yetu na bajeti yetu yote

inaelekea kwenye maendeleo kwenye maendeleo na ukiona Mhe. Mwenyekiti fedha za maendeleo zimekaribia kufikia asilimia 50 ujue hio ndio serikali ya wananachi na hiyo ndio bajeti ya wananachi.

Sasa nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango hii imefikia asilimia 43 pesa za maendeleo. Kwa hivyo, tunasema bajeti hii itaenda kwenda kumtumikia mwananchi moja kwa moja niipongeze sana serikali yangu kwa kazi kubwa hii ambayo inaweza kuifanya. Lakini vile vile Mhe. Rais amesema alipoingia madarakani na siku ya mwanzo anahudumia atakusanya mapato na katika MKUZA kufikia asilimia 8 mpaka 10 sasa safari hii tumefika mpaka 8 nasema asilimia 8 niseme tu Mhe. Waziri *big up*, lakini Mhe. Hamza Hassan Juma alisema ana haki ya kutununikiwa uprofesa na mimi nakwambia tu kwamba ni kweli unayo *PHD* na ndio maana ukaandika, lakini maandiko yake hasa kama hujaandika maandiko mengine hata hii bajeti inatosha sasa wewe kuanza kupewa uprofesa.

Sisi kuanzia leo tunataka tukupe uprofesa kama tulivompa Mhe. Ali Mzee Ali hapa kwa sababu bajeti yako nzuri na umefanya vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuna *Join Financial Commission* nataka nisome Katiba hii ya Tanzania Mhe. Mwenyekiti kwenye kifungu cha ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zimebakia dakika tano.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nitajaribu kwenda haraka sana. Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Tume ya Pamoja na Fedha.
Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha, ambayo inasema hivi:

> "Kutakuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha yenye wajumbe wasiozidi saba ambao watateuliwa na Mhe. Rais kwa mujibu wa ibara hii na masharti ya sheria itakayotungwa na Bunge".

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na ukakasi mkubwa sana kuweza kuona tume hii inafanya kazi gani nilienda kutembelea pale na mipango mingi sana, lakini tume hii imejaribu kutoa mapendekezo mengi sana lakini serikali zetu mbili bado hazijaweza kuyafikia malengo haya Mhe. Waziri utakapokuja ningeomba tu uniambie ni sababu zipi labda tume hii imekwama kwenye kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala nyengine, nikipingie katika miongoni mwa hatua za mapato ambazo 17/18 pamoja na kufanya marekebisho yenye Sheria ya Ajira na mamba 11 ya mwaka 2015 ambayo yametekeleza kuwa malipo yote ya mishahara kufanyia kupitia *account* za benki za waajiriwa. Kimsingi ni hatua nzuri sana katika kuimarisha mapato pamoja na kuhamisisha wananchi kujiwekewa hakiba katika *account* zao, hata hivyo hatua hiyo imekuwa na usumbufu kwa wananchi kutokana na uchache wa huduma za kibenki wakati wa siku za mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ni shuhuda mkubwa sana umeona watu katika benki utaoambiwa *network* hakuna wanasumbuka wanafanya hivi kila wakati imekuwa tatizo tungeomba kituo hichi kwenye *PBZ* angalau kiwekwe sawa. Hatua nyengine ni kuimarasha mapato ya 2017/2018 ni kutungwa kwa Sheria Ushuru wa Bidhaa pamoja na Ushuru wa *Stemp*, Kamati ya Bajeti ilipendekeza kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria hizo ili wazifahamu kwa upana naomba kufahamu utekelezaji wake na mapendekezo ya kamati ya bajeti umefikiwa wapi. Mhe. Waziri atakapokuja naomba niambie kidogo basi amefikia wapi kuhusu mapendekezo haya.

Vile vile, jambo la kupongeza kutokona na kuongezeka kwa bajeti ya serikali ambyo imepungua utegemezi wa nje tunasema siku zote Ilani ya Chama cha Mapinduzi ndio ilani yenye kutekeleza na tumeona bajeti hii na bajeti halisia nimeisema imepunguza utegemezi. Kwa hivyo, nawaomba wananchi sana kuingua mkono hususan katika maeneo ya miradi ya maendeleo hicho kitu kitapendeza sana niseme tu mwenyekiti na ndio uzuri wa bajeti.

Lakini uzuri wa bajeti yetu kutotafsiriwa kwa nyongeza na namba sio namba pekee ambayo inaweza kutafsiri lakini tumeona bajeti yetu inatafsiriwa kwa vitendo hii jambo jema sana Mhe. Mwenyekiti, hakuna bajeti au nchi nyingi zinaenda kwa namba tu tunaweza tukaletewa hapa *trillion* 6, lakini katika matumizi mengineo yaliyopita tumenda na fedha za maendeleo asilimia 96 sasa hii ndio bajeti inayotekelezwa kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwa kuwa uendeshaji wa sekta ya utalii ni sehemu ya vipao mbele vyetu ambavyo tumeviekea lakini tunataka tuende mbele zaidi Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kuna utalii wa aina nyingi tu tusiendelee kwenye utalii wa fukwe tuweze kupamba nyingi sana katika elimu, lakini vile vile katika afya tuendelee na utalii kama huo.

Mhe. Mwenyekiti nikushukuru sana kwa kunipa nfasi hii na kutumiza dakika zangu lakini niseme tu naunga mkono kwa asilimia mia bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ashante nakushukuru sana Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na muda kama utaturuhusu basi Mhe. Miraj Khamis ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamis: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuweza kuichangia hotuba hii ya bajeti kuu ya serikali ambayo iko mbele yetu. Lakini awali kabisa niweze kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na watendaji wake wote kwa kuweza kuiwasilisha ripoti hii ambayo kwa kweli tunafarajika nayo. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji wa ripoti yao kwa kweli ripoti yao pamoja na kwamba Mwenyekiti amesimama na kuweza kutia nyalio, lakini ripoti ili kwa kweli kama itazingatiwa imezingatia mambo mengi sana. *(Makofi)*

Niwashukuru vile vile wajumbe wenzangu ambao wametangulia kuweza kuichangia hotuba hii wamechangia mengi sana na kadri tunavyokwenda tunahisi kama tunarudia rudia lakini tuna haki ya kuweza kufanya hivyo ili kuweza na sisi kuweza kutilia mkazo.

Mhe. Mwenyekiti, wachangiaji walipita wamesifu sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wao, lakini Mhe. Mwenyekiti Waswahili wanasema mgema akisifiwa tembo hulitia maji, ingawa mimi si fikirii kama Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango anaweza akalitia tembo maji kutokana na sifa ambazo amepewa, isipokuwa imani yangu kwamba ataongeza bidii zaidi katika kuona kwamba hali ya makusanyo ya mapato ya serikali hii na kuweza kukuza uchumi wa nchi hii yanaendelea mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nina maeneo machache mno kwanza niweze kuisifu bajeti hii ambayo imewasilishiwa kwetu, ninaita kwamba ni bajeti ya matumaini na ni bajeti ya matumaini kutokana na viashiria mbali mbali ambavyo tunaviona, kwanza bajeti hii inaelezwa kwamba hakuna ongezeko la kodi hii ni faraja kubwa sana kwa wananchi wetu kwa sababu kodi ni moja kati ya mambo unapoyaongeza maana yake unaongeza ukali wa maisha kwa mwananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Vile vile, tunaelezwa kwamba bajeti hii kwa kiasi kubwa itakuwa imepunguza ule utegemezi wa bajeti. Sasa hii inaipa heshima kubwa sana nchi yetu kwani kadri bajeti inapokuwa na upungufu wa nakisi maana yake uchumi wa nchi na heshima ya nchi inaongezeka. Lakini tunaambiwa vile vile mategemeo ya ongezeko la mapato hii inaashiria vile vile kwamba hali ya uchumi itakuwa imepiga hatua na kwa maana hiyo hata kipato cha mtu mmoja mmoja kinaweza kuongezeka.

Lakini chengine kinacholeta faraja ni ile *projection* ya mfumuko wa bei za bidhaa ,mbali mbali tunataka kuweza kudhibiti na tubaki na tarakimu moja hichi nacho ni kiashiria tosha cha kuweza kuisema kwamba bajeti hii ni bajeti ambayo ya matumaini sana kwa wananchi wetu inaweza ikawaletea unafuu wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka katika kuitaza bajeti kwa uhalisi wake na kadiri inavyoleta matumaini sasa nieleke katika suala zima la mazingatio maalum ya serikali Mhe. Mwenyekiti nilikuwa niaangalia mazingato maalum ya serikali katika bajeti ya 2017/2018, Mhe. Mwenyekiti katika maeneo maalum kuna baadhi ya maeneo ya mazingatio maalum Mhe. Mwenyekiti tunashindwa kuona utekelezaji wake ukoje, lakini vile vile katika baadhi ya maeneo maalum yanaonekana kujirudia rudia yale 2017/2018 na katika bajeti hii 2018/2019 lakini hata zile *statement* zake azioneshi kwamba eneo lile ni muendelezo wa lile ambalo limepita.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atakapokuja basi atushibishe kidogo juu ya yale maeneo maalum yanayozingatiwa na serikali. Kwa mfano, kuna suala la uimarishaji wa maakazi ya askari wa Idara Maalum hili eneo mwaka uliopita uliidhinisha hapa shilingi bilioni 1.6 lakini hali ya utekelezaji wake ikoje, tunataka kujua ili kuweza kujitathmini kwamba yale maeneo ambayo tuliyaweka basi yako vipi utekelezaji wake umekwenda. Lakini tulisema kwamba tuaanzishe bima ya afya na tulidhinisha hapa shilingi bilioni 2, basi ni vyema Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango akija atwambie utekelezaji wake tumeidhinisha bilioni 2 kwamba tutanzisha mfuko wa bima ya afya tumefikia wapi.

Tumesema vile vile kuongezwa kwa bajeti ununuzi wa dawa, chanjo na vifaa tiba ambapo tuliidhinisha shilingi bilioni 8. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango atakapokuja atuambie tumepiga hatua kiasi gani baada ya kuidhinisha fedha hizo. Je, tatizo la dawa limepungua kwa kiasi gani, suala la chanjo liko vipi, vifaa tiba viko vipi, kwa sababu

wakati mwengine wananchi wanalalamika juu ya upatikanaji wa dawa lakini tayari hili eneo ilikuwa ni eneo maalum sasa tulitarajia kwamba katika kitabu cha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango tuweze kuona kwamba tumefikia wapi katika haya maeneo ambayo tumeyaita maalum. *(Makofi)*

Vile vile, katika eneo jengine maalum kutoa fedha za mtaji kwa Wakala wa Uchapaji, tumefikia wapi tuliweza kuidhinisha shilingi bilioni 1.5. Je, hali ikoje, tumeweza kutekeleza hilo na je hivi sasa wakala anaendelaje wa uchapaji. Lakini tulizungumzia juu ya kuimarisha usafiri katika visiwa vidogo *land craft* kulikuwa na shilingi bilioni 0.8 katika mwaka 2018/2019 vile vile tumeweza kutenga bilioni 2.4 ununuzi wa *land craft,* sasa Mhe. Waziri atueleze ile 0.8 bilioni ilitumika kwa nini na hii 2.4 imelezwa hapa kutakuwa na ununuzi sasa ile ya mwaka jana nini ambacho tulikifanya zaidi.

Lakini vile vile tulisema kwamba tutaanzisha mfuko wa elimu ambapo tuliidhinisha shilingi bilioni 2.5 tumefanikiwa kiasi gani katika hili kumalizia ujenzi wa Skuli za Sekondari JKU tumefikia wapi tilitenga bilioni 1.3 na hivi sasa ukipita unakuta jengo lile halijamaliza na *statement* ilisema kwamba kumalizia ujenzi kwa fedha sasa tumefikia wapi. Vile vile tulisema kwamba umaliziaji wa madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi ambapo hapa kulikuwa na bilioni mbili ambazo ziliidhinishwa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo haya ni mengi kwa mfano katika mwaka huu kwenye matumizi ya mfuko wa miundo mbinu imeleza hapa kwamba tutaendeleza visima vya Ras-el-Khaimah, lakini katika maeneo ambayo tuliyataja katika mwaka uliopita tulisema kwamba kumalizia visima vilivyojengwa kwa msaada wa Ras-el-Khaimah ambapo shilingi bilioni 2 zilitengwa. Sasa hizi *statement* zinasutana kwa ufupi mwaka jana tulisema kumalizi visima vilivyojengwa kwa msaada wa Ras-el-Khaimah mara hii tunasema kuendeleza sasa napenda kidogo kuwekwa wazi hapa ili tuweze kuona iko vipi.

Kuna ununuzi wa mitambo ya lami ambapo tuliidhinisha shilingi bilioni 2.5 tumefikiwa wapi tumeweza kuinunua mitambo ya lami pamoja na vifaa vya barabara, vile vile tulikuwa na eneo jengine muhimu wa ujenzi wa Mahkama Kuu ya Tunguu ambapo kuna shilingi 0.9 bilioni, Mhe. Waziri atueleze hivi sasa tunapita tunaona eneo limefyekwa lakini je ili 0.9 bilioni ilitumika kwa ajili ya kulisafisha eneo tu au kuna shughuli nyengine ambazo zimefanya, kwa sababu hivi sasa tayari tumetenga pesa nyengine kwa ajili ya uendelezaji wa jengo hilo. *(Makofi)*

Sasa nishauri tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba katika tunapozungumzia haya maeneo maalum basi iwe yanatolewa thathmini kutoka bajeti iliyopita kuelekea bajeti hii na kwa yale maeneo ambayo yanaonekana kujirudiarudia basi zile *statement* zake zioneshe kwamba ni muendelezo, lakini vyenginevyo inakuwa kidogo zinatuchanganya tunapopitia hii.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee sasa katika Mfuko wa Miundombinu. Mhe. Mwenyekiti, kwenye mfuko huu katika kitabu hiki tunaona mambao yanakaribiana na yale miradi ya kujirudia rudia, ni vyema kuwa wawazi kwa ile miradi ambayo ilitekelezwa isemwe kwamba imetekelezwa na miradi ambayo inajirudia basi ionekane kwamba inajirudia.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, tuangalie uimarishaji wa Taasisi za Viwango. Katika uimarishaji wa taasisi za viwango katika bajeti ya mwaka 20172018 zilitengwa shilingi bilioni mbili, lakini mwaka 2018/2019 vile vile kuna shilingi bilioni mbili. Je, mwaka uliopita pesa hii haikupatikana au ni mwendelezo wa mradi huu wa uimarishaji wa taasisi ya viwango. Mhe. Waziri atakapokuja atueleze.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna eneo la uimarishaji wa Elimu Mbadala mwaka 2017/2018 kulikuwa na shilingi bilioni 1.6, lakini mwaka 2018/2019 kulikuwa kuna shilingi bilioni 1.6. Kwa hivyo, vile vile tuweze kuona ni muendelezo au ni kitu kipya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna programu ya Upatikanaji wa Rasilimali Fedha mwaka 2017/2018 kulikuwa kuna shilingi bilioni moja, na mwaka 2018/2019 kulikuwa kuna shilingi bilioni moja. Je, hii pesa haikupatikana au ni mwendelezo wa programu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuondoka hapo nije sasa katika kitabu cha Mhe. Waziri cha mwelekeo wa hali ya uchumi mwaka 2018/2019. Nielekee katika suala zima la ajira kwa vijana. Mhe. Mwenyekiti, nafarajika sana na naipongeza sana serikali yetu kwa kuweza kufikiria suala zima la ajira kwa vijana. Suala la ajira kwa vijana Mhe. Mwenyekiti, ni changamoto kubwa na sio kwa nchi yetu tu, lakini hata kwa nchi ambazo zimeendelea.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wana tatizo kubwa sana la ajira na katika bajeti kwenye wizara inayohusika tuliona kwamba serikali imetenga karibu ya shilingi bilioni tatu kuweza kutekeleza programu hii ya ajira. Mhe. Mwenyekiti, katika programu hii inasema kwamba, kuwawezesha vijana wa rika na elimu tofauti kupata ajira katika maeneo mbali mbali, yakiwemo kilimo cha mboga mboga, ufugaji wa kuku, samaki, eneo la viwanda ikiwemo usarifu wa matunda na mboga mboga, useremala, ushoni, eneo la mazingira ikiwemo huduma za usafi wa miji na manispaa na kuwajengea uwezo kwa kupitia fani mbali mbali za sanaa na michezo.

Mhe. Mwenyekiti, hili jambo ni bora sana, ni jambo zuri na mimi naliunga mkono. Lakini kabla ya utekelezaji umakini unahitajika. Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba vijana wetu unaweza ukawaingizia fedha na ukawapa taaluma ya nyanja mbali mbali ambazo zimesemwa hapa, lakini ukweli ni kwamba kuna nyanja moja lazima izingatiwe kabla ya utekelezaji wa programu hii. Vijana wetu kwa kiasi kikubwa wana dhana ambayo inapaswa ibadilike. Vijana wetu *mindset* zao ziko zaidi katika za kuajiriwa na sio za kujiajiri. Sasa programu hii inawalenga sana vijana wajiajiri, lakini *mindset* za vijana wetu ziko katika kuajiriwa zaidi.

Sasa mafikiri programu hii ianze na taaluma na elimu kubwa sana ya kuweza kuwabadilisha vijana wetu, ili waondokane na mawazo ya kuajiriwa na waelekee katika mawazo ya kujiajiri wenyewe. Tukiliweza hilo basi na haya mengine yanaweza kufuata, lakini kama hatukuliweza hilo la kubadilisha *mindset* za vijana wetu, basi nafikiri tunaweza kupoteza pesa nyingi, lakini vijana wetu wasiweze kuingia katika ajira, sasa hili ni tatizo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, ningeweza kutoa ushauri. Kwa mfano, vijana wetu wanaohitimu vyuo vikuu, hizi taaluma za ujasiriamali nafikiri zingeanza katika programu za vyuo vikuu, ili hata wanapokuja kwenye uraia huku basi tayari wamekwisha kubadilika na kama utawapa mtaji basi wanaweza kufanya lolote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliopita walizungumzia masuala mawili muhimu sana. Moja ni suala la msamaha wa ushuru, lakini vile vile la pili ni suala la kupunguza unafuu wa kodi ili kulinda viwanda vya ndani. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linataka umakini mkubwa sana, linataka mazingatio makubwa sana, tusije tukafanya makosa. Katika suala la viwanda vyetu vya ndani, tuhakikishe kwamba viwanda vyetu vinazalisha bidhaa ambazo zinatosheleza mahitaji ya Wazanzibari kabla ya kuweza kuondosha ule msamaha wa ushuru wa bidhaa muhimu za lazima, hilo lazima tuhakikishe. Tusipohakikisha hilo halafu tukajakuondosha ule ushuru wa bidhaa muhimu, basi tunaweza tukajakuwaweka wananchi wetu njia panda.

Kwa hivyo, naomba kusisitiza tu umakini unahitajika sana tusije tukavipunguzia kodi viwanda hivi, lakini kumbe uzalishaji wao haukidhi mahitaji ya Wazanzibari, Wazanzibari tutakuja kuwapa wakati mgumu sana, watakuja kuzinunua bidhaa kwa bei kubwa sana kwa sababu patakuwa hapana ushindani. Wakati mwaka huu uliopita tumeweza kutengeneza hapa Sheria inayohusiana na Ushindani Halali wa Kumlinda Mtumiaji. Sasa sheria ile tuizingatie na haya maamuzi ambayo tunatarajia tuyafanye.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikija katika suala zima la msamaha wa ushuru wa bidhaa muhimu. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, suala hili bado halijakaa vizuri sana tunawapa watu msamaha wa ushuru wa bidhaa, lakini bado wananchi Wazanzibari hawajanufaika vizuri na msamaha huo. Tumeona mwezi wa Ramadhani uliopita hapa, wafanyabiashara tumewapa msamaha wa ushuru wa bidhaa, lakini je kama tumefanya tathmini tumeweza kuona kweli wananchi wamepata unafuu ule uliotarajiwa, nafikiri hatujafikia lile lengo. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango akae na Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda ili kuweza kuliratibu vizuri suala hili, kwa sababu tuweze kuona ni tani ngapi hasa Wazanzibari wanahitaji za sukari, unga na za mchele katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Lakini jengine ni nani na nani hasa waweze kupewa msamaha huu na bidhaa hizo ziingie wakati gani. Kuna watu wanaingiza bidhaa hapa karibu na mwisho wa mwezi wa Ramadhani na wamepewa msamaha, maana yake unawatajirisha zaidi wale wafanyabiashara kuliko kuzingatia yale maslahi na yale malengo ya nchi hii ambayo yametarajiwa katika kuweza kuondosha au kupunguza ushuru huu.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, suala la msamaha wa ushuru wa bidhaa muhimu linahitaji kukaliwa kitako, ili tuweze kuona kwamba wananchi wa Zanzibar wananufaika na hilo na sio kuwatajirisha wafanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia suala zima la udhibiti wa bei. Udhibiti wa bei kwa kweli bado hatujafikia yale malengo ambayo tumeyakusudia. Kunahitajika kuweze kukaa na kuweza kuzingatia hasa na vyombo vinavyohusika kuweza kuona kwamba kuna udhibiti wa bei za bidhaa, ili kuweza kupunguza ule mfumko wa bei za bidhaa kama tunavyotarajia, ili tuziweze kuingia katika tarakimu mbili tubaki katika tarakimu moja. Lakini je, hali ya usimamizi ikoje, taasisi zinazohusika sheria zikoje ili kuweza kuona kwamba unafuu unapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naipongeza sana hotuba hii ya Mhe. Waziri kama nilivyotangulia kusema, ni bajeti inayowapa matumaini wananchi na kama ni kweli msingi hii na

haya tuliyoyaweka humu yatasimamiwa vizuri, basi ina imani kwamba uchumi wa Zanzibar utafikia ile *projection* tunayoitaka ya asilimia 7.7. Kwa tafsiri hiyo, nchi hii itakuwa imekaa vizuri na unafuu wa maisha kwa wananchi wetu utapatikana. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii ya bajeti kwa asilimia mia na nawaomba wenzangu na wao waichambuwe na waichangie, ili kuweza kumpa moyo Mhe. Waziri kuweza kuendelea na yale malengo aliyojipangia ili kuweza kuona nchi hii inapiga hatua za kiuchumi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, kama muda utaturuhusu basi nitampa nafasi Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame: Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuchangia machache katika hotuba mwanana ya bajeti ya serikali kama ilivyotolewa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yake kwa kitabu kifupi lakini kilichojaa falsafa, kilichojaa takwimu. Maana yake takwimu unaweza kuziweka kwenye majadweli, lakini unaweza kuzitia kwenye *text* na zikafahamika. Kwa hivyo, tunampongeza sana Mhe. Waziri, kwa kweli takwimu alizozitaja zina-*flow* nzuri na zinafahamika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi kwa Mhe. Waziri na timu yake naomba ni-*quote* wenyewe wanaita *quote of the week* katika gazeti la *Sunday News* la jana. Sasa nimejaribu kutafsiri kwa Kiswahili kama ifuatavyo; Anasema;

> "Maendeleo ya nchi yoyote yanapatikana kutokana na uchumi wa nchi ambao unamuelekeo wa kujitegemea, kwa hivyo nchi zinapaswa kupanga mikakati madhubuti kufikia lengo hilo. Hakuna mtu kutoka nje atakayekuja kutumiminia mapesa kwa maendeleo yetu, lazima tufanye kazi kwa bidii kwa kupata maendeleo yetu. Pia nchi ikijitegemea inakuwa na heshima yake na kamwe haitoyumbishwa na ukoloni mamboleo".

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka kwenye mabano kama nilivyoitafsiri kwa Kiswahili iko kwenye Kizungu kwenye gazeti la *Sunday News* la jana. Kwa muono huo Mhe. Mwenyekiti, nilijaribu sana kutafuta hii bajeti yetu tuipe *theme* gani, tuipe jina gani. Mimi nikajaribu ku-*brainstorm* nikashauri. Ninamuomba Mhe. Waziri anikubalie bajeti hii tuiite bajeti ya kujitegemea na maendeleo. Naamini kabisa kwa malengo yaliomo humu ndani na mikakati iliomo ya kujitegemea na maendeleo tunayo-*focus* naamini tutafika tunakokwenda.

Kwa nini nikasema hivyo. Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumza hayo mambo ambayo Mhe. Waziri ambayo ameyataja. Nitatoa mfano, kwanza suala la umeme. Tumeamua kujitegemea kulilipa deni lote. Nampongeze Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, yeye hili deni jengine kubwa kalikuta, lakini kasema hapana mimi ndiye niliyomo madarakani, sasa kuweka heshima ya nchi yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tulilipe. Tena

alivamiwa na waandishi wa habari nakumbuka anatoka safari, sijui kama ni Vietnam vile, baada ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kutoa ile ilani, akasema basi kama deni lipo tutalilipa. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. Rais kwa ile kauli yake kwamba deni lilipwe na Alhamdulillah tumeanza kuchukua hatua za kulilipa na tumefikia pazuri tu.

Mhe. Mwenyekiti, kinachotuvunja moyo na ambacho hicho kinatu-*cost* hata kwenye kupanga bajeti yetu ya SMZ, yaani kunaonekana kuna athari kwamba wenzetu yale maeneo ambayo tunawadai hawataki kutulipa sasa kwa nini. Hili Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka huu tumeambiwa kodi ya mapato kwa kupitia Mhasibu Mkuu imetarajiwa kufikia shilingi 21 bilioni, sawa na asilimia mia moja kwa mwaka huu je, miaka ya nyuma kwa nini hatutaki kulipwa. Sasa najua kuna kamati inayoshughulikia matatizo ya Muungano, kamati ile inakaa lakini naona imekuwa muda mrefu.

Kwa hivyo, nataka kumuomba Mhe. Waziri. Unajua wanapozungumza mawaziri kwa mawaziri kunakuwa na *discipline* ya kuzungumza, lakini *backbenchers* sisi huku inakuwa kidogo wakati mwengine tunakwenda *straight to the point*. Sasa ningemuomba, sio kwamba na wao hawaendi *straight to the point*, lakini ile lugha laini *backbenchers* wakati mwengine hawana. Kwa hivyo, nataka kumuomba kikao kijacho chagua timu ya kwenda kukusaidia kwa suala hili, kwa nini maana yake wenzetu walitukaa wee deni la umeme, tumeamua kulipa na tunaendelea vizuri. Sasa kwa nini wenzetu madeni yetu hawataki kulipa, inaonesha wazi hawataki tu. Maana yake sasa hivi huu sijui mwaka wa ngapi tunazungumzia kitu hicho hicho.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aunde timu hasa tuko tayari twende tukaonane na Mhe. Waziri wa Fedha au hata na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili tuwasilishe hoja yetu, hii ni hoja kwa sababu kwa kweli inaathiri sana mipango yetu ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, napongeza sana kama nilivyosema bajeti hii ambayo tunaiita ya maendeleo na kujitegemea, kwa sababu kuna vitu ambavyo lazima kwa kweli tuvipongeze. Kwa mfano, suala kubwa la malipo kwa wastaafu, bajeti ya serikali yetu tunaigharamia wenyewe ya *OC*, lakini zaidi wastaafu nao sasa wanalipwa kwa wakati, tena vizuri zaidi ile *take home* ya wastaafu imeongezwa yaani imeboreshwa lakini yote tunailipa. Kwa kweli hili ni suala la kupigiwa mfano sana.

Mhe. Mwenyekiti, gharama za elimu kuanzia msingi mpaka sekondari, sasa tumesema hakuna malipo. Haya ni mafanikio makubwa kabisa ambayo ni lazima tuipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunasema watu wa mipango na wa fedha hawakai pamoja, maana yake kila mmoja anaona yeye ndio mkubwa zaidi wa muhimu. Lakini mimi niwapongeze sana chini ya Mhe. Waziri mwenyewe, timu ya mipango na timu ya fedha wanakaa pamoja huku kwenye *resources* na huku kwenye mipango na wanakwenda vizuri tu na matunda yake tunayaona.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ununuzi wa vifaa au dawa na vifaa tiba ni suala la kupigiwa mfano sana, vipi serikali inavyowajali watu wake. *Bill* hii imeongezeka mara tatu au asilimia mia moja.

Sasa pesa imeshapatikana na imeshatengwa, lakini suala ununuzi ukoje, hapa ndio kwenye kizungumkuti. Mhe. Mwenyekiti, naomba kushauri sana na ninamuomba Waziri wa Fedha na Mipango ajaribu sana kufuatilia hii *procurement system* ya dawa hatumuoneshei mtu kidole, lakini tatizo liliopo wale wanaolipwa wanalipwa pesa kamili, lakini ujaji wa dawa unakuja matoro toro tu, leo unakuja ah! Asilimia 3, kesho 4, keshokutwa 5, wakati pesa wameshalipwa. Matokeo yake kwetu huku wanasababisha mapungufu makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, hili namuomba sana Mhe. Waziri Fedha na Mipango au kwa ujumla Wizara ya Fedha na Mipango ilifuatilie tuone hasa suala la *procurement system* ya dawa na mambo yake yanakwenda vizuri na tusiwe tunakwama katika manunuzi ya kitu hiki muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti kama nilivyosema imeandikwa vizuri sana ukijaribu pakupenya unapatafuta. Lakini nataka nizungumzie suala la usimamizi wa kazi zetu, nimefurahi sana nimesoma kitabu cha *Guidelines Monitoring and Evaluation Framework* ya Zanzibar *Strategic for Growth and Deduction Poverty III* kimeeleza vizuri sana jinsi ya *MKUZA* unavyotekelezwa na unavyosimamiwa. Kwa kweli, kimeelezwa vizuri na hasa *role* walionayo Wakurugenzi wa Sera na Mipango na Utafiti hawa ni watu muhimu sana kwa kushirikiana na watu wa takwimu, kwa kushirikiana na ofisi na watu wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa ujumla nataka kusema, ukiangalia hawa Wakurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti wenye jukumu kubwa la kusimamia mipango sera na utafiti wao ni kama *dictionaries* wa wizara hii kazi asilimia ndogo wanaifanya najua kuna maofisa wao, lakini kwa kweli wao ni kama roho ya wizara, wizara zote bajeti *speech* mwenye Mkurugenzi Mipango, Bango Kitita mwenye Mkurugenzi Mipango, ikitokea kazi kubwa mwenye Mkurugenzi Mipango, najua ana timu yake.

Mhe. Mwenyekiti, *point* ninayotaka kuileta ni kwamba ile kazi *monitoring and evaluation* ifanywe ipasavyo, tuone tunakwendaje, tumefika wapi, tujitathmini tusingoje mpaka Mhe. Rais, anaitisha Bango Kitita watu ndio wanakurupuka, mbio wana-*compute data rather than* matokeo ya zile pesa zilizotumiwa. Lakini zaidi Mhe. Mwenyekiti, kule *field* wewe shahidi mwenyewe, kamati yetu pamoja tunapokwenda *field* tunayaona yale mambo yaliyokuwepo kule, kwa kweli kuna mapengo mengi ambayo kama kunatasimamiwa vizuri na kana mtu anafuatilia kule *field* basi naamini baada ya kipindi pale pale imetokea athari basi inakaribishwa.

Mhe. Mwenyekiti, hili ningeomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kile Kitengo cha *Monitoring and Evaluation Secretariat* kiliopo kwenye *MKUZA* akiimarishe sana, na akipe pesa, na atoe mapitio yake kila baada ya muda waseme je, tumefikia wapi, kuna tatizo gani.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa tulionalo pesa *Alhamdulillah* mwaka huu tumeipanga vizuri na tume–*locate* vizuri karibu katika maeneo muhimu sana, ya elimu, maji, ambayo Waheshimiwa wengi wamezungumza, suala la maji ingawa haikuzungumzwa sana humu, lakini kwenye sekta yenye limezungumzwa kwa undani zaidi. Kwa kweli suala la maji sasa kwetu sasa ni siasa, kama ilivyokuwa chakula basi na maji nayo ni siasa, kwahivyo lazima tulikabili ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, leo tu naomba nichomekee juzi nilikuwa nazungumza na Mhe. Waziri wa Maji, tunampango wa kupata pampu nyengine moja kule Dimani basi hiyo moja iliyokuwepo

ndio roho yetu nayo imeshakufa, imeshakufa kabisa. Kwa hivyo, ndio hilo lilosemwa suala la *Monitoring and Evaluation* kwenye miradi yetu, kwenye kazi zetu, ufualiaji na tathmini, suala la maji ni suala la msingi sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri hebu twendeni kwa awamu, twendeni kwa awamu, hebu leo mfano tusingoje kukalala kote, leo tuseme tunapiga Mkoa wa Mjini Magharibi, baada ya miezi sita, tunapiga Mkoa wa Kaskazini, tunauingia hasa timu yao yote, kama wanavyokwenda kukata maji wasiolipa madeni basi wafanye hivyo hivyo. Kwa hivyo, nashauri sana Mhe. Mwenyekiti suala la maji sasa kwetu ni siasa, lazima tulipige ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikazie tena suala la serikali yetu inavyolichukua katika pesa zile ambazo tumezi–*allocate* kwenye maendeleo, lazima tutoe sifa au wahisani, au wafadhili, *Partners in Development* sio wa kutegemea kwasababu wao wana misimamo yao, wanataka lazima na sisi Zanzibar tuifate, na sisi tunasema Mapinduzi Daima. Kama tunaendeleza mapinduzi yetu na msimamo wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo napongeza sana pesa tunazotoa kwenye maendeleo bora tuwe na kitu kidogo, tugawane kidogo kidogo, nakazi iende kidogo kidogo, kuliko tunasema tunamtegemea bwana mkubwa a-*dictate* anavyotaka yeye mwende hivi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwapongeze sana, wizara kwa kujali, na si lazima maana yake miradi ile, na unajua nimepeleleza kwamba kuna miradi mpaka uwe na *external component* yaani fedha za nje, basi una–*qualify* kupewa pesa za mradi wa maendeleo, kuna miradi maana yake mradi unajaribu kukamilisha jambo ndani ya muda fulani, basi hata kama *external component* lakini tuseme, Mradi wa Maji Dimani unaupa miezi na pesa zake, halafu unaufatilia, unaukamilisha umekwisha huo, sasa utamkamata yule mtekelezaji kwanini huku tekeleza tatizo nini.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri sana, suala la usimamizi hili lazima, tulipe bajeti nzuri sana Mhe. Waziri wa Fedha, lakini suala la usimamizi kwa wizara zote, ni suala la kusimamiwa ipasavyo bado kwenye kamati zetu tumepita tumekuta *field* bado kuna matatizo ya watendaji, hakuna *link* kati ya wizara na watu walioko *field.* Sasa tumegatua, nashukuru ni lengo zuri sana tumegatua sekta ya kilimo, sekta ya afya, na sekta ya elimu *to some extent*, lakini sasa tusiwatupie kwanza yule ni mtoto tumemza tusimamie tufatilie, wanakwenda vipi bado wizara mama wanajukumu kubwa kusimamia kufanikisha lengo letu.

Mhe. Mwenyekiti, sina mengi kama nilivyosema hii bajeti ya maendeleo, bajeti ya kujitegemea nakutakia kila la kheri na naunga mkono bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa dakika 10 ambazo zimebaki nahisi zinamtosha kwa mujibu alivyoomba, basi naomba Mhe. Miraji umalizie dakika zilobaki.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, sina mengi kweli kwenye bajeti hii ya serikali, kwa sababu mambo mengi yameelezwa vizuri na naomba nichukue fursa hii kukupongeza Mhe. Waziri Dkt. Khalid Salum Mohammed, Katibu Mkuu, Baba yangu Khamis Mussa, maana mimi Miraji Khamis Mussa, Naibu Katibu Mkuu, lakini na watendaji wote, bila ya kumsahau Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, lakini niwapongeze pia viongozi wote serikali wakiwemo mawaziri, makatibu wakuu, kwa ujumla kwenye Bajeti hii ya Serikali, wametoa mashirikiano makubwa na ndio maana tukafika pahala pazuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nielekee moja kwa moja kuwapongeza, lakini pia kutoa mchango wangu katika yale mapendekezo ya hatua ya kuimarisha mapato. Katika kitabu hichi cha Muelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo wameeleza vizuri, na wametaja maeneo muhimu sana. Moja wapo likawa kufanya mapitio ya misamaha ya ushuru, katika kuhaulisha mali au *transfer of properties.*

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana serikali katika hatua hii, sababu lazima tukubali ukenda katika uekezaji hasa katika majengo yale ya hoteli, maeneo haya yanafanyiwa haya yanafanyiwa *transfer* sana lakini mfumo hasa na kufanya yale mapitio, hata katika ule uwekezaji wa zile *lease* walizopewa mpaka sasa, naomba niseme moja kwamoja hatuko vizuri, kwasababu ilivyo ainishwa hapa lakini pia nakufanywa mapitio ya viwango vya ada nimefurahika nayo, hasa katika eneo moja ambalo litatusaidia tupitie viwango vya ada katika eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tutoe mikataba mbayo inaturuhusu kufanya mapitio katika eneo la uwekezaji kila baada muda fulani, maana angalau kama tutakuwa hatuko katika uhalisia ule wa kawaida. Maana muekezaji tunaweza tukampa mkataba una miaka 90, au 35 lakini utaratibu wa mapitio wa vile viwango vile vya ulipaji wa ada zetu lazima uwe kwa hatua maalum. Kwa hivyo, katika eneo hili naomba tu moja kwa moja niipongeze serikali imefanya vizuri imeona kuna jambo jema ambalo linaweza likatusaidia katika kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niseme tena leo, liniwahi kuchangia katika kuongeza mapato kwenye Benki ya Watu wa Zanzibar. Kwa kweli, ni benki yetu lazima tushauri lile jambo jema ambalo linaweza likatusaidia kuingia katika uchumi wa kisasa. Tunajua jitihada ipo na serikali inajitahidi sana kuisukuma benki ile.

Lakini lazima tukubali bado tuko mfumo wa zamani. Mhe. Mwenyekiti, maana mfumo wa zamani na benki tulizonazo sasa, nahisi tukibadilika sisi mwanzo na zile nyengine hata zikaja zikabadilika ile kodi ya nchi na *transfer* baadhi ya maeneo tutazipata hara. Maana nikisemema Mfumo wa wazamani Mhe. waziri naongelea ile *paper money* ndio tuliyonayo, hatuko kwenye *electronic money,* maana kama tuko kwenye *electronic money* lazima sasa tuwe tunatumia *card system* hatuko huko leo hii ukenda katika nchi za wenzetu na *cash* hata kama ni ya *dollar* , nchi inatumia *dollar* hawawezi kupokea wanakwenda na mfumo huo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa sisi nchi yetu sasa hivi eneo kubwa la uchumi wetu ni utalii, tunapokea kwa asilia kubwa sana tunawalazimisha watembee na *cash* wakati sisi tukianzisha mfumo, mfumo huu tutaiwezesha benki yetu kukushanya kodi vizuri kupitia *transfer* za matumizi yao wanayoyafanya lakini katika dakika hii tuko katika *paper money* tunahangaika nayo *electronic*

money hatujaifikiria. Sasa niseme tu ule uwekezaji hivi sasa wa benki kutumia mikopo, ni asilimia ndogo sana ya kuchangia uchumi wetu. Mkopo huo mpaka unafika miaka miwili ndio unapata ile *interest* lakini eneo hili *transaction* zikifanyika vizuri basi mapato yanaenda vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini eneo jengine, niende katika matumizi ya Mkonga wa Taifa. Lazima serikali katika kupunguza matumizi ya fedha katika serikali yetu mkonga huu tuutumie, tuimarishe huduma za kuuboresha Mkonga wetu Taifa, lakini na huduma za maeneo yote ya serikali, kuwe na mkakati maalum wote wanaotaka huduma za *internet* waende kule hatuna haja sasa kwenda kutaka *service* hii tuka-*out source* wakati kile chetu hatukiboreshi, kuna haja gani ya kuvianzisha. Sasa moja katika kupunguza matumizi ya serikali tuelekeze nguvu zetu kuboresha lakini na watu wetu kuwaelekeza waelekee katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna Wakala wa Uchapaji katika pia kuongeza, naomba kutoa rai tu, kwa sababu mambo wanasema yamekwenda vizuri sinatatizo na nishaunga mkono asilimia 180, lakini naomba nielekeze katika Wakala wa Uchapaji. Wakala wa Uchapaji tunaenda vizuri, angalau unaona vitabu hivi vimechapishwa vizuri, lakini ipo dhamira ya serikali kuanzisha Bohari Kuu ya *Stationeries* ambayo tunaweza tukapunguza yale mambo mengi ambayo yanafanyika katika ununuzi wa vifaa hivi, maana vifaa vya kuandikia *stationary.*

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kama unafanya *research* kamili basi serikali inatumia zaidi ya bilioni arubaini kwenye *stationeries* hizi. Lakini, tukitumia utaratibu mzuri tutakao kwenda nao nakama tutausimamia vizuri na zile *transaction* mtu anakwenda kuchukua mzigo pesa yake tu, anafanyiwa *transfer* tu, maana hupewi ukalipe wewe, basi tunaweza tukaja hapa tukasoma bajeti haitazidi bilioni kumi, na imezidi sana basi itakuwa bilioni kumi na tano. Kwa hivyo tunapunguza matumiai ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini dhamira ile naomba tuipele pia kuna Hospitali ya Mnazi mmoja, serikali imeekeza pesa nyingi na watu wote wanalalamika karibu bilioni kumi na mbili zinakwenda pale, lakini ukenda wapo wanaolalamika dawa hukutani nayo, mimi sijawahi kulalamika, kwa sababu kipindi cha karibuni sijawahi kupita katika kutafuta huduma, lakini malalamiko haya wakati mwengine yanatengeneza taswira ya ukweli.

Sasa nako tuandae mfumo rafiki wa serikali ambao utafanya ununuzi wa moja kwa moja kwenye viwanda vya madawa, tukifanya hivyo tunaweza tukaondosha sasa huu urasimu na mgogoro na mazingira ya yale ya asilimia 10, kwa nini serikali isiingie mkataba maalum na kiwanda maalum cha uzalishaji wa madawa tukatoa ile aina ya madawa tunayoyataka na tukapokea moja kwa moja. Sasa katika kupunguza matumizi ya serikali naomba sana tuelekee kwenye eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba mwisho, nishauri katika eneo la matumizi ya *EFB* tumezungumza zamani na kila siku tukawa tunapokea ahadi mfumo huo utaanza, lakini hatuuoni, tukiimarisha mfumo wa matumizi ya *EFB* naamini tutaengeza kwa asilimia kubwa sana makusanyo katika serikali yetu, na hii kama mara hii tumekuja na asilimia tano ule utegemezi tunaweza tukafika pahala tukiende vizuri tutakuja hapa na asilimia moja.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti zile dakika zangu 10 nimezitumia vizuri naomga kuendelea kuunga mkono hoja kwa asilimia ile mia moja thamanini niliyoisema. Lakini niwapongeze sana viongozi wa wizara hii, viongozi wote wa serikali kwa ujumla wao wamefanyakazi nzuri na niwatakie kila la kheri katika kuitumikia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuendelea kuwashauri vizuri na wewe nashukuru kwa kunipa nafasi Mhe. Mwenyekiti. Ahsante, *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nakushukuru Miraji Khamis Mussa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuchukua fursa hii kwa kuwashukuru wote wajumbe wa humu Barazani kwa michango yenu. Kwa hivyo naomba niakhirishe mpaka kesho tarehe 26/06/2018 saa 3:00 asubuhi barabara. *(Makofi).*

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 26/06/2018 saa 3:00 asubuhi)